# Nipashe

Jumanne Novemba 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581137

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



JACKPOT BABA LAO!

TZS. 407,110,340

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Kocha** Simba kortini tuhuma kukamatwa na dawa za kulevya

UKURASA 3


Nipashe TESA

Jumanne Novemba 22, 2022 TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Inawezekana mifumo ya kidijitali haifai kutumika mazingira yote

Kusifia, kuwatunza wanaonengua majukwaani shuleni, asema ni kuharibu hatima ya maadili

AJALI YA BUKOBA

Injinia: Tuanze kufundisha abiria kujiokoa kwenye mwendokasi, mabasi

ELIMU

NA BEATRICE SHAYO, ALIYEKUWA MPWAPWA

Ijue shule wanafunzi wanaotembea k'mita 7, wamo wa darasa kwanza

• Wanafika hoi, wengi wageuka watoro
• Walianza 199, wamehitimu la saba 60

UKURASA 13



# CCM yafuta uchaguzi kwa madai rushwa

• **Yadai** baadhi ya wagombea mikoa, Jumuiya walitumia fedha wachaguliwe... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**DK. BASHIRU AZIDI KUMWAGIWA UPUPU**

MAKADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamezidi kummwagia 'upupu' Mbunge wa...

UKURASA WA 4

**MBARONI KWA MADAI KUMWINGIZIA CHUPA**

WATU wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Manyara kwa tuhuma za...

UKURASA WA 5

**MTUHUMIWA MAUAJI AZUA KIZAAZAA KORTINI**

Mshtakiwa Amani Filipo, anayetuhumiwa kumuua Askari wa Kikosi Cha Usalama...




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia, Nathan Belete (kushoto), wakibadilishana mikataba ya mikopo nafuu ya dola za Marekani milioni 535 (Sh. trilioni 1.24) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya nishati vijijini na kukabiliana na mafuriko katika Bonde la Mto Msimbazi, Dar es Salaam jana. Anayeshuhudia (kulia) ni Waziri wa Nishati, January Makamba. **PICHA: BEN MWAIPAJA**

## Wagonjwa walalamikia malipo kabla ya tiba Muhimbili

UKURASA 3



## Mwanga waonekana marekebisho sheria kandamizi habari

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAPANIA KUISHUSHA AZAM UK.32

**KATUNI** UK.6

# CCM yafuta uchaguzi madai ya rushwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUHUMA za rushwa katika uchaguzi wa ndani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi mbalimbali, umesababisha kufutwa kwa mchakato huo na sehemu zingine kusimamishwa katika baadhi ya mikoa.

Madai hayo yameelezwa kuwa ni chanzo kikuu cha baadhi ya wagombea kusaka kuchaguliwa kwa kutumia fedha kama kishawishi kwa wajumbe.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uamuzi wa chama hicho kufuta na kusimamisha uchaguzi katika baadhi ya mikoa.

Alisema CCM imefuta uchaguzi wa Umoja wa Vijana (UVCCM) mkoa wa Simiyu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo baadhi ya wagombea kujihusisha na vitendo vya rushwa.

"Tumeshatuma timu yetu ya kufanya uchunguzi na baada ya kukamilisha italeta ripoti na hatua zitachukuliwa kwa watakaobainika kujihusisha na rushwa ikiwamo kuwaondoa kabisa katika uchaguzi na kuwakabidhi katika vyombo vinavyohusika na masuala ya rushwa kama vile TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa)," alisema.

Pia alisema CCM imesimamisha uchaguzi kwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) katika mikoa ya Mbeya na Arusha kutokana na kuwapo kwa tuhuma za wagombea kujihusisha na rushwa.

"Aidha katika uchaguzi uliofanyika jana (juzi) katika mkoa wa kichama wa Magharibi Zanzibar kumekuwapo na malalamiko ya baadhi ya watu kuondoka na boksi la kura kwa madai kuwa walikuwa wanapeleka katika chumba kilichokuwa kimeandaliwa kwa ajili ya kuhesabu kura," alisema.

Chongolo alifafanua chama kinaendelea na uchunguzi kuhusu malalamiko hayo na endapo itabainika kuwa waliochukua sanduku la kura walikuwa katika utaratibu sahihi, matokeo ya uchaguzi yatabaki kama yalivyo sasa lakini kama itakuwa vinginevyo, uchaguzi huo utafutwa mara moja.

"Kama tunavyofahamu mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu wa ndani wa Chama Cha Mapinduzi na mimi ndiye mkurugenzi mkuu wa uchaguzi. Tumeendelea kufanya uchunguzi tangu ulivyoanza ngazi ya shina, tawi, kata, jimbo, wilaya na sasa ngazi ya mkoa.

"Tumekuwa tukisema mara kwa mara popote tutakapoona kuna changamoto tutachukua hatua na tumekuwa tukifanya hivyo kwa ngazi zote. Sasa tumeshatuma timu leo (jana) hii ni siku ya tatu ikimaliza kufanya uchunguzi wake, watatuletea taarifa na sisi tutafanya maamuzi (uamuzi)," alisema Chongolo.

Pia alisema chama kimetuma maofisa na viongozi kuwa wasimamizi wa uchaguzi kila mkoa kwa kuwa hawakutaka uchaguzi ufanyike bila macho ya maofisa na viongozi.

Kadhalika, alisema CCM kimekuwa kikifanya vikao na yale yote yanayohusisha mamlaka ya kikatiba yanachukuliwa hatua kwa taratibu ilizojiwekea.




Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (katikati), akipokea mtungi wa gesi kutoka kwa Meneja Masoko wa Kampuni ya Oryx, Peter Ndomba (wa nne kushoto) jana ili kuhamasisha wanawake kutumia nishati safi ya kupikia, hafla iliyofanyika wilayani Serengeti mkoani Mara katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto Njiti yaliyoratibiwa na Taasisi ya Doris Mollel Foundation. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanga waonekana marekebisho ya sheria kandamizi vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amewahakikishia wadau wa habari kuwa atakamilisha mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari Namba 12 ya Mwaka 2016.

Nape aliyasema hayo wakati wa kikao cha pamoja baina ya wadau wa Haki ya Kupata Habari (CoRI), jana jijini Dar es Salaam.

Wadau hao ni Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Umoja wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari (MOAT), Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Chama wa Waandishi wa Habari Tanzania (JOWUTA).

Pia alisema serikali imepokea maoni kuhusu marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016.

"Niwahakikishie kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inayo nia ya dhati katika jambo hili. Nimekuja mwenyewe kuwasilikiliza na imani yangu ni kuona sekta inaendelea kukua," alisema.

Kikao hicho cha pili cha CoRI na serikali cha kupitia mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya habari kiliongozwa na Nape.

"...Tupo kwa ajili ya kufanya mapitio ya mwisho ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya 2016," alisisitiza Nape.

Nje ya kikao hicho, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema: "Kikao kilikuwa kizuri, serikali imeendelea kuonesha dhamira yake ambayo ilikuwa nayo tangu mwanzo. Tumemaliza na serikali inaendelea na hatua zake kabla ya kupelekwa bungeni."

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa MISA Tanzania, Elizabeth Riziki, alisema " Naishukuru serikali kwa kutusikiliza wadau ni mwanzo mzuri kwa ustawi wa sekta ya habari nchini, naamini maboresho yatakayofanyika yataiweka sekta ya habari mahali pazuri sana, pia kutakuwa na ustawi wa watu wake na taifa kwa ujumla." Miongoni mwa mapendekezo ya CoRI kwa serikali ni pamoja na mamlaka ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) yafutwe na kiundwe chombo ambacho pamoja na mambo mengine, kitashughulikia masuala ya usuluhishi yanapotolewa malalamiko dhidi ya chombo cha habari, badala ya kazi hiyo kufanywa na mtu mmoja.

Wadau wanataka marekebisho dhidi ya kifungu cha 6 (e) kinachoelekeza magazeti kupatiwa leseni badala ya usajili wa moja kwa moja.

Pia wadau hao wanapendekeza magazeti yasiendeshwe kwa kupewa leseni, badala yake yapewe usajili wa kudumu au wa muda mrefu, ili kudhibiti changamoto ya ufutwaji holela wa leseni na kuvutia wawekezaji.

Mapendekezo mengine kuhusu sheria hiyo, ni marekebisho dhidi ya kifungu chake cha 7 (2) (b)(lV), kinachoelekeza vyombo vya habari kutangaza au kuchapisha habari na masuala yenye umuhimu kwa taifa, kadiri itakavyoelekezwa na serikali, wadai wakieleza kipengele hiki kinaingilia uhuru wa uhariri.

Sheria zingine zinazolalamikiwa ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Huduma za Posta (EPOCA, 2010), Sheria ya Makosa Mtandaoni (2015), Sheria ya Haki ya Kupata Habari (2016) na Kanuni za Maudhui Mtandao (2018) kama zilivyorekebishwa mara kadhaa.

Sheria hizi zinalalamikiwa kuwa zina vifungu vinavyofifisha uhuru wa habari nchini hivyo zinahitaji kubadilishwa.

# Jela miaka minne kuua bila kukusudia

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu kifungo cha miaka minne gerezani Ayoub Jokolo baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumuua bila kukusudia rafiki yake Said Kombo.

Adhabu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, ambaye alisema amezingatia hoja zilizotolewa pande zote mbili na kumkumbusha mshtakiwa asisahau kuwa rafiki yake aliyemuua alikuwa na familia inayomtegemea.

Pia alisema familia hiyo ingependa wawe naye hadi leo na kwamba anapaswa apewe adhabu inayostahili kwa kuwa mshtakiwa alikuwa na njia nyingi za kuepuka kadhia hiyo ikiwamo kukimbia baada ya kuona wanagombana.

Alisema, sheria inatoa adhabu ya kifungo cha maisha kwa kosa la mauaji na mauaji bila kukusudia kifungo cha miaka isiyopungua 11.

"Nimezingatia muda wa miaka sita na nusu umekaa gerezani, mahakama inakuhukumu kifungo cha miaka minne jela," alisema Hakimu.

Kabla ya hukumu, Wakili wa Serikali, Grace Rwila, aliiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho na hasa ikizingatiwa silaha ya kisu aliyotumia na sehemu aliyomchoma marehemu.

Rwila alidai mshtakiwa huyo Juni 3, mwaka 2016, marehemu alikuwa nyumbani kwake Yombo Vituka, Temeke na ilipofika saa 3:30 usiku alitoka nje na kukutana na mshtakiwa huyo.

Ilidaiwa kwamba, wakiwa hapo waligombana na mshtakiwa alitoa kisu na kumchoma nacho Kombo (marehemu) na kisha kukimbia kusikojulikana.

Wakili huyo aliendelea kudai kwamba, Kombo alidondoka chini na kuomba msaada na watu waliokuwa eneo la karibu walimchukua na kumpeleka kituo cha polisi Makangarawe kwa ajili ya kupatiwa fomu namba 3 ya matibabu kabla ya kupelekwa Hospitali ya Temeke.

Ilidaiwa kwamba Kombo alifariki wakati akipatiwa matibabu.

Juni 9, mwaka 2016, mshtakiwa alikamatwa na alipohojiwa alikiri kutenda kosa hilo na kufunguliwa kesi hiyo.

Uchunguzi wa kitabibu ulibaini kwamba, chanzo cha umauti ilikiwa ni kuvuja kwa damu nyingi kutokana na jeraha kubwa lililokuwa chini ya tumbo.

HABARI KITAIFA

# Wagonjwa wa nje walalamikia malipo ya awali Muhimbili

**Na Mwandishi Wetu**

WAGONJWA wanaokwenda kupatiwa huduma katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), wamelalamikia utaratibu wa kulipia fedha kabla ya matibabu kuwa unasababisha kutopata huduma kwa wakati na kukuza ugonjwa.

Mmoja wa wagonjwa waliopitia kadhia hiyo, Hassan Msuba, aliambia Nipashe kuwa alilazimika kuishi na maumivu ya tumbo nyumbani kwa wiki mbili baada ya kukosa fedha ya kufanya vipimo vya 'ultrasound'.

Hassan alisema kuwa alikwenda hospitalini hapo mapema mwezi huu akiwa na maumivu ya tumbo na baadaye akahitajika kufanyiwa vipimo vya 'ultrasound' vinavyogharimu Sh. 216,000 fedha ambazo hakuwa nazo kwa wakati huo.

"Niliomba kama kuna uwezekano nifanyiwe vipimo kwanza ili nipate matibabu nipunguze haya maumivu kisha nitafute pesa lakini ikashindikana, ikabidi nikae nyumbani wiki mbili na maumivu yangu. Ndugu walijichanga taratibu na wiki iliyopita ndipo nikafanikiwa kupima na kupata dawa," alisimulia.

Hassan alisema wiki mbili alizokaa nyumbani kumesababisha ugonjwa kuwa mkubwa na kwamba alikuwa akihisi maumivu yakiongezeka huku nyakati za usiku akikosa usingizi.

Mgonjwa mwingine, Hadija Ramadhani, alisema Septemba, mwaka huu, alilazimika kuomba wagonjwa wenzie wamchangie Sh. 4,000 aliyokuwa anadaiwa na hospitali hiyo ili kulipa deni aendelee na huduma, iliyozuiwa kutokana na deni hilo.

"Kuna deni la nyuma la Sh. 4,000 nililokuwa nadaiwa baada ya kulazwa lakini sikufanikiwa kupata. Siku niliyokwenda kuchukua vidonge ambavyo vinatolewa bure, waligoma kunipa mpaka nilipe hilo deni," alisema.

Mmoja wa mashuhuda ambaye hakutaka jina lake liandikwe, alisema alilazimika kurudi na mgonjwa wake nyumbani baada ya kupungukiwa fedha kwa ajili ya vipimo vya 'ultrasound'.

"Niliienda na mgonjwa ana maumivu makali ya kifua, tukatakiwa vipimo vya 'ultrasound'. Sikuwa na fedha kwa wakati huo, nikaomba tuendelee na matibabu wakati ndugu wanajichanga ikashindikana. Ikabidi turudi nyumbani mpaka baada ya siku mbili ndipo tukapata pesa na kufanya vipimo," alisema.

Nipashe ilifanikiwa kuuona waraka wa ndani uliotolewa na Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa hospitali hiyo, Ashraph Abdukarim, Oktoba 31, mwaka huu, ukiwasisitiza wafanyakazi wa hospitali hiyo juu ya utaratibu huo.

Waraka huo ulieleza kuwa mgonjwa wa msamaha atakayekwenda kulazwa katika hospitali hiyo, atatakiwa kulipia malipo ya awali ya Sh. 50,000 kabla ya kupata huduma.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa pia wagonjwa hao watakaokwenda kulazwa wodi ya wazazi, watatakiwa kilipia kiasi hicho, huku waliolazwa kwa ajili ya kunyonyesha watatakiwa kutoa malipo ya awali ya Sh. 100,000.

**KAULI YA MUHIMBILI**

Akizungumzia madai hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohammed Janabi, alisema utaratibu wa kulipia kabla kwa wagonjwa wa kuchangia na wanaolipia si mpya na unafanyika ili kuwasaidia wagonjwa hao kupata matibabu kwa haraka.

"Ni kweli kabisa watu wanajilipia na wanaochangia tunaomba walipe siku mbili kabla. Kwanza ni faida kwao, badala ya nataka kutoa damu nenda kalipie, nataka kulipia dawa nenda kalipie, ni kwa manufaa ya wagonjwa na si vingine," alisema Prof. Janabi.


Pia alisema huduma hiyo haiwahusu wagonjwa wa msamaha kwa sababu kundi hilo linatakiwa kupata huduma bure na kuwa hospitali hiyo haijafuta huduma ya msamaha.

"Sisi tuna makundi manne ya wagonjwa. Kuna wagonjwa wa msamaha ambao hawalipi chochote, hata mwezi uliopita tumetoa msamaha wa Sh. bilioni 1.6 kwa wagonjwa. Pia tuna watu wanaochangia, tuna watu wa bima na wale wanaolipia hapo hapo," alifafanua.



Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, si kweli kuwa wagonjwa wanaohitaji huduma ya haraka wanalazimishwa kulipia kabla ya kupata huduma na kuwa na utaratibu uliopo mgonjwa atajiandikisha kwa barua kisha kuendelea na huduma wakati ndugu zake wanafanya utaratibu wa kulipia.

Vilevile aliwashauri Watanzania kujiunga na mfuko wa bima ya afya ili kuepuka ufumbufu wa aina hiyo, ili hospitali hiyo ijiendeshe na kutoa huduma bora inahitaji fedha.




Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Benki ya NCBA, Peter Kimweri (kushoto), akiwazawadia washindi wa Kampeni ya Mpawa iliyopewa jina la 'Chuzi Limekubali' Martin Simbeye ( wa pili kushoto), aliyeshinda pikipiki na Zebedayo Mwasongole ( wa tatu kushoto), aliyekuwa mshindi mkuu wa Sh. milioni 5, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Simba kortini tuhuma za kukamatwa na dawa za kulevya

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA kocha wa makipa wa Klabu ya Soka ya Simba, Mwalami Sultan na mmiliki wa Kituo cha Soka cha Kambiasso Sports Academy, Kambi Seif, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Maulid Mzungu, Said Matwiko, John John na Saraha Eliud, ambao walifikishwa mbele ya Hakimu Mkuu, Mary Mrio na kusomewa mashtaka yao na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga.

Ilidaiwa kuwa Oktoba 27, 2022 katika eneo la Kivule, ndani ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 27.10 za dawa za kulevya aina ya herione.

Katika shtaka la pili ilidaiwa Novemba 4, 2022 huko Kamegele, Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani hapo kwa kuwa Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka upelelezi katika kesi hiyo bado haujakamilika na kesi imeahirishwa hadi Desemba 5, mwaka huu, kwa kutajwa.


## UBALOZI WA NETHERLAND, DENMARK, GATSBY AFRICA NA WATAALAM MBALI MBALI, DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Netherland,Denmark, GATSBY Africa na wataalam mbali mbali watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani na Ofisi na Magari tarehe 26 November, 2022 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street. Fenicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Sofa cam bed, Chest drawer, Meza za chakula, Meza za mkutano,Viti, Book case, School Study table, Makabati ya jikoni, Fridge double door, Majiko ya gas na umeme, Washer,TV set, Printer, Karaoke Music system, Photocopy m/c, A/c split unit, Brad baking oven, Simtank 1,000lts.& 2,000 Lts. na vingine vingi.

**Magari yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Toyota Hilux Double Cabin | 2KD Diesel Engine | 2015/2017 | Umelipwa |
| 1 | Toyota RAV4 Station Wagon | 2AZ Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado TX | 1KD Diesel Engine | 2014 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Station Wagon | 1HZ Diesel Engine | 2002 | Umelipwa |
| 1 | Toyota HARRIER Station Wagon | SXU10 Petrol Engine | 2000 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Murano Station Wagon | Z250 Petrol Engine | 2006 | Haujalipwa |
| 1 | Ford Escosport Station Wagon | FY5 Petrol Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | Lathe Machine Colchester EX. UK | 10 Hose power x 2mts | - | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 23 mpaka 25 November, 2022, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 1 December, 2022 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu lazima awe na bid namba itakayopatikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926 E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

21715702

# Mbaroni kwa madai kumwingizia chupa sehemu za siri mwanamke

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATU wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Manyara kwa tuhuma za kumwingizia chupa ya bia kwenye njia ya haja kubwa mhudumu wa baa katika mji wa Mirerani, baada ya kumbaka na kumwingilia kinyume cha maumbile.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kumfanyia ukatili mhudumu huyo (jina limehifadhiwa), walipomaliza kunywa naye bia na pombe kali katika eneo la Songambele katikati ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, walimchukua na kwenda kutimiza dhamira yao katika eneo la Kazamoyo.

Jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, aliwataja wanaoshikiliwa kwa mahojiano kuhusiana na ukatili huo ni Frank Batezi na Nico Ngowo, wote wakazi wa Mirerani.

"Hawa watuhumiwa wawili walishirikiana na wenzao wengine wawili kufanya ukatili huo na baada ya kumaliza walichoamua kufanya walikimbia. Lakini kwa sababu serikali ina mkono mrefu, watuhumiwa hao wawili walitafutwa na kukamatwa," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Katabazi, uchunguzi wa tukio hilo utakapokamilika, watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja kati ya shuhuda wa tukio hilo, Hassan Juma, alisema Batezi na Ngowo, walikuwa wanakunywa pombe na msichana huyo eneo la Songambele na baadaye walikwenda kulala naye eneo la Kazamoyo nje kidogo ya Songambele.

Shuhuda huyo alidai kuwa watuhumiwa hao walishirikiana na watu wengine kumfanyia mhudumu huyo unyama huo kwa kumbaka, kumlawiti na kisha kumwingizia chupa ya bia kwenye sehemu ya haja kubwa.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mirerani, Dk. Deogratius Mazengo, alipoulizwa na Nipashe kuhusu majeruhi huyo, alithibitisha kutibiwa kituoni hapo baada ya kupelekwa na polisi akiwa na fomu namba tatu ya polisi (PF3) inayomruhusu kutibiwa.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akikabidhi tuzo ya mlipakodi wa viwango vya juu katika sekta ya madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kampuni ya Geita Gold Mining (GGML) na kutambulika kwa kuzingatia kiwango bora cha thamani ya bidhaa zilizosafirishwa nje ya nchi kwa Meneja Mwandamizi wa Fedha GGML, Ikingo Gombo (kulia) na Meneja Utatuzi wa Migogoro ya Kodi GGML, Godvictor Lyimo (katikati), mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Bashiru azidi kumwagiwa upupu

**Na Waandishi Wetu**

MAKADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamezidi kummwagia 'upupu' Mbunge wa Kuteuliwa, Dk. Bashiru Ally, kuwa kauli yake inaweza kuleta taharuki kwa Watanzania wanaotegemea kilimo kuendesha maisha yao ya kila siku.

Aidha, wametaka ajifunze taratibu za chama na kuwa kwenye upande wa kukijenga kwa kumsaidia aliyemteua badala ya kumpiga 'mawe'.

Mwishoni mwa wiki, Dk. Bashiru alikuwa mgeni rasmi kwenye mkutano wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), aliwataka kushikamana kupaza sauti ili ziwatishe wanyonyaji pamoja na mawakala wanaowadanganya wanaupiga mwingi.

Kauli ya 'kuupiga mwingi' imekuwa ikitumiwa na watu mbalimbali kumsifu Rais Samia Suluhu Hassan, kutokana na kazi za maendeleo anazozifanya tangu aingie madarakani Machi 19, mwaka 2021, baada ya kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Wakati wa serikali ya Hayati Dk. Magufuli, Dk. Bashiru alikuwa ni Katibu Mkuu wa CCM Taifa na Februari 26, mwaka 2021 aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi hadi Machi 31, mwaka huo aliteuliwa kuwa Mbunge na nafasi yake kuchukuliwa na Balozi Hussein Kattanga.

Mbunge wa Nzega Vijijini (CCM), Hamisi Kigwangalla, amesema kauli Dk. Bashiru ni ya kichochezi, na kwamba inaweza kuleta tafarani ikiachwa bila kukemewa.

Pia alisema kabla Dk. Bashiru hajaongea alipaswa kuwa na taarifa sahihi, na kwamba bajeti ya kilimo kwa miaka ya nyuma haikuwahi kuzidi Sh. bilioni 250, lakini iliyopitisha mwezi Juni mwaka huu imepanda hadi Sh. bilioni 950.

"Hili ni ongezeko kubwa ambao unafanywa na Rais Samia kwenye sekta ya kilimo, inapotokea mtu ambaye angepaswa kuwa na taarifa sahihi na kuwatia moya wawakilishi wa wakulima wadogo, angepaswa kuwaeleza kwamba rais anawekeza kwa kiasi kukubwa kukuza sekta ya kilimo nchini," alisema Kigwangala.

Aidha, alieleza kuwa kinachofanyika ni upotoshaji wa makusudi, licha ya kwamba serikali inajitahidi kuongeza bajeti katika sekta zinazowagusa wananchi moja kwa moja.

"Kwa zaidi ya miaka mitano iliyopita hatujawahi kupata fedha nyingi, kama tulizozipata kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia, kama Dk. Bashiru anataarifa tofauti na hizi nilizozisema ajitokeze atoe majibu," alisema Kigwangala.

Naye Mbunge wa Mvumi (CCM), Livingstone Lusinde, alisema Dk. Bashiru anatakiwa kuachia nafasi yake kwasababu ameshindwa kumtetea aliyemteua na badala yake aanahamasisha watu kumpinga.

Alisema "Nimepokea kwa masikitiko kauli ya Katibu Mkuu mstaafu, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu na Mbunge wa kuteuliwa na Rais kutoka jimbo la Ikulu, maneno aliyosema Dk. Bashiru kama yangesemwa na mwanachama wa kawaida wa CCM nisingemjibu, mtu mwenye viapo vingi ana mambo mengi ya nchi hii anayajua anapozungumza maneno yale kwa wakulima sio yanayoweza kunyamazwa kimya."

"Bashiru anataka Rais asipongezwe anakerwa na neno la Rais anaupiga mwingi, akawataka wakulima waungane kwa kuwa watawala hawawezi kuwa na amani, na wanashiba kutokana na nguvu ya wakulima," alisema.

Alisema wakati akiwa Katibu Mkuu wa CCM, Chama cha Ushirika Kagera, kahawa ilikuwa inauzwa Sh.600 hadi 700 kwa kilo na mshauri Mkuu wa Chama alikuwa Bashiru, na sasa bei ni Sh. 2,000.

"Hapo Bashiru hataki kusema mama ameupiga mwingi kutoka Sh.600 hadi 2,000, amesahau akiwa Katibu Mkuu korosho zilinunuliwa na serikali, na ikashindwa kuziuza lakini pamba hali ilikuwa taabani, juzi alikuwa China Rais amepata soko kubwa la kuuza parachichi, katika misimu yote ambayo amekuwa kiongozi wa chama bajeti ya kilimo imekuwa Sh. bilioni 250, lakini sasa tangu ameingia madarakani Samia na kuweka vijana wapigakazi, imefika Sh. bilioni 950,"alisema.

Aliongeza "Yeye hapaswi kuchukia uchawa alitakiwa kuwa chawa mkuu kwa kuwa ubunge wake unatoka Ikulu, tulimtegemea yeye aongoze mapambio kama ilivyokuwa mwanzo."

Naye Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku 'Msukuma' alimtaka Dk. Bashiru kujiudhulu nafasi yake kwa kuwa anataka rais asisifiwe akifanya vizuri.

"Kama yeye alichomoa fyuzi na sisi tunachomoa, inauma kusikia Rais wako anatukanwa, wakati akiwa Katibu Mkuu tulimsifu Rais Magufuli na hakuna aliyepinga na Dk. Bashiru alikuwa mbele kumsifia ndani ya CCM na majukwaa."

Mwakilishi wa wakulima mkoa wa Mtwara, Karimu Chipola, alikaririwa akimtaka Dk. Bashiru kuwaacha wakulima wajisemee wenyewe mambo yao huku akieleza serikali ya Samia imetoa pembejeo za korosho zenye thamani kubwa bure kwa wakulima.

**Imeandikwa na Mauld Mmbaga (DAR), Augusta Njoji (DODOMA)**

# Mapya yaibuka kesi ya Sabaya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAWAKILI wanaomtetea aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, katika kesi ya uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na rushwa, wameibua hoja mpya mahakamani wakitaka hakimu anayesikiliza shauri hilo, abadilishwe.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Salome Mshasha.

Wakili wa utetezi, Helena Mahuna, aliwasilisha ombi hilo la upande wa utetezi jana, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Jenifer Edward, aliyesikiliza shauri hilo baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi Mshasha, kuwa kwenye shughuli nyingine za kimahakama jana.

Katika wasilisho lake, Mahuna, alidai kuwa ombi lao linatokana na kuchelewa kusikilizwa kwa kesi hiyo na kuendelea kumfanya mteja wao kuteseka magereza bila kujua hatima yake.

Upande wa utetezi katika kesi hiyo, unaongozwa na Wakili Mahuna, akisaidiwa na Wakili Fauzia Akon na Emanuel Anthony, wakati upande wa mashtaka unaongozwa na Wakili Mwandamizi, Suzan Kimaro akisaidiwa na Wakili Kassim Nassir.

"Leo (jana) ni mara ya pili vibali vinashindwa kuwasilishwa mahakamani hapa kutokana na kutokuwapo kwa hakimu anayesikiliza shauri hili. Tunaomba mheshimiwa, mliangalie hili, kwa kuwa mteja wetu anaendelea kuteseka magereza," alidai Mahuna.

Wakili Mahuna alipomaliza kuwasilisha hoja yake, Wakili Kimaro alidai kuwa nyaraka zote zimekamilika na upande wa mashtaka wako tayari kuviwasilisha, lakini wametaarifiwa kuwa hakimu anayesikiliza shauri hilo hayupo na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa kesi hiyo.

Baada ya hoja hizo kuwasilishwa kwake, Hakimu Jeniffer, alisema amepokea maoni hayo na anaahirisha kesi hiyo hadi Desemba 5, mwaka huu, itakapotajwa tena mahakamani.

Makosa yanayomkabili Ole Sabaya ni kuongoza genge la uhalifu katika Wilaya ya Hai, Februari 2, mwaka jana na kuomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, Februari 22, mwaka jana.

Aidha, Ole Sabaya anadaiwa kujipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai, kwa nia ya kuzuia taarifa za uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi. Pia anakabiliwa na kosa la ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma katika Wilaya ya Hai na shtaka la utakatishaji wa fedha.

## HABARI KITAIFA

# EU yaipa Tanzania bil. 34/- kupeleka umeme vijijini

**Na Beatrice Shayo**

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umesaini mkataba na Umoja wa Ulaya (EU) wa Sh. bilioni 34 kwa ajili ya mradi wa kupeleka umeme vijijini katika vituo vya afya na visima vya maji, ili kupunguza maambukizi ya magonjwa ya milipuko ikiwamo UVIKO-19.

Mradi huo utanufaisha hospitali sita, vituo vya afya 57 na miradi ya maji 363 ambayo itaunganishwa kupata huduma ya nishati ya umeme katika mikoa 25 ya nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam baada ya kusaini mkataba huo, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Saidy, alisema kazi hiyo itafanywa na makandarasi wazawa watatu kusambaza umeme katika vituo vya afya na vituo vya maji.

Alisema mradi huo ni mpango maalumu ambao ulilenga kusaidia jitihada za serikali kuzuia magonjwa ya maambukizi ikiwamo UVIKO-19 na mengine.

Aidha, Saidy alisema utekelezaji wa mradi huo ni miezi tisa hapatakuwa na ongezeko la muda wafanye kazi ndani ya muda au wamalize kabla ya muda uliopangwa.

Alisema kwa upande wa REA watatimiza wajibu wao ikiwamo kuwalipa kwa wakati, ili kazi hiyo imalizike kwa wakati na wananchi wapate huduma kwa wakati.

Naye Kamishna wa Umeme wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Stydem Rwebangira, alisema katika ugonjwa wa Uviko-19 kampeni kubwa ni kunawa na maji tiririka wakabaini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya maeneo mengi ambayo yana shida ya vyanzo vya maji katika miradi ya maji.

Alisema hata katika uhifadhi wa chanjo zilikuwa na changamoto licha ya kuwapo kwa miradi ya umeme vijijini, hivyo EU umewaongezea fedha hizo kuhakikisha maji tiririka yanapatikana na kuhifadhi chanjo za UVIKO-19.

# Mtuhumiwa mauaji azua kizaazaa, ataka kumpiga mwandishi kortini

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Amani Filipo, anayetuhumiwa kumuua Askari wa Kikosi Cha Usalama Barabarani, Sajenti Mensah kwa kumpiga risasi akiwa kazini eneo la mataa ya Sayansi, Kijitonyama Julai 22, mwaka huu, amezua kizaa zaa mahakamani baada ya kutaka kumpiga mwandishi wa habari aliyempiga picha.

Filipo alitoka katika chumba cha wazi cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam huku akisindikizwa na askari Magereza kurudishwa katika mahabusu ya mahakama hiyo jana.

Hata hivyo, wakati akisindikizwa ghafla aliinama chini na kuokota kokoto na kutaka kumpiga mpigapicha huku akizungumza kwa hasira akihoji kwanini anapigwa picha. Licha ya askari kujitahidi kumzuia, mshtakiwa huyo alikuwa akitaka kumkimbiza mpigapicha huyo kitendo hicho kilichozua vurugu na kusababisha askari wengine watatu kuongezeka ili kumdhibiti kutokana na nguvu alizonazo na kufanikiwa kumsukuma hadi kwenye ukuta wa kuingia mahabusu.

Pamoja na kudhibitiwa na askari hao, alitaka pia kupigana nao walipokuwa wakimzuia asimfuate mpigapicha huyo, hali iliyosababisha mkusanyiko wa watu katika eneo hilo. Awali, wakati kesi yake ikilisikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya, askari usalama barabarani, Ashirafu alidai kuwa hakufanikiwa kumpa televisheni Sajenti Mensah kama alivyomwahidi kwa sababu walivamiwa na majambazi na kumuua.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Yasinta Lyimo, Ashirafu alidai Julai 22, 2016 aliingia kazini saa 11:30 alfajiri hadi saa moja usiku katika eneo la mataa ya Sayansi, Kijitonyama na alikuwa akiongoza magari.

Alidai kuwa katika pointi hiyo walikuwa watatu akiwamo kiongozi wake Sajenti Mensah na ilipofika saa moja usiku alitoka katikati ya barabara na kwenda katika kibanda kupumzika akiwa na marehemu na Joshua ambaye ni dereva wa marehemu.

Alidai kuwa yeye na afande wake walikuwa wamekaa kwenye viti ndani ya kibanda hicho na Joshua alikuwa amesimama nje huku wakiendelea na mazungumzo yao ya kawaida.

Shahidi huyo alidai kuwa, alimweleza marehemu kwamba anataka kumpatia TV, kwa sababu yeye anaishi kwenye chumba kimoja na anazo mbili, kwa hiyo anataka kumpatia moja.

Alidai kuwa Sajenti Mensah alikubali kupokea licha ya kwamba nyumbani kwake ana TV pia, lakini kwa sababu amepewa anaipokea, wakakubaliana kwa sababu yeye hakai mbali, kijana wake Joshua aende akaichukue kwa sababu yeye alikuwa na gari.

Alidai wakati anageuka ili atoke katika kibanda hicho na kwenda kupanda gari, alisikia sauti ikisema 'hapo hapo mlipo toeni kila kitu mlichokuwa nacho', alisema kauli hiyo ilishtua kwa sababu hakuna mwananchi aliyewahi kuwaambia hivyo.

Alidai ilibidi ageuke ili amtazame huyo mtu aliyotoa maneno hayo na alipogeuka na afande wake naye alisimama, wote wakawa wanamwangalia usoni, kabla hawajasema chochote mshtakiwa alichomoa bastola na kupiga risasi moja hewani.

"Kwenye akili yangu nikasema hii ishu ipo serious kwa sababu asingefyatua risasi wangemuhoji kuhusiana na kauli yake, lakini kwa kuhofia maisha yangu niligeuka nyuma ili kuangalia wapi naweza kukimbilia ili kuokoa maisha," alidai.

"Kabla ya mimi kutoka, akaja mtu mwingine ambaye alikuwa anakuja uelekeo wake, niliingiwa na hofu, lakini nilipata ujasiri wa kumsukuma akadondoka kwenye kibanda na mimi kwa sababu ya kiwewe nilidondokea kwenye boneti ya gari," alidai Ashirafu.

Alidai kuwa gari hilo lililokuwa limepaki karibu na kibanda hicho lilikuwa ni kwa ajili ya kumchukua Afande Mensah na kumrudisha nyumbani ambaye dereva wake ni Joshua, baada ya hapo aliamka na kukimbia.

Alidai wakati anakimbia alisikia tena mlio wa risasi, hofu ilizidi kuongezeka akaongeza tena mbio na kufanikiwa kupata sehemu yenye giza na kujificha huku akiangalia barabarani na pia alivua nguo zake za trafiki na kubaki na bukta na vesti ili kuondoa mng'ao wa nguo.


# NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT COMPANY LIMITED na JADA INVESTMENT LIMITED** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama zilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GAIMO CONSTRUCTIO N COMPANY LIMITED | GAUDENCE VICENT LYIMO AND MONICA GAUDENCE LYIMO | NYUMBA YENYE HATI YA MAKAZI Na. 21393, PLOT No.407, BLOCK 'JJ' | OLOIRIEN, MANISPAA YA ARUSHA, ARUSHA | 08-12-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT COMPANY LIMITED |
| 2 | KITWANA TWALIB JONGO | KITWANA TWALIBU JONGO | ENEO LENYE HATI MILIKI Na. 140995, PLOT No.49, BLOCK '10' | MABWEPANDE MANISPAA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 9-12-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 3 | PIUS AGUSTINO MTALO | PIUS AGUSTINO MTALO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.KND014243, ARDHI Na.KND/MBR/MWZ28/1 | MWONGOZO, MAKUBURI, MANISPAA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 10-12-2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 4 | MICHAEL SIMBA | MICHAEL SIMBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI Na. 49866, PLOT No.91, BLOCK 'H' | MBEZI BEACH, MANISPAA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 25-12-2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | |
|---|---|
| **HARVESTER CAPITAL INVESTMENT COMPANY LIMITED**<br>**P. O. Box 11898**<br>**ARUSHA**<br>**Tel: 0784200283/0768247735**<br>**Email: harvestercapital558@gmail.com** | **JADA INVESTMENT LIMITED**<br>**P. O. Box 69098**<br>**Dar es Salaam**<br>**Tel: : 0788493699**<br>**Email: jadainvestmentlimited@gmail.com** |

217158902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mazingira yatunzwe kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

**HALI** ya ukosefu wa mvua na baadhi ya maeneo kuonekana kukumbwa na ukame ni moja ya sababu ya uharibifu wa mazingira hasa wa ukataji miti ovyo.

Ukiwa unasafiri kwa njia ya barabara unaweza kushuhudia jinsi baadhi ya maeneo yalivyoathirika kwa kukosa mvua baada ya mazao kukauka na wanyama kuhangaika kutafuta malisho na maji ya kunywa.

Hii inatokana na uharibifu mkubwa wa mazingira wa kukata miti ambayo inasaidia kuleta mvua.

Miti inakatwa kwa wingi kwasababu ya biashara ya mkaa na imeshamiri kwa kiasi kikubwa kutokana na malori na pikipiki zilizosheheni magunia hayo yanavyotoka msituni kuyabeba.

Katika kudhibiti hali hiyo, serikali imechukua juhudi mbalimbali kwa kufanya kampeni ya kupanda miti ili kuweza kurudisha uoto wa asili na kuhifadhi mazingira.

Kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032) kwa lengo la kutoa mwongozo wa hatua za kuchukua ili kutatua changamoto za mazingira nchini kwa kuzingatia upekee wa changamoto katika sehemu husika na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, wakati wa mjadala ulioandaliwa na Benki ya Dunia kuhusu jitihada za Tanzania katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni sehemu ya mijadala katika Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unaoendelea Sharm El-Sheikh, Misri, anaeleza mpango kambambe huo unaonesha changamoto za mazingira zinazoikabili Tanzania ikiwa ni pamoja na uharibifu wa ardhi; uharibifu wa vyanzo vya maji; athari za mabadiliko ya tabianchi; uchafuzi wa mazingira; ukataji ovyo wa miti na uharibifu wa misitu; upotevu wa makazi ya wanyamapori na bioanuai.

"Uharibifu wa mfumo-ikolojia ya pwani na baharini; uharibifu wa ardhi oevu; usimamizi hafifu wa taka; kuenea kwa viumbe vamizi; na changamoto za mazingira katika miji zimeainishwa katika mpango huo," alisisitiza Naibu Waziri Khamis.

Mpango huo kabambe unatoa hatua za kimkakati na mahsusi kwa kuzingatia jiografia na mifumo ikolojia ya maeneo husika. Hatua hizo zinazingatia utofauti wa mtawanyiko wa changamoto za mazingira na hatua muafaka zinazopaswa kuchukuliwa na kutoa mwongozo kuhusu usimamizi wa mazingira.

Kupitia ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mfuko wa Uendelezaji Mitaji (LoCAL), serikali imeanza kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika halmashauri tatu za Kondoa, Chamwino na Mpwapwa pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi wa kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Wito unatolewa kwa jamii kuhakikisha zinaendelea kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kuwa Mabadiliko ya Tabianchi ni halisi na kusisitiza utekelezaji wa sera na mikakati kwa pamoja kwa kesho iliyo bora kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Serikali inaishukuru Benki ya Dunia (WB) kwa kuunga mkono jitihada zake katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi nchini.

Itakumbukwa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira ulizinduliwa Juni 5, 2022 na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa niaba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Hapana, kimya TRC kinatupa hofu zaidi

**SISI** ni Watanzania ambao mbali na kuwa na uchungu sana na hali yetu ya kimaisha tunapata wasiwasi kuhusu baadhi ya mienendo inayotutia shaka tukihisi kuwa pengine tunadanganywa kwa manufaa ya watu wachache, wanaodhani kuwa hatuwezi kufuatilia.

Ni hofu tunayokuwa nayo kuhusu ahadi ya kazi tuliyopewa na Shirika la Reli (TRC) miezi minne iliyopita na sasa ni ukimya usio na wa kumuuliza licha ya sisi kusaini mikataba.

Tulianza kuwasiliana kwa waraka huu uliokuwa na ujumbe mahsusi: Tangazo la kuitwa kazini (kazi ya muda mfupi).

Shirika la Reli Tanzania linapenda kuwaarifu wafuatao hapo chini (majina tunayo) kuwa maombi yao ya kazi za muda mfupi yamekubaliwa na hivyo wanaarifiwa kuripoti ofisi ya Mkurugenzi wa Rasilimaliwatu na Utawala Dar es Salaam, siku ya tarehe 12-15 /8/2022 kwa ajili ya kusaini mikataba ya kazi.

Kwa mawasiliano yote yapitie kwa Mkurugenzi Mkuu wa 'Locomotives Maintenance Manager TRC-Morogoro', kwa kuamini kila kilichoelezwa tulikwenda kusaini mikataba.

Kwa upande wetu ilikuwa tarehe 16, Agosti 2022, mamia ya mafundi tuliitwa katika Ofisi za Shirika la Reli (TRC) kwa ajili ya kusainishwa mikataba mbalimbali ya kazi za kiufundi.

Hatua hiyo inakuja baada ya TRC kutoa nafasi za kazi za mafundi wa aina mbalimbali kuanzia wa gereji, karakana za mabehewa, seremala, uwashi, fundi chuma, mabomba na mengine mengi.

Baada ya kusoma tangazo tulipopeleka barua za maombi tuliambiwa kuwa tutaitwa. Na kweli ilipotimia siku hiyo ya Agosti 16, tuliitwa na kwenda kusaini mikataba ya kila mmoja tukiwa zaidi ya mafundi 200.

Tulifika kwenye ofisi ya TRC Dar es Salaam, tukakabidhiwa mikataba na kuisoma na katika maelezo tulielezwa tutafanya kazi gani ni kwamba tutafanya kwa muda gani na mkataba ukitufahamisha kuwa tutatumia miezi mitatu ya majaribio, na baada ya hapo tutapewa ajira kamili.

Tulisaini mikataba hiyo lakini cha ajabu hatukupewa nakala wala chochote tulichosaini kama kopi yetu binafsi wala kufahamu sababu hasa za kukusanya karatasi hizo bila sisi kupewa karatasi ambazo tunadhani ni haki yetu.

Chakushangaza zaidi hadi leo hatujapata taarifa yoyote ya kuitwa kazini wala kupigiwa simu licha ya ahadi tuliyopewa waliyosema kwamba tutapigiwa simu kujulishwa muda wa kufika na kuelekea kazini.

Huu ni mwezi wa nne bila jibu wala mawasiliano ndiyo maana tunaiomba serikali itusaidie kuufahamu ukweli kuliangalia suala hili kwa maana lina maswali mengi kuliko majibu tena hofu kuwa huenda kuna nia mbaya, inawezekana ya kutumia sisi mafundi kujinufaisha jambo linaloweza kufanywa na watu wajanja wachache.

Tuseme kweli tuna wasiwasi kuwa inawezekana kuna watu wachache wanaonufaika na mishahara yetu ambayo tungelipewa, lakini wajanja wanajibandika kazi na mikataba tuliyosaini kama mafundi na kujineemesha.

Hatulaumu mtu lakini kazi tuliyojulishwa ya kufanya ni kukarabati viti kwenye mabehewa ya treni lakini tunapenda kufahamu hivi kazi hiyo ipo? Ilikuwa hewa au ni nini hasa?

Ni jambo ambalo TRC ilikusudia kulifanya au ni ujanja wa kuhalalisha mipango ambayo inatumia majina yetu kwa baadhi ya wadanganyifu ambao huenda hata TRC haiwajui?

Tulioitiwa kazi hii ni mafundi zaidi ya 271 tukipewa majukumu mbalimbali kama mafundi wa filter (filter mechanics) umeme, 'black smiths', kazi za vyuma, mafundi mchundo wa mabehewa, maseremala, 'gas plant', rangi na 'trimmers' lakini wote hatujapewa kazi wala hatufahamu lengo la kutusainisha mikataba hiyo.

Tunaomba kuwasilisha ili tuujue ukweli maana hatukuwa na mwongozo wala njia ya kuwasiliana na mwajiri huyu.



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Hassan Saidy (kushoto), akisaini mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme vijijini na Mhandisi wa Kampuni ya On Electrical, Mrisho Masud (wa pili kulia), jijini Dar es Salaam jana. Mradi huo umefadhiliwa na Umoja wa Ulaya. Wengine ni Meneja Miradi wa EU, Francis Songela. **PICHA: MAULID MMBAGA**

## Serikali yaahidi kumaliza machungu vifurushi vya intaneti mwezi ujao

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema bado mwezi nmoja kumaliza machungu ya gharama za vifurushi vya intaneti.

Amesema Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inaendelea na tathmini ya kupitia gharama halisi za utoaji wa huduma za vifurushi vya intaneti na wanatarajia kukamilisha kazi hiyo mwezi ujao.

Nape aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu kazi inayofanywa na TCRA ya kupitia gharama zinazotozwa na watoa huduma zinakidhi viwango vilivyowekwa kisheria.

"Kwa muda mrefu watumiaji wa huduma za vifurushi vya intaneti wamekuwa na malalamiko ya kutoridhishwa na huduma zinazotolewa na kampuni za simu. Tathmini inaendelea na itakamilika mwezi Desemba na Januari ripoti itatolewa rasmi," alisema Nape.

"Serikali inafanya mambo mawili makubwa kupitia TCRA, ikiwamo kufanya tathmini ya kawaida inayofanyika kila baada ya miaka mitano.

Baada ya tathmini hiyo, tutatoa bei elekezi ingawa watoa huduma wote kwa sasa wako katika viwango vya bei elekezi iliyowekwa na serikali ambayo ni kati ya Sh. 2.03 hadi Sh. 9.35," aliongeza.

Alisema baada ya kukamilika kwa mapitio hayo anaamini kutakuwa na mabadiliko ya kushuka kwa gharama za intaneti.

"Nasisitiza wakati tukisubiri matokeo ya tathmini hiyo hakutakuwa na mabadiliko yoyote ya gharama za intaneti hadi kukamilika kwa kazi inayoendelea," alisema.

Nape pia alitangaza kufungua dirisha la maombi ya wajumbe wa bodi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Mawasiliano ambalo tangu limeanzishwa halijulikani kwa sababu ya kukosa bodi.

"Tulitangaza watu waombe lakini mwitikio ulikuwa mdogo nikashindwa kuteua wajumbe, hivyo tumeongeza siku saba za watu kufanya maombi ili tupate watu watakaoingia katika baraza hili.

"Tukishaliunda kazi yao ya kwanza ni kukusanya maoni ya watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini na wakikamilisha watayaleta serikalini ili tupitie marekebisho ya baadhi ya kanuni kwa lengo la mtoa huduma ajue haki yake na mtumiaji pia afahamu," alisema Nape.

# Polisi yakamata silaha za kivita

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limekamata bunduki mbili aina ya Ak47 ambazo zilikuwa zikitumika katika matukio mbalimbali ya uhalifu.

Jeshi hilo pia limepokea silaha 30 ambazo zimesalimishwa na wananchi, kutokana na agizo lililotolewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camilius Wambura. Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Alisema jeshi hilo kuanzia Septemba hadi mwezi huu, katika misako mbalimbali ambayo limefanya, limekamata vitu mbalimbali vya wizi, dawa za kulevya, mitambo ya kutengeneza pombe haramu ya gongo, mitungi ya gesi na silaha mbili za kivita aina ya AK47, huku bunduki 30 zikisalimishwa.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga tumekamata silaha mbili za kivita aina ya AK47 ambazo zilikuwa zikitumika kwenye matukio mbalimbali ya uhalifu, huku, silaha 30 zikisalimishwa kufuatia agizo la IGP," alisema Magomi.

"Tumekamata pia pikipiki 12, baiskeli moja zote za wizi, dawa za kulevya aina ya heroine kidonge kimoja, kete 10, bangi kilogramu 55, mirungi kilogramu 10, mitungi ya gesi mitano, Tv tatu, mitambo miwili ya kutengenezea pombe haramu aina ya gongo," aliongeza.

Magomi alitaja vitu vingine walivyokamata kuwa ni majiko manne ya gesi, kompyuta tatu, sabwoofer sita, monitor tatu, darubini tatu za maabara, king'amuzi kimoja, magodoro matatu na bidhaa mbalimbali za dukani zikiwamo juice.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wananchi mkoani hapo kufika katika jeshi hilo wakiwa na nyaraka muhimu, ili kutambua vitu vyao ambavyo viliibiwa, huku akiwataka pia kuendelea kutoa taarifa za uhalifu.


## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED,** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK (T) LTD,** tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba dhamana ifuatayo baada ya siku 14(kumi na nne) kuanzia tarehe/siku ya tangazo hili.Dhamana hii imewekwa rehani kudhamini mkopo uliyotolewa na benki ya **ICBTL kwa SKYMAX ELEVATORS LIMITED** (mkopaji).

Pia, Tangazo hili la Mnada wa hadhara, ni notisi ya siku 14 (kumi na nne) kwa Mkopaji /Mdhamini wa mkopo kuhusu mauzo ya dhamana husika kwa mnada wa hadhara.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAZOUZWA**





| NO | JINA LA MKOPAJI/MDHAMINI | TAARIFA ZA DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **i. SKYMAX ELEVATORS LIMITED (MKOPAJI)** | Jengo la biashara na makazi yenye hati nambari: 80902, Plot na.1364, Block 'A', KinyerezI, Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam. Eneo: Mita za mraba 2243 | - |
| | **ii. ARM STRONG NICO JERRY (Mortgagor)** P.O. Box 14760 Dar Es salaam. | | 08/12/2022 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. |

217159102

**Wanunuzi wote wenye nia na uwezo,mnakaibishwa kuja kukagua mali kwa vigezo na masharti yafuatayo:**

**VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA;**

1. Mali/Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 kutokea siku ya mnada.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
4. Gharama za kuhamisha umiliki na kumtoa mdaiwa/mpangaji "Eviction" na nyinginezo, zitakuwa juu ya Mnunuzi.
5. Ukaguzi wa dhamana unaweza kufanywa na wanunuzi, siku yoyote kuanzia siku ya tangazo hili wakati wowote baada ya saa tatu asubuhi.
6. **Kwa taarifa zaidi,wasiliana nasi kwa namba: 0755 506 970/0653005019**

# Serikali yaeleza nguvu mpango wa taifa

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema ili kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, nguvu kubwa imeelekezwa kwenye maendeleo ya jamii kwa kuweka afua za kuondoa njaa nchini.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angella Kairuki, wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la BRAC nchini Bangladesh na miaka 15 Tanzania.

Alisema nchi inatekeleza mpango wa tatu wa maendeleo ya taifa ya miaka mitano kwa mwaka 2021 hadi 2026 ili kuhakikisha inajenga uchumi shindani na kuongeza uwezo wa nchi katika sekta ya uzalishaji.

"Ili nchi iweze kufikia malengo hayo, nguvu kubwa inaelekezwa katika maendeleo ya jamii kuweka afua za kuondoa njaa kwa lengo la kuboresha kilimo na kutafuta masoko kwa wakulima na wafanyabiashara," alisema Kairuki.

Aidha, alisema imani yake kwa BRAC itaendelea kugusa maisha mengi ya Watanzania hususani wanawake na wajane ambao wanahitaji huduma zao.

Alisema shirika hilo limefanikiwa kuleta mabadiliko chanya katika jamii hasa masuala ya uwezeshaji wa kiuchumi miaka 15 iliyopita na limeendelea kukua na kugusa maisha ya wananchi katika elimu, kilimo na kifedha.

"Waendelea kutekeleza mwongozo wa malezi na makuzi ambao umeandaliwa na taifa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2021 hadi 2026," alisema.

Kairuki alisema serikali haiwezi kutekeleza majukumu peke yake bali kupitia ushirikiano huo ambao wamekubalina baina ya sekta ya umma na binafsi na kupata mafanikio katika maeneo mengi ya nchi.

Pia alisema shirika hilo limetoa mkopo usiohitaji dhamana kutokana na kwamba wanawake wengi hawajamaliza kuweka dhamana, na kwamba wamewafikia wengi hasa walioko vijijini.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema shirika hilo limekuwa likitekeleza miradi mbalimbali nchini ambayo inagusa masuala ya kiuchumi, ili kukabiliana na umaskini.

Gwajima alisema anatambua mchango mkubwa wanaoutoa katika eneo la malezi na makuzi ya watoto na kwamba wamejenga vituo 30 vya kijamii na malezi ya awali.

Alisema vituo 25 vimekamilika na vimeashaanza kutoa huduma na vitano vilivyobaki vipo katika hatua tofauti tofauti ya ujenzi na vimegharimu jumla ya Sh. milioni 400 na manufaa yake yameanza kuonekana.

Dk. Gwajima alisema Septemba, mwaka huu, kwa kushirikiana na BRAC wametia saini mkataba wa makubaliano, ili kuchangia katika utekelezaji wa mipango ya wizara wana imani watafanya kazi vizuri.

Mkurugenzi wa BRAC Maendeleo Tanzania, Suzan Bipa, alisema shirika hilo lilianzishwa nchini Bangladesh mwaka 1972 na Fazle Hasan Abed, likiwa na lengo kuu la kuhudumia wakimbizi zaidi ya milioni 10 ambao walikuwa wanarudi nyumbani baada ya vita nchini humo.

Alisema mpaka sasa wanafanya kazi katika nchi 16 na wamefanikiwa kupata tuzo mbalimbali kama asasi bora duniani kwa miaka mitano.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akipiga kura wakati wa uchaguzi wa chama hicho Mkoa wa Mjini Magharibi juzi. **PICHA: CCM**

# CCM: Wingi wa wanachama kuwania uongozi ishara ya kukubalika kwake

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema mwitikio mkubwa wa wanachama kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya shina hadi taifa katika uchaguzi wa mwaka huu, ni salamu za kukubalika kwa Mwenyekiti wa Chama, Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia kimesema wingi huo wa wanachama ni salamu za historia mpya katika kufanya vizuri katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kwa kuwa viongozi watakaopatikana mwaka huu ndio watakaokiongoza chama katika mchakato huo.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wajumbe wa mkutano mkuu wa Mkoa wa Magharibi katika ukumbi wa Banquet, mjini Unguja.

"Viongozi hao wa chama wa mikoa ndio watakaotoa mweleekeo wa ushindi wa CCM mwaka 2024 katika uchaguzi wa serikali za mitaa Tanzania Bara na mwaka 2025 uchaguzi mkuu kwa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Shaka alisema CCM bado chaguo la umma kwa kuwa ni madhubuti, ina muundo bora, mtandao mpana, viongozi imara, sera nzuri na kubeba matumaini na matarajio ya wananchi.

Alisisitiza kwamba mwitikio wa wanachama wa CCM kujitokeza kuomba uongozi umekuwa mkubwa kuliko wakati wowote katika historia ya chama.

Kwa mujibu wa Shaka, mwitikio huo ni kielelezo cha kukubalika, demokrasia pana na utendaji haki ndani ya chama pamoja na imani kubwa waliyo nayo wanachama na wananchi kwa uongozi wa Rais Samia ambaye ni mwenyekiti wa taifa wa chama hicho.

Sambamba na hilo, alisisitiza kuwa kuelekea mwaka 2025, chama kwa mujibu wa utaratibu na utamaduni wake, hakina mpango wa kupata wagombea urais wengine kwa upande wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, badala yake kazi kubwa iliyoko mbele yao ni kuendeleza umoja, mshikamano na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 ili itekelezwe kwa viwango kama ilivyoahidiwa kwa wananchi.

"Tabia na utamaduni huu wa kuahidi na kutekeleza umeendelea kuifanya CCM kutokuwa na mpinzani katika siasa za ushindani. Wanachama wa CCM fanyeni uchaguzi wa viongozi kwa sifa na uwezo wa kuongoza kwa maslahi ya chama na nchi yetu," alisema.

## Tanzania na SADC kupunguza gharama za mawasiliano nje

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

TANZANIA itashirikiana na nchi nyingine za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kuboresha huduma za mawasiliano ikiwamo kupunguza gharama za mawasiliano (roaming costs) miongoni mwa nchi wanachama.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Pili wa Kamati ya Udhibiti wa Uchumi (ERC) ya Chama cha Wadhibiti wa Mawasiliano Kusini mwa Afrika (CRASA) ulioratibiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, Dk. Khalid Mohamed, alisisitiza kuwa serikali itatathmini pendekezo la CRASA kupunguza gharama za mawasiliano kwenye ukanda wa SADC.

"Kuhusu suala la 'roaming' kama ulivyolizungumzia Mwakilishi wa Katibu Mtendaji wa CRASA, sisi pamoja na wenzetu tutaangalia namna tutaweza kulitekeleza suala hilo ili kuwezesha wananchi wetu kupata gharama nafuu za mawasiliano wanapokuwa kwenye nchi wanachama wa SADC," alisisitiza.

Mkutano huo wa siku tano utatanguliwa na warsha inayolenga mbali na mambo mengine kuwajengea washiriki uwezo katika ukusanyaji, uchambuzi na utoaji taarifa za viashiria vya ukuaji wa sekta ya Mawasiliano, chini ya uwezeshaji wa Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU).

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema wajumbe wa CRASA watapata fursa ya kuelewa masuala muhimu ya ukuzaji sekta ya mawasiliano na kwamba TCRA kama mwanachama hai, itapata uelewa wa masuala muhimu yatakayosaidia usimamizi madhubuti wa gharama za mawasiliano.

"Huu ni mkutano muhimu sana na tunatarajia washiriki wote tukiwamo TCRA kurejea nyumbani tukiwa tumeshibishwa elimu katika maeneo bayana. Ikumbukwe kwamba kwenye mkutano huu,washiriki watajengewa uwezo kuhusu upangiliaji gharama za vifurushi vya mawasiliano ili kuongeza uelewa wa nchi wanachama hatimaye kukuza ufanisi wa utoaji huduma za mawasiliano katika nchi za SADC na sisi hapa kwetu tutanufaika sana," alisema.

Naye Kaimu Katibu Mtendaji Mkuu wa CRASA, Shukya Kiroga, ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Kielektroniki wa CRASA, alisema hatua zilizofikiwa na wanachama ni utafiti wa kitaalamu wa gharama elekezi tayari umekamilika na kinachotakiwa ni nchi wanachama kuanza utekelezaji.

Aidha, alitoa angalizo kwamba utekelezaji unahitaji makubaliano ya nchi wanachama ili kufanyika bila mkwamo.

HABARI KITAIFA

# Miradi 5 ya maendeleo yakamilishwa Matuli

**Na Christina Haule**, MOROGORO

MRADI wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) umefanikiwa kutekeleza asilimia 90 ya ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kijiji cha Lulongwe, Kata ya Matuli kwa kukamilisha miradi mitano ya maendeleo baada ya kukusanya zaidi ya Sh. milioni 250 kutoka kwenye shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii (USMJ).

Katibu Kata Matuli (CCM), Maalim Semindu, alisema hayo jana wakati viongozi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) wanaotekeleza mradi huo kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC) walipotembelea vijiji vyenye miradi kuangalia mafanikio ya tangu ianzishwe mwaka 2016 na kuanza kutoa matokeo mwaka 2017.

Semindu alisema mwaka 2015 kwenye uchaguzi wakati akimnadi mgombea udiwani wa kata hiyo, Lucas Lemomo aliahidi kutekeleza ilani ya uchaguzi ikiwa ni pamoja na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi ikiwamo ujenzi.

Alitaja miradi aliyoahidi wananchi wa kijiji hicho kuwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara ambayo ilikuwa inapitika kwa shida, ujenzi wa shule ya sekondari ya kata kwa kuongeza madarasa mawili ili itumike, uwapo wa vikundi vya hisa (Vicoba), kuweka huduma za afya kwa kujenga zahanati ya kijijini na ujenzi wa nyumba za walimu.

Naye Diwani wa Kata ya Matuli, Lucas Lemomo, alisema hali ya kijiji cha Lulongwe ilikuwa ngumu kimapato kabla ya mradi, lakini baada ya mradi wamejengewa ofisi ya kisasa ya kijiji na kuepukana na adha ya mvua kwa kukaa chini ya miti.

Lemomo alisema matumizi bora ya ardhi yanazingatiwa na wakazi wa kijiji hicho kwa asilimia 90 kwa sasa na zamani kabla ya mkaa endelevu kulikuwa na biashara kubwa ya mkaa uliovunwa kiholela wa baiskeli na pikipiki.

Alisema anaushukuru mradi huo kwa kuingiza vijiji vitatu kati ya vinne vilivyoko kwenye kata hiyo kwenye mradi wa mkaa endelevu na kupata mafanikio katika kijiji cha Diguzi kwa kukusanya Sh. milioni 80 na kutumia katika maendeleo mbalimbali ya kijiji.

Aidha, Matuli wamepata zaidi Sh. milioni 104 kujenga mindombinu ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyoo vya wanafunzi na kupanua madarasa, zahanati na kukarabati madarasa.

Mradi wa CoForEST unatekelezwa katika vijiji kadhaa vilivyoko kwenye wilaya za Morogoro, Kilosa na Mvomero mkoani Morogoro, Liwale, Ruangwa na Nachingwea mkoani Lindi na Kilolo mkoani Iringa.

# DC aagiza watumishi wa afya wanaokiuka maadili waadhibiwe

**Na Thobias Mwanakatwe**, MANYONI

MKUU wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, amewaagiza viongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida kuwachukulia hatua watumishi wa afya wanaokiuka maadili yao ya utumishi.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni katika kikao kilicholenga kutatua changamoto katika hospitali hiyo ili kuboresha huduma.

"Ninazo taarifa wapo walinzi wetu ambao wamegeuza geti kuwa sehemu ya biashara kwa kuuzia wajawazito vifaa vya kujifungulia kwa gharama kubwa, kuanzia sasa naagiza tabia hii ikomeshwe mara moja," alisema.

Mwagisa aliongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya, alisema serikali inapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaofika kupata huduma za matibabu katika hospitali hiyo.

Alisema wananchi wanahitaji kupokewa vizuri wanapofika kupata huduma za matibabu na inapotokea hawahudumiwi vizuri malalamiko lazima yawapo, serikali haitasita kuchukua hatua kwa wasiozingatia maadili ya kazi.

"Kuna baadhi ya watumishi wanaingia kazini kwa muda wanaotaka wao na wengine kukataa kuingia kwa madai kuwa wanadai fedha za uhamisho, kama taratibu za malipo zinaendelea watumishi mnapaswa kuingia kazini na kutoa huduma kama kawaida," alisema.

Alisema madaktari na wahudumu wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni wanapaswa kuwaelimisha wajawazito wanapokwenda kliniki ya mwisho kabla ya kujifungua kuandaa vifaa ambavyo wanapaswa kwenda navyo siku ya kujifungua ili waviandae mapema kuepuka kununua kwa gharama kubwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Fadhili Chimsala, alisema watumishi wanaokiuka maadili ya utumishi watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu na sheria.

"Niweke wazi wanaokiuka maadili kama watumishi hatua stahiki zitachukuliwa na hili siwezi kulifumbia macho maana nia yetu ni kuhudumia wananchi kwa maslahi mapana ya nchi na sio vinginevyo hivyo kama utashindwa tutakutaka uwapishe wanaoweza kuwatumikia wananchi kwa kufuata taratibu na kanuni za utumishi," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda, alisema watumishi wa idara ya afya wanapaswa kutambua kuwa hospitali ni kama gereji na wanapaswa kuwahudumia wananchi vizuri ili kusiwe na malalamiko.

Mganga Mkuu Wilaya ya Manyoni, Dk. Furaha Mwakafwila, alisema kuna baadhi ya wananchi wanatoa rushwa halafu hawasemi kwa uongozi, lakini kwa wale wanaosema hatua zimekuwa zikichukuliwa papo kwa papo.

Dk. Mwakafwila alisema uongozi wa hospitali unaendelea kuelimisha jamii inayotuzunguka ili wajue Sera ya Afya inasemaje ikiwapo wanaostahili kupata msamaha wa matibabu.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Knauf Gypsum, Ilse Boshoff (kulia) na Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Lilian Mangaru (kushoto), wakimkabidhi Mkurugenzi wa Kampuni ya Super Terrazzo Ltd, Nish Hiran, tuzo baada ya kuibuka mshindi wa usambazaji wa bidhaa za kampuni hiyo katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO: Mgawo wa umeme kuwa historia 2025

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Umeme Nchini (TANESCO), limejipanga kuhakikisha mgawo wa umeme unakuwa historia nchini ifikapo mwaka 2025 na limeanza kwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Maharage Chande, wakati akizungumza na wanachama wa Jukwaa la Wahariri (TEF).

Chande ambaye alikuwa akizungumzia mwaka wake mmoja ndani ya shirika hilo, alisema mgawo huo utatoweka kutokana na mipango mbalimbali wanayojiwekea ikiwamo kuongeza vyanzo vingi vya kuzalisha umeme.

Alisema miezi mitatu ya mwanzo Shirika hilo lilikuwa katika hali ya kujipanga kujua matatizo, changamoto na kubaini fursa na kuweka mipango ya kuchukua fursa kuzitumia kutatua matatizo yaliyoko.

"Kwa kipindi kile cha miezi mitatu ya mwanzo tulimaliza kujipanga kwa maana ya kubaini sehemu zenye matatizo na fursa ziliko na kutengeneza mikakati kuzichukua fursa kutatua changamoto na tuliainisha maeneo saba ambayo tutayazingatia," alisema.

Alitaja maeneo ya kuzingatiwa kuwa ni maslahi bora ya wafanyakazi wa shirika hilo, wateja, miradi ya kimkakati, ufanisi, kutafuta fedha, kuondoa vihatarishi vya kuendesha shirika hilo na kuimarisha mawasiliano baina yao na wateja.

Alisema baada ya kukamilika awamu ya kujipanga walikuja na awamu ya pili ya utekelezaji wa mambo yote waliyobaini ikiwamo kuongeza idadi ya wateja na kutafuta vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme.

"Kwenye sekta hii ya umeme kuna kitu kinaitwa enegy mix iimaanisha uwe na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme badala ya kutegemea chanzo kimoja sasa kwa mwaka huu tunategemea mradi wa Megawati 185 wa Kinyerezi I umeme wake utaingia kwenye gridi ya taifa," alisema.

Kuhusu uzalishaji umeme Mkoa wa Kigoma, alisema shirika lilikuwa linatumia Shilingi bilioni sita kila mwezi wastani wa Sh. milioni 36 kwa siku kwa ajili ya kuendesha majenereta, lakini baada ya kuyazima na kuwaingiza kwenye gridi ya taifa limepata ahueni.

Kuhusu malalamiko ya umeme mdogo mkoani humo, Chande alisema shirika hilo lilizima majenereta hayo ili kuwaingiza kwenye gridi ya taifa lakini bado yapo ili umeme wa gridi utakaposumbua wayawashe na wananchi wa mkoa huo waendelea kupata huduma.

"Gridi ya taifa ikisumbua tutayawasha si yako palepale Kigoma, gridi ikiwa sawa tunaendelea kuokoa gharama kubwa zilizokuwa zinatumika kwa mwezi, lakini kwa sasa changamoto walizonazo zimeshughulikiwa," alisema Chande.

Alisema matumizi ya gesi katika uzalishaji wa umeme yamekuwa yakiongezeka kuanzia mwaka 2010 na lengo kuu ni kuhakikisha nishati hiyo inatumika kwa wingi kuzalisha umeme kwa kuwa ni ya kuaminika kulinganisha na kutegemea maji.

Kuhusu mradi wa uzalishaji umeme Rusumo, alisema unatarajiwa kuanza kuzalisha na kuingiza kwenye gridi ya taifa kuanzia mwezi Desemba, mwaka huu au Januari mwakani na mwaka huu wa fedha wanatarajia kufikia uzalishaji wa Megawati 1,900.

"Mwaka 2023/2024 tutakuwa na mradi wa jua Kishapu Shinyanga ambao sasa hivi tunafanya tathmini ya zabuni, tuna mradi mwingine Manyoni Singida, Zuzu Dodoma, Mafia na katika kuyafanya haya msingi mkubwa ni wafanyakazi wetu na tumeongeza maslahi yao kwa kiwango kikubwa kwasababu tunaamini tukiwajali hawa mambo yetu yatakuwa mazuri," alisema Chande.

# Serikali kutopandisha nauli ya treni Kanda ya Kaskazini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewahakikishia wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Arusha kuwa hakutakuwa na ongezeko la nauli ya treni inayopita katika mikoa hiyo ili kuwawezesha kufanya safari zao kwa urahisi hasa katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka.

Akizungumza jijini Arusha, baada ya kutembelea stesheni ya reli ya kati, Naibu Waziri Atupele Mwakibete amesema kuwa uwepo wa treni hiyo umerahisisha shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya Dar es Salaam na mikoa hiyo na serikali inatarajia kuongeza idadi ya mabehewa ili kuwawezesha abiria wengi zaidi kutumia usafiri huo.

"Toka kuanzishwa kwa safari za treni kwa mikoa hii mwaka 2020 kumekuwa na ongezeko kubwa la abiria na mizigo na kazi ya serikali ni kutoa huduma, hivyo niwahakikishie wananchi kuwa serikali itaendelea na nauli zile zile pamoja na ongezeko la abiria ili kuwawezesha kwenda kusalimia ndugu zao mwisho wa mwaka," alisema.

Kadhalika, alisema safari za treni zinatarajiwa kuongezeka kutoka safari tatu kwa wiki mpaka nne kwa wiki mabehewa mapya yatakapowasili mwishoni mwa mwezi Novemba, mwaka huu.

Vile vile, alisema serikali kupitia Shirika la Reli Nchini (TRC), inaendelea na ukarabati wa mabehewa 600 lengo likiwa ni kuhakikisha kuna mabehewa ya kutosha ya kusafirisha abiria na mizigo.

Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa TRC, Focus Sahani, alisema kwa sasa kupitia treni hiyo wanasafirisha zaidi ya tani 11,600 za mizigo safari moja ni zaidi ya 300.

Alisema kuanza kwa treni hiyo kumeleta mafanikio kwa kuwa wananchi wamepata ahueni ya kupungua kwa bei ikiwamo saruji kushuka kutoka Sh. 20,000 kwa mfuko mmoja mpaka Sh.15,000.

Naibu Waziri Mwakibete yuko mkoani Arusha kwa ziara ya siku mbili kukagua miradi ya maendeleo na kuangalia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akikabidhi cheti cha udhamini wa Tuzo za 16 za Rais za Wazalishaji Bora wa Viwandani (PMAYA) kwa Meneja Uhusiano na Mawasiliano ya Nje wa Kampuni ya Tanga Cement, Mtanga Noor (wa pili kushoto). Tanga Cement iliibuka kidedea kwa mshindi wa jumla na mzalishaji bora wa kampuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania, Canada kushirikiana kujengea ujuzi vijana

**Na Steven William,** MUHEZA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Taasisi ya Vyuo nchini Canada (CICan), wamepanga kutekeleza mradi wa kujengea ujuzi vijana (ESP).

Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Canada kupitia Global Affairs Canada ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka saba hadi mwaka 2028.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa utambulisho wa mradi huo, Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) Kiwanda wilayani Muheza, Geofrey Mwiga, alisema mradi huo unatekelezwa na Chuo cha FDC Kiwanda kwa kushirikiana na Kituo cha Msaada wa Kisheria (ZICOSAD).

Mwiga alisema kuwa mradi huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana wakiwamo wasichana waliokosa elimu kupitia mfumo rasmi wa kupata elimu, ujuzi na ufundi ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Alisema mradi huo unalenga kuwezesha msichana pamoja na jamii kupata ujuzi utakaomwezesha kutumia fursa mbalimbali kibiashara na elimu ya masuala ya kijinsia. Mwiga alisema kuwa FDC Kiwanda ni miongoni mwa vyuo 12 vitakavyotekeleza mradi huo na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliendesha mafunzo maalum Novemba 2021.

Alisema kuwa mafunzo hayo yaliwashirikisha wakurugenzi wa halmashauri ambao ni wenyeviti wa bodi za vyuo, wakuu wa vyuo, maofisa maendeleo ya jamii, walimu na mkufunzi mmoja wa kike kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kufahamu mradi huo na manufaa yake katika halmashauri husika.

Alisema, mpango wa uwezeshaji ujuzi ESP kupitia uhamasishaji wa jamii kuhusu usawa wa kijinsia na haki za binadamu unalenga kusaidia familia, jamii na serikali kuwawezesha wasichana waliobalehe kuwa na maarifa na ujuzi kwa ajili ya maisha bora ya kesho.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Edward Mgaya, alisema wanaukaribisha mradi huo kwa mikono miwili kwa kuwa utakuwa na faida kubwa kwa vijana wa Muheza kupata ujuzi.

## Walimu waelezwa umuhimu wa kufundisha fasihi

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

WALIMU wametakiwa kuwafundisha watoto kuandika fasihi kutokana na kuwasaidia kuelewa kwa haraka na kuimarike mapema.

Hayo yameelezwa na Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kiswahili Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Vida Mutasa, alipokuwa akizungumza kwenye Tamasha la Fasihi lililofanyika mwishoni mwa wiki mjini Kisarawe.

Mutasa alisema ni vyema walimu wanaowafundisha wanafunzi uandishi wa fasihi, wawafundishe pia kuandika kupitia hadithi mbalimbali ambazo zitawafanya kuwa na vitabu watakavyoviuza na kujipatia kipato.

Aidha, alisema ili uhamasishaji huo na umuhimu wa kuandika fasihi uonekane waandaaji wa tamasha hilo ambao ni Mfuko wa Fasihi Tanzania (TAFF), wanatakiwa kufika katika maeneo mbalimbali nchini badala ya kuishia Kisarawe pekee.

Mkurugenzi wa TAFF, Hussein Wamaywa, alisema wamefanya tamasha hilo kwa lengo la kuwatambua waasisi wa fasihi, kutoa tunzo kwa washindi na kuwaunganisha wadau wa fasihi pamoja kujadili mambo yatakayoenda sambamba na kuhamasisha uandishi wa vitabu.

Mratibu wa tamasha la pili la fasihi ya Kiswahili Tanzania Mwamwingila Goima, alisema kitabu kila mahali, kusoma siachi ng'o ni kampeni mahsusi iliyoanzishwa ili kuibua na kukuza uandishi wa kazi za fasihi kwa ngazi mbalimbali tokea kwa watoto, vijana mpaka watu wazima.

Alisema lengo ni kuhamasisha jamii kuhusu utunzaji fasihi kwa njia ya machapisho, utambaji wa hadithi na shughuli mbalimbali zinazoakisi fasihi ya kitanzania.

"Kampeni hii imeanzia Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani, mwaka 2018 na 2022, hii inatuonesha kuhusu nafasi ya kitabu katika jamii zetu kadhalika ahadi ya mwanajamii katika kukikumbatia kitabu bila hofu."

Kitabu humjengea mtu maarifa pamoja na uelewa wa mambo mbalimbali yanayoizunguka dunia, pamoja na kuibua fursa za kimaendeleo zilizojificha ambazo ni nadra kwa mtu yeyote kuzifuma na kuziona katika macho ya kawaida," alisema.

Wensesilaus Kidakule, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kimani Kisarawe aliibuka mshindi wa kwanza kwa shule za sekondari kwenye uandishi wa fasihi.

Aliwashauri wanafunzi wa shule nyingine kuanzia za msingi kujenga tabia ya kuandika fasihi, kusoma vitabu bila kujali mkondo wa masomo wanayosoma kwa kuwa kwa njia hiyo itakuza Kiswahili katika maeneo mbalimbali nchini.

Shadya Muhidini, mwanafunzi wa darasa la sita Shule ya Msingi Masaki, aliibuka mshindi upande wa shule za msingi kutokana na hadithi yake iliyomhusu kijana aliyemaliza masomo ya mtandao na kutumia vibaya elimu yake, aliomba walimu kuhamasisha uandishi wa fasihi shuleni kukuza Kiswahili.

# Ofisa apewa tuzo kwa mchango wa kusaidia wachimbaji wadogo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

CHAMA cha Wachimbaji Madini wa Mkoa wa Manyara (MAREMA), kimempatia tuzo ya utumishi uliotukuka, Ofisa Madini Mkazi wa Mirerani, Fabian Mshai, kutokana na mchango wake katika sekta ya madini kutoacha shaka kwa wadau anaowahudumia.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi tuzo hiyo, Katibu wa MAREMA, Tawi la Mirerani, Rachel Njau, alisema wameamua kumkabidhi tuzo yao Mshai kwa kutambua mchango wake kwa muda wa miaka miwili aliyowatumikia wachimbaji wa madini ya tanzanite yanayopatikana Simanjiro, mkoani Manyara.

"Mshai amekuwa na mafanikio makubwa kwenye utumishi wake, hivyo tumeona tumpe tuzo hiyo ya heshima iliyotukuka ili apate faraja huko anakokwenda. Kutambua mchango wa mtu mwingine ni jambo zuri katika maisha na inajenga heshima na imani kwa jamii na serikali kwa ujumla wake, kwamba ni mtu anayeaminika," alisema.

Mshai ambaye ni Ofisa Madini wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, anakwenda kusomea shahada ya pili ya fani hiyo katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Katika hafla hiyo ya makabidhiano, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alimwelezea Mshai kwamba mara zote alikuwa anawatetea wachimbaji wadogo ili kuhakikisha uchumi wao unakuwa mzuri.

Mmoja wa wamiliki wa mgodi wa madini ya tanzanite, Fatuma Kikuyu, alimkabidhi Mshai Biblia na taji la maua ili kuonyesha kwamba anakokwenda kila mahali anapaswa kuthamini mchango wa wachimbaji.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Mshai aliishukuru MAREMA Tawi la Mirerani, kwa kumpatia tuzo hiyo, kwa kuwa imempa imani kubwa na kumbukumbu isiyofutika kwenye maisha yake.

"Kama unafanya kazi kwenye jamii na wao wakaona unafanya jambo kubwa na kukupatia tuzo unapaswa kushukuru tangu mwaka 2017 nilipokuja Mirerani, miaka mitatu nikiwa afisa wa kawaida na miaka miwili nikiongoza ofisi," alisema.

Mbali na tuzo hiyo, pia MAREMA imewakabidhi vyeti vya kutambua michango yao kwenye sekta ya madini, baadhi ya kampuni ikiwamo Bilionea Saniniu Laizer, Bilionea Anselm Kavishe, Franone Ltd, Chusa Mining na God Charity.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Edward Mgaya (kushoto), jana akiwakaribisha wageni kutoka Taasisi za Vyuo nchini Canada (CICan), ambao wamejipanga kutekeleza mradi wa kujengea ujuzi vijana (ESP) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, mradi huo unafadhiliwa na serikali ya Canada kupitia Global Affairs Canada unaotarajiwa kutekelezwa kwa miaka saba. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kampuni kuchunguzwa mkataba hewa TANESCO

**Novatus Makunga,**
ARUSHA

KITENGO Maalum cha Polisi kinachoshughulikia Diplomasia na Utalii, kimepewa kazi ya kuchunguza mwenendo wa Kampuni ya Kimataifa ya Cosortium Energo Invert ya Bosnia, iliyoshinda zabuni ya mradi wa ujenzi wa kituo cha kupozea umeme wa msongo mkubwa, unaotoka Singida/Namanga hadi Lemuguru, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha.

Uamuzi wa kuichunguza kampuni hiyo ni kutokana na tuhuma za kukiuka makubaliano ya mkataba, kati yake na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), ulitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela.

Kwa mujibu wa Mongela, kampuni hiyo imeingia mkataba wa siri wa utekelezaji wa mradi huo na kampuni nyingine ya SPK Power ya India bila kuihusisha serikali ya Tanzania.

"Huo mkataba TANESCO inadai haiutambui na inashangaa kazi kubwa ikifanywa na Kampuni ya Sky Outdoor ya Tanzania. Hakuna kinachoendelea chenye tija zaidi ya mradi huo wa kitaifa kusuasua kwa kuwa ulipaswa uwe umekamilika mwaka 2020.

"Mradi huo wa msongo mkubwa wa umeme unaanzia Singida hadi mpakani mwa Tanzania na Kenya, ambako kiko Kijiji cha Lemuguru. Kituo hicho kitakapokamilika, kitakuwa na uwezo wa kupoza umeme wa kilowati 220 pamoja na kilowati 400," alisema.

Kutokana na tuhuma hizo, Mongela alisema: "Naagiza maofisa wa Jeshi la Polisi, wapelekeni hawa makandarasi katika Kitengo maalumu cha Polisi cha Masuala ya Utalii na Diplomasia, mkawahoji.

"Polisi chukueni huyo Meneja wa Fedha na Biashara wa Kampuni hiyo, Erol Merdzanic, na Meneja Msimamizi wa Kazi, Nedm Politak. Na ninyi maofisa wa Kampuni ya Cosortium Energo, tusaidieni meneja wa mradi huu, Irfan Djogic, ambaye inadaiwa ametoweka na hajulikani yuko wapi ajisalimishe."

Baada ya kuwekwa chini ya ulinzi, Merdzanic alipoulizwa bosi wake yuko wapi, alisema hajui aliko kama alivyotakiwa kumsalimisha.


Kabla ya Mongella kutoa maelekezo ya kukamatwa na kuhojiwa maofisa hao, aliwalaumu maofisa wa TANESCO wanaosimamia mradi huo, akiwamo Mhandisi Blandina Joachim, kwa kushindwa kusimamia mradi huo.

"Mkurugenzi Mkuu (Mtendaji) wa TANESCO, lazima mlete mtu ambaye atawamudu watu hao na si huyu Blandina. Huyo ni vyema mkampangie kazi nyingine kwa kuwa haiwezekani yupo hapa anashindwa kufahamu meneja wa mradi yuko wapi," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Kanda ya Kaskazini wa TANESCO, Fedgrace Shuma, alimweleza Mongela kwamba walibaini udanganyifu wa mkataba huo baada ya muda kwamba kampuni hiyo iliingia mkataba wa siri na kampuni hiyo ya India, pasipo kushirikisha shirika hilo.

Alisema kutokana na uhamishaji wa mkataba huo kinyemela, hivi sasa kumekuwa na migogoro ya wafanyakazi kutolipwa mishahara kwa kuwa kuna mkanganyiko wa ubia na Kampuni ya Sky Outdoor, ambayo umiliki wake kwa asilimia 100 ni wa Tanzania.

Alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, mwakilishi wa SKY Outdoor, Albert Joseph, alisema walilazimika kukatisha kazi ya ujenzi wa mradi huo Julai, mwaka huu, kutokana na kutolipwa gharama yao ya ujenzi.





# TAKUKURU yachunguza miradi ujenzi madarasa kwa tuhuma za ubadhirifu

**Na Jaliwason Jasson,**
KITETO

MIRADI ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo na nyumba za walimu, iliyokuwa ikitekelezwa katika Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, inachunguzwa kutokana na tuhuma za ubadhirifu.

Miradi hiyo inatekelezwa kwa fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVICO-19.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Manyara (TAKUKURU), Suzana Raymond, alisema jana kuwa mbali na miradi hiyo, katika wilaya zote za mkoa huo, wanachunguza miradi mingine inayohusisha sekta za madini, afya na maji.

Suzana alidokeza hayo jana kuhusu kuanza kwa uchunguzi wa miradi hiyo, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa TAKUKURU, kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

"Kwa miezi mitatu iliyopita, TAKUKURU imefuatilia miradi 10 ya maendeleo katika Mkoa wa Manyara, yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 7.34. Sasa katika ufuatiliaji wetu, tumebaini mradi mmoja huko wilayani humo una viashiria vyote vya ubadhirifu wa fedha.

"Tayari tumeanzisha uchunguzi wa awali kuhusu miradi inayotiliwa shaka. Siwezi kutaja lakini miradi tunayochunguza ni ile inayohusu sekta za madini, afya, maji na miradi inayotekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVICO-19," alisema.

Pia Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema walifanya ufuatiliaji wa michango inayokusanywa kutoka kwa wananchi, kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa baadhi ya vijiji vilivyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

"Katika ufuatiliaji huo, ulibaini kuwa viongozi wa vijiji wanaokusanya michango hiyo kutoka kwa wananchi walikuwa hawazingatii sheria, kanuni na taratibu za fedha wakati wa ukusanyaji na utumiaji wa fedha hizo."

Alisisitiza kuwa, jambo hilo linasababisha kuwapo kwa matumizi ya fedha mbichi pasipo kupelekwa benki, kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za ukusanyaji wa mapato na matumizi pamoja na makusanyo ya fedha kutoka kwa wananchi kutokupelekwa benki kwa wakati.




Mwanzilishi na Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya FRED TREKKING & SAFARIS Moshi, Fredrick Elihuruma Mkonyi (wa nne kulia), akiwa na wageni wake kutoka mataifa mbalimbali katika Ziwa Momella mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Bil. 45/- kutekeleza uwezeshaji ujuzi

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

SHIRIKISHO la Vyuo na Taasisi za Ufundi za nchini Canada (CICan), limetenga zaidi ya Sh. bilioni 45, kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Uwezeshaji kupitia Ujuzi (ESP), unalenga kuwanufaisha zaidi watoto wa kike na wanawake 7,000 nchini.

Mradi huo wa miaka saba (2021 -2028) unatekelezwa na CICan kwa ubia na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (DTVET).

Akizungumza jana jijini Arusha kuhusu mwelekeo wa ubia, Mshauri wa Mradi wa ESP, Dk. Alice Mumbi, alisema mradi huo unalenga kuimarisha njia mbadala za elimu, ajira, kujiajiri na kufungua fursa za ujasiriamali kwa wanawake na wasichana.

"Mradi huu utafanya kazi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) na Asasi za Kijamii (CBO) katika jamii nchini Tanzania. Kimsingi, unalenga kuongeza viwango vya ushiriki, kati ya wanawake na wasichana kupitia programu za mafunzo ya ujuzi na kuboresha upatikanaji wa mafunzo ya biashara, ujuzi, jinsia na haki za binadamu katika jamii zao.

"Vilevile, mradi huu utapanua fursa katika sekta rasmi na zisizo rasmi kupitia usaidizi, baada ya mafunzo ili kuingia kwenye ajira au kujiajiri. Mradi huo utafanya kazi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 12 vilivyochaguliwa pamoja na Asasi za Kijamii 12 zilizochanguliwa," alisema.

"Hawa wote wataanzisha mtandao wa timu za jinsia na washauri wa kike, kushirikisha jamii katika shughuli za kukuza uelewa wa kijinsia, juu ya faida za elimu kwa wanawake na uwezeshaji wa kiuchumi. Tunawajibika kutoa mafunzo endelevu kwa washirika hao ya kujenga uwezo katika usawa wa kijinsia, haki za binadamu, mbinu za ufundishaji na mafunzo ya watu wazima," aliongeza.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, akizungumza katika kikao hicho, alisema wizara hiyo ni muhimu katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) hasa kwa kuwawezesha wanawake kufuata fursa za kiuchumi na kijamii, kuendeleza mazingira wezeshi kwa mahusiano ya usawa wa kijinsia na kwa kusaidia nafasi salama kwa wanawake katika jumuiya zao.

Naye Mkuu wa Uendeshaji na Mshauri na Masuala ya Kimataifa wa Canada, Bronwyn Cruden, alisema serikali ya Canada inajivunia kuunga mkono ukuaji wa mpango mpya wa mwitikio wa kijinsia nchini Tanzania kupitia mpango wa uwezeshaji kupitia ujuzi.

Kwa mujibu wa Cruden, ESP inatoa fursa kwa Canada kuendeleza uwekezaji wake mwingine katika maeneo ya utekelezaji ya elimu, usawa wa kijinsia, haki za binadamu na ukuaji wa uchumi, ambao unafanya kazi kwa kila mtu.

Makamu wa Rais wa CICan, Alain Roy, alisema vyuo na taasisi za Canada, vinajivunia kupewa fursa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Masuala ya Kimataifa ya Canada, kufanya programu hiyo kwa washirika wa FDC na AZAKI.

# Wapinga uamuzi wa kufutwa kazi

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

WAJUMBE wa Bodi ya Wadhamini ya Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Burunge, waliofutwa kazi baada ya kutuhumiwa kuligomea Baraza la Uongozi (AA), kuvunja mkataba na Kampuni ya Uwindaji wa Kitalii ya EBN ili kupisha uwekezaji wa kampuni nyingine, wamepinga uamuzi huo.

Mbali na wajumbe hao, pia Baraza la Uongozi linadaiwa kumsimamisha kazi, Katibu wa Jumuiya hiyo, Benson Mwaise, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma inayomkabili ya kukubali kutia sahihi mkataba na Kampuni ya EBN, ambayo inafanya utalii wa picha katika kitalu hicho, ambacho kinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Uamuzi wa kupinga azimio hilo la AA, lilitangazwa jana na mmoja wa waathirika hao, Lembrice Makao, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hatua ya Baraza hilo kuwafuta kazi Wajumbe wa Bodi na kumsimamisha kazi Katibu wao.

"Kilichofanyika ni vurugu za viongozi wachache wa baraza, ambao wanashinikiza kuvunjwa mkataba na Kampuni ya EBN, huku wakitaka iingie makubaliano na Kampuni nyingine ya Uwindaji wa Kitalii.

Baraza hilo, halina mamlaka ya kisheria kuondoa Bodi ya Wadhamini, kwa kuwa Bodi imesajiliwa kisheria.

"Kwanza hawajui sheria, siku Bodi ya Wadhamini ikiondoka, Baraza nalo linavunjika kisheria. Tunasubiri watuandikie barua zao ili tuwafunde nao kwa kuwapa kwanza elimu na maelekezo," alisema.

Aidha, Makao, alisema mkataba na EBN, ulisainiwa baada ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kutoa baraka baada ya kufanya tathimini na ilishirikisha Kamati ya Ushauri ya Maliasili ya Wilaya, Maofisa kutoka Taasisi za Uhifadhi ikiwepo Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA).

"Tunashangaa kwa nini wanalazimisha, wakati Wizara iliunda kamati ikiongozwa na Mwanasheria wa Wizara, ikaja kufanya tathimini, walikaa siku nne huku Burunge na baadae walitoa barua kuridhishwa na mwekezaji na tuendelee na kutia sahihi mkataba. Inashangaza leo hiyo hiyo wizara inageuka na kuja kudai hatukufata taratibu,"alieleza.

Meneja Uhusiano wa EBN, Charles Sylvester, akizungumzia mgogoro huo, alisema vurugu kuhusu kitalu hicho, inachochewa na watu wachache kwa maslahi yao, ikiwepo kutaka kuwinda jirani na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Alisema EBN ni Kampuni ya Kimataifa ya Utalii inayomilikiwa wa wawekezaji wakubwa wa utalii kutoka nchini Ufaransa, ambayo tangu mwaka 2013 imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 20, hoteli na kufanya utalii wa picha na kuajiri wafanyakazi 240.

"Tunaomba serikali ifanye uchunguzi kuhusu mgogoro huu, kwa sababu EBN ilifuata taratibu zote, kabla ya kutiwa sahihi mkataba huo, lakini kinachofanyika sasa ni hujuma kwa maslahi ya wachache,"alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 22, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



**Inawezekana mifumo ya kidijitali haifai kutumika mazingira yote**
Ukurasa 17



Ukurasa 14
Kusifia, kuwatunza wanaonengua majukwaani shuleni, asema ni kuharibu hatima ya maadili



Ukurasa 15
**AJALI YA BUKOBA**
**Injinia: Tuanze kufundisha abiria kujiokoa kwenye mwendokasi, mabasi**

ELIMU

NA BEATRICE SHAYO, ALIYEKUWA MPWAPWA

# Ijue shule wanafunzi wanaotembea k'mita 7, wamo wa darasa kwanza

- Wanafika hoi, wengi wageuka watoro
- Walianza 199, wamehitimu la saba 60

WANAFUNZI kutembea umbali wa kilometa saba wanapoenda shule kila siku, imetajwa moja ya changamoto ya utoro katika Shule ya Msingi ya Sazima, iliyoko Kata ya Mima, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Inaelezwa kuwa wanafunzi hao wakisharudi nyumbani, siku inayofuata, baadhi yao hushindwa kwenda shule kutokana na kutembea umbali marefu, hasa wanaotoka kitongoji cha Mseche, Chehanga na Mgogo. Ni shule iliyoanzishwa mwaka 1970, iko kilomita 46 kutoka mjini Mpwapwa.

Mbali na kuchelewa kufika shuleni, wanafunzi hukosa somo la Hisabati, wengi wao ni wanaotoka katika vijiji hivyo wamejikuta wakifeli somo hilo.

Mwaka huu inaelezwa wanafunzi waliohitimu darasa la saba walikuwa 60, kati yao wavulana ni 32 na wasichana 28 ambao darasa la kwanza walipoanza walikuwa 199 wavulana 100 na wasichana 99.

Mwanafunzi Mola Malugo (15) wa darasa la sita katika shule hiyo, anayeishi kitongoji cha Mseche, anasimulia ugumu anaokutana nao anapoenda shule, akitembea umbali mrefu.

Anasema, hutoka nyumbani majira ya saa 12 alfajiri na kufika shuleni kati ya saa mbili hadi saa mbili na robo asubuhi, jambo linalomfanya akose kipindi cha kwanza cha masomo.

"Kuna wanafunzi wenzangu, huwa wanachoka na kuacha kwenda shule siku inayofuata. Mimi huwa ninajitahidi nisikose shule,"anasimulia Malugo, anayeeleza huwa anatoka shule saa 9:30 alasiri na kufika nyumbani saa 12 jioni, akikutana na majukumu mengine nyumbani.

Anasema ni hali inayomnyima muda wa kujisomea, kwani anapofika, anahamia jukumu la kwenda kuchota maji katika visima vya kienyeji na endapo akikuta foleni humlazimu kusubiri ili arudi nyumbani na maji.

"Unafika nyumbani umechoka, naambiwa nikachote maji ukirudi unakuta vyombo vinanisubiri nivioshe tunachoka hatuna namna,"anasema Malugo, akidokeza ni hali inayomyima muda wa kujisomea.

### WAZAZI NA WALEZI

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Chihanga, Henry Sudani, anasema wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa shule katika vitongoji hivyo, hata inawalazimu wanafunzi wao kutembea zaidi ya saa mbili hadi tatu, hata wanakosa kipindi cha kwanza kila siku, hali inayowatesa wazazi.

Mkazi wa Kijiji cha Sazima, Ernest Makali, anasema kitendo hicho kimewasababishia wanafunzi kupata uvivu wakashindwa kufika shuleni, hivyo rai yao ni serikali iwasaidie kuwawezesha upatikanaji wa vituo shinikizi vya shule.

### DIWANI AFUNGUKA

Diwani wa Kata ya Mima, Bezarery Mnyambwa, anasema wanafunzi kutembea umbali kilometa saba, hata kuwa changamoto inayohitaji uangalizi wa serikali, ibebe jukumu hilo, hata kusaidia kuwapunguzia utoro.



Hali halisi ya darasa la shule hiyo, isiyo na samani. **PICHA: BEATREACE SHAYO**

Kwa mujibu wa Diwani Mnyambwa, changamoto iliowafanya waamue kufyatua matofali 10,000 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya awali katika kitongoji cha Mgogo, kuwanusuru wanafuzi kutembea umbali mrefu.

Mnyambwa anasema, kitongoji cha Makawira wamejenga madarasa manne, Igoji madarasa sita, tatizo lililoko ni namna ya kupata usajili,

Anasema mwaka jana, Mdhibiti Ubora wa Elimu, alipita mahali hapo kuikagua na baada ya hapo hawajapatiwa taarifa zaidi.

Anasema wakati wanajipanga kufanya uboreshaji wa majengo hayo, choo kilianguka na kuwalazimu kuweka nguvu kubwa ya ujenzi wa choo, ili kuwasaidia wanafunzi hao.

"Shule yenyewe hata useme unafanya uboreshaji ni kama tunajisumbua. Kwa ubovu uliopo, kinachotakiwa ni kujengwa upya shule ya tangu 1970, uchakavu wake ni mkubwa," anasema.

Anaeleza mshangao wake kwamba wilayani humo, hawajawahi kutembelewa na mamlaka za wilaya au juu zaidi, kukagua kile wanachokilalamikia licha ya taarifa zao kufikishwa mahali husika.

"Viongozi wapo, hawajawahi kuja hapa shuleni kujionea hali halisi ya hii shule na hata nyumba za walimu zipo katika hali mbaya,"anasema Mnyambwa.

### MWALIMU MKUU

Nipashe iliongea na Mwalimu Mkuu, Dotto Chawala, anayekiri changamoto mojawapo kwao ni wanafunzi kutembea umbali mrefu, hali inayochangia utoro kuwa juu zaidi.

"Leo mwanafunzi akija, kesho haji. Anakuwa amechoka na ukiangalia hawa ni watoto wadogo,

**INAENDELEA UK.18**

ELIMU

**NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA**

DIWANI ANAPOKEMEA

# Kusifia, kuwatunza wanaonengua majukwaani shuleni ni kuharibu



Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama, akiwa na wahitimu wa Shule ya Msingi Milo alipokemea ukiukwaji wa maadili kwenye burudani shuleni. **PICHA: JULiETH MKIRERI**

WASWAHILI husema mtoto umleavyo ndivyo akuavyo na kwa namna hiyo usemi huu pia unaendana na samaki mkunje angali mbichi, ni nahau na methali zinazowapa wazazi, walezi na walimu jukumu muhimu kwenye makuzi na malezi.

Misemo hiyo hutumiwa shuleni na walimu, wazazi na walezi nyumbani na jamii, ikiwa ni kwenye kuwakanya na kuwaongoza watoto kwenye malezi mazuri hasa kwenye hatua za mwanzo wakiwa wadogo.

Katika misemo hiyo ujumbe au ukweli unaonekana baadaye hasa inapobainika kuwa mtoto hakulelewa kimaadili akiwa mdogo na ukweli unapodhihiri kuwa usitegemee maadili mema wakati wa utu uzima kama mwanzoni mafunzo yalisahaulika.

Mazoea ya kufanya mambo yasiyo na maadili kama kucheza muziki, kunengua mbele za watu bila maadili huku jamii ikiwatunza fedha na kuwashangilia watoto shuleni ni mambo yanayoelezwa kuwa yanapeleka maadili kombo.

Nipashe inakutana na Diwani wa Vigwaza Halmashauri ya Chalinze, Mussa Gama anayekemea muziki usio na maadili kwa watoto shuleni, ambao anasema ukiendelea kuruhusiwa kizazi cha baadaye hakitakuwa na maadili, heshima na hata utu na kujithamini.

Tofauti na ilivyo kwa wageni rasmi kwenye maeneo mengine shuleni kwenye burudani hasa wakati wa kucheza kuimba na kushangilia, mambo yanayofurahisha ikiwamo miondoko mbalimbali ya muziki na dansi kama singeli, bongo fleva au mchiriki ambayo imeenea sana mijini, Gama anakasirishwa.

> Hili halifai na tabia hii sitaivumilia mtoto kasimama hapa mbele anakatika ananengua mbele yetu halafu tunatoka wazazi kwa walezi kuwatunza kuonyesha wanafurahishwa hili siyo nzuri kabisa.

Anakemea wanafunzi kucheza mbele ya wazazi, walezi, walimu na hadhira inayokuwa mbele yao kwa mwenendo wa kukosa maadili na kuonyesha upotovu mkubwa.

Akiwa katika Shule ya Msingi Ruvu, alipoalikwa kama mgeni rasmi kwenye moja ya shughuli shuleni hapo, anakemea kitendo cha wazazi kufurahia miondoko ya muziki ambayo ilikuwa haiendani na maadili na kuwatunza kwa fedha.

Gama anawaeleza walimu, wazazi na wazazi kuwa na mabadiliko na kuacha kufurahia wanafunzi kucheza miondoko hiyo kama 'singeli' bongo fleva ambayo isipokemewa baadaye itawafanya wapotoke kimaadili.

"Tumeona watoto wetu wamecheza na sisi wazazi tunashangilia na kuwatunza hii siyo tabia nzuri tena siyo malezi kwa watoto wadogo kama hawa kukatika, kuzungusha nyonga mbele zetu namna hii, nawaomba tuwasimamie kwenye maadili mema tusiunge mkono haya yanayofanyika hapa".

"Tukiwashangilia sana tutambue baadaye wataharibikiwa tuwasimamie katika maadili yanayotakiwa na kwenye masomo wapende elimu ili watumie vyumba vya madarasa vinavyojengwa na fursa ya serikali kugharamia elimu tusipokuwa makini hawatasoma watajikita kwenye muziki zaidi tena uliojaa maneno machafu, matusi na kunengua kusikowajenga," anasema Gama.

Akiwa katika Shule ya Msingi Vigwaza, Gama anaendelea kusisitiza kauli yake ya wanafunzi kuachwa ovyo wakacheza muziki wenye miondoko ambayo haina heshima.

Anatoa maelekezo kwa Mwalimu Mkuu pamoja na Mtendaji wa Kata Vigwaza kuhakikisha kwenye mahafali mengine hali hiyo haijirudii badala yake wanafunzi wafundishwe nyimbo zenye heshima, michezo bora na yenye kushirikiana na Watanzania wengine kama wimbo wa Taifa, wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazoendana na maadili na uhalisia wa kile wanachokiendea.

"Hili halifai na tabia hii sitaivumilia mtoto kasimama hapa mbele anakatika ananengua mbele yetu halafu tunatoka wazazi kwa walezi kuwatunza kuonyesha wanafurahishwa hili siyo nzuri kabisa," anasisitiza Diwani Gama.

Anatumia muda huo kuwakumbusha wazazi, walezi na walimu kusimamia suala la elimu na kuachana na hali ya kujikiti kuwapongeza namna ya kucheza muziki kwa mienendo ya kunengua tena isiyofaa.

### NGOMA, MILA MBOVU

"Twendeni tukawasimamie watoto wetu kwenye suala la elimu tusiwaachie walimu pekee, tukumbuke kwa kufanya hivi tunawaandalia maisha ya baadaye ili wakidhi vigezo vya kuajiriwa, kujiajiri, kuwa viongozi na hata kuongoza familia zao," anasema Gama.

Gama anawasisitiza wazazi na walezi kuungana na walimu ili kukuza ufaulu na kuwa na wanafunzi wenye uelewa kwenye masomo na wenye maadili mema.

"Mtoto asipofaulu mtawalaumu walimu katika ufundishaji kumbe wote mnatakiwa kushirikiana wanaporudi nyumbani kuwasimamia, kazi za shule, kuangalia madaftari na kazi, kufuatilia mahudhurio na kuwakumbusha waliyosoma na kufuatilia mienendo yao wakiwa darasani na mitaani". Anasema.

Akizungumzia suala la mila za ngoma kwa watoto wa kike, anasema wazazi na walezi waachane nazo kwani wanatakiwa kubadilika na kuanza kuwacheza watoto wao wakiwa wamehitimu kidato cha nne.

"Tunapowacheza wakiwa shule za msingi bado wanakuwa na mambo mawili wanayoyaweka kichwani na katika kuyafanyia kazi ndiyo unakuta wananiingiza kwenye mahusiano wakiwa wadogo. Tunaanza tena shida ya mimba za utotoni na mabinti kutosoma".

### ANAUNGWA MKONO

Mmoja wa wazazi mwenye wanafunzi shule hapo mkazi wa Vigwaza, Mwanahamisi Juma anasema tabia ya wanafunzi kucheza kwa miondoko isiyo na maadili imezoeleka na wazazi pamoja na wamekuwa wakijisifu watoto wao wanavyofanya.

Anasema wanatakiwa kuungana na kufuata maelekezo ya diwani huyo ili kuwaweka salama watoto wao hususani wa kike ambao wengi wanaingia kwenye vishawishi wakiwa wadogo.

"Tusipowarekebisha mapema tukiwasifia kunengua baadaye tutashindwa kuwapangia njia sahihi ya kufuata na tayari dunia itakuwa imeshawaonyesha njia nyingine mbovu inayowaumiza ninawaomba wazazi tubadilike" anasema Mwanahamisi.

Abdallah Bakari mlezi na mzazi makazi wa Vigwaza anasema kuna wakati wanashindwa kuwaeleza walimu kwa namna wanavyowaandaa wanafunzi kwenye sherehe za maafali hasa kwenye burudani licha ya kwamba hata wao hawafurahishwi.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Vigwaza Paul Mwanilezi, anasema wako tayari kutekeleza maagizo yaliyotolewa na diwani huyo na kukaribisha maoni na ushauri mwingine unalinda makuzi na malezi bora ya watoto.

Anasema Diwani Gama ameagiza mabadiliko ya uchezaji muziki kwa wanafunzi na mavazi yao, yote akisema walimu watayatekeleza kwa wakati ujao.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

AJALI YA BUKOBA

# Injinia: Tuanze sasa kufundisha abiria kujiokoa kwenye mwendokasi, mabasi

• Video, maelezo ya Kiswahili yaandaliwe, kufunza wasafiri

MWEZI Novemba ulianza na ajali ya ndege, lakini mioyo ya watu inaendelea kutafakari ajali hiyo ya ndege ya Precision Air iliyotokea Bukoba na kuua 19 wakiwamo marubani wawili.

Tafakari ya ajali ina mambo mengi lakini, kubwa ni kuangalia wapi Watanzania walipoangukia au kukosea ili kubadilisha kasoro zilizosababisha watu kupoteza maisha ili zirekebishwe ajali zinapotokea madhara yapungue.

Ya Bukoba yanasubiri uchunguzi wa kitaalamu hivyo kuanzia sasa pengine ni kujielekeza kwenye hatua ziwe ni za kuokoa watu kwenye vyombo vya usafiri vinavyobeba abiria wengi.

Jijini Dar es Salaam kuna mabasi ya mwendokasi ambayo iwapo kukitokea hitilafu kwenye injini, au basi likishika moto na milango ikanasa ni lazima abiria wafahamu namna ya kujikokoa.

Ndani ya mabasi hayo kuna maelekezo yanayoeleza cha kufanya lakini watu wanafahamu?

Ni swali linalojibiwa na mbobezi wa uhandisi na teknolojia na mhadhiri mstaafu Dk. Kamugisha Byabato, anayesema kuna haja ya kuwaeleza tena, mara nyingi na mara kadhaa la kufanya iwapo ajali ikitokea.

"Kwenye basi karibu yote kila dirisha kuna maandishi yanayosomeka 'emergency door' mlango wa dharura, wakati mwingine kwenye kioo cha nyuma. Maandishi yanaambatana na namna ya kujiokoa tatizo likitokea."

Ndilo eneo la kuanzia maandishi hayo na maelezo yanayoambatana nayo yawe kuanzia sasa yaandaliwe kwa Kiswahili kama kuna tatizo iwe rahisi kusoma na kuchukua hatua, anasema.

Anakumbusha kuwa kwa mabasi hayo pia juu kuna 'vimilingo' ni kwa ajili ya kupitisha hewa, lakini ni sehemu ya kujikokolea.

Anasema iwapo kuna ajali watu wanaifungua kwa nguvu na kutoka kama basi limeanguka upande, yote hayo ni mambo ya kuwaelezea ili wayafahamu.

Kwenye mabasi yakiwamo ya mwendokasi na ya mijini, ya masafa au mikoani kuwaelimisha abiria jinsi ya kuchukua tahadhari ni suala muhimu lisilokwepeka sasa, anashauri Dk. Byabato.

Anawashauri wanaoohusika na usafiri kuanzia makondakta, madereva, mamlaka ya usafirishaji ardhini (LATRA), kikosi cha usalama barabarani, vyama vya kuwatetea abiria kutoa elimu ya kujiakoa kwenye vyombo vya usafiri angalau mara tatu.

"Tuanze na kutafsiri maelezo na alama zilizoweka, tuonyeshe pia sehemu za kujiokoa na namna ya kujiokoa. Baada ya kuweka taarifa kwa Kiswahili, kuwe na matangazo ya mambo ya kufanya ajali ikitokea. Ndani ya mabasi kuna redio na video uandaliwe ujumbe uliorekodiwa na kurushwa mara kwa mara watu wasikie na kuelewa" anasema Dk. Byabato.

Anakumbusha kuwa abiria wanatakiwa kufahamu kuwa kioo cha basi kikivunjwa ajali inapotokea hakiwi vipande vinavyoweza kukata na kuumiza bali vinasagika sagika na kuacha uwazi ambao watu watatoka kwa usalama.

Mhandisi huyo anaongeza kuwa masomo ya kujiokoa yanaweza pia kutolewa kwenye vipindi kwenye redio, televisheni, na mitandaoni.

Kwa mfano vipindi vya kipimajoto, meza huru na kumepambazuka, ili watu wajifunze na kuufahamu na virudiwe mara kwa mara.

Anasema ukweli ni kwamba kila wakati kuna abiria wapya kwenye chombo cha usafiri kuanzia meli, boti, daladala mijini, treni na mwendo kasi hivyo elimu inahitajika.

Anataka badala ya kuendeleza mijadala ya ajali ya ndege ya Precision ni bora kurekebisha makosa yanayoweza kusababisha watu wengi kupoteza maisha kwenye vyombo vya usafiri.

Anasema taifa linapofikiria maafa ya ajali ya ndege lina mambo mengi ya kuangalia, kurekebisha kasoro kuanzia ufahamu na utayari wa watu kukabiliana na maafa yanapotokea.

Kwenye masuala ya zimamoto ni vyema pia watu wakafahamu kuhusu viashiria vinavyotambulisha kuwepo moto na pia jinsi ya kuuzima unapotokea kwa kutumia vifaa vilivyopo kwenye vyombo vya usafari na kwenye makazi yao pia.



Abiria wakiwa ndani ya basi la mwendokasi. Ndani ya basi la mwendokasi ndiyo sehemu ya kuanza kutoa maelezo ya namna ya kujiokoa na kubadilisha maelekezo ya Kiingereza kuwa Kiswahili. **PICHA: BLOG YA BUNGE**

> Kadhalika ndege nayo ina mifumo mingi ya kufungua milango, tena kuna milango ya dharura, ya kuingilia kwa utaratibu wa kawaida na wataalamu wameweka mbadala ili kuleta ufanisi.

### MLANGO WA NDEGE

Mtaalamu wa masuala ya ndege anayezungumza kwa kuhifadhi jina lake anasema ajali ya Bukoba imeibua maswali mengi likiwamo la ni nani hasa aliyefungua mlango.

Akijibu swali iwapo ni mhudumu au Jackson Majaliwa, aliyeokoa abiria kadhaa anasema:

"Katika eneo la teknolojia na sayansi kwa ujumla kuna kitu tunakiita 'redundant system" ni utaratibu unaowezesha chochote kinachoundwa kuwa na njia na nyenzo mbalimbali za kufanyakazi ya aina moja."

Nitoe mfano hata katika uumbaji binadamu ana viungo viwili viwili angalia macho mawili, figo mbili na mapafu pia. Vyote vinafanyakazi moja. Si kwamba ukiumia jicho unashindwa kuona kabisa la pili lipo unaona tena kwa zaidi ya asilimia 60.

"Kadhalika figo moja inatosha lakini ziko mbili yote hayo ni kuwa na mfumo zaidi ya mmoja unaofanyakazi moja ili unaposhindwa, mwingine ufanye kazi kusiwe na kushindwa au kukwama.

"Kadhalika ndege nayo ina mifumo mingi ya kufungua milango, tena kuna milango ya dharura, ya kuingilia kwa utaratibu wa kawaida na wataalamu wameweka mbadala ili kuleta ufanisi.

"Kwa hiyo kama ilivyo milango hata magurudumu nayo yana 'mechanism' ya kufunguka na mmoja ukikwama mwingine na mwingine unatumika pia, hivyo si lazima kufikiria kuwa ni lazima mlango ufunguliwe na nguvu ya injini."

Anaeleza kuwa kuna mfumo unaofungua milango ya ndege kwa utaratibu wa mkandamizo mkubwa wa presha au hewa ambao unaibana.

Anafafanua kuwa unaitwa 'pneumatic system', tofauti na mfumo wa kufungua milango ya magari kama ya mwendokasi unaotumia 'hydraulic fluid'.

Anasema kwenye ndege mafuta hayo ya 'hydraulic fluid au vilainishi hivyo, havitumiki kwa sababu ya uzito hivyo mifumo ya uundaji imezingatia utaalamu wa kupunguza uzito angani.

Anafafanua kuwa hakuna haja ya kulumbana sana kuhusu kufungua mlango wa ndege kwa sababu taarifa za kisanduku cheusi itatoa maelezo na watu watauafahamu ukweli. Anasema baadhi ya mambo yanayoibuka kwenye ndege hiyo ni maswali yanayohoji kwanini ilianguka kama jiwe badala ya kusereraka kama ambavyo ndege zinafanya.

"Wanaofahamu masuala ya usafiri huu wanashangaa pia kuwa ndege ni kubwa na ina miundombinu na vifaa ambavyo vinaeleza na kutambua mambo mengi kwa mfano iwapo rubani anakaribia ardhi au maji inafahamishwa kulingana na mifumo na utambuzi ulioko ndani ya ndege ndiyo maana kuna maswali kuwa imekuwaje ikakimbilia majini?

Anafafanua kuwa ndege zinatua kwenye theluji na ukungu mzito na kwamba zina 'mechanism' au mifumo mingi ya kudhibiti ajali hivyo ni bora kuvuta pumzi kusubiri taarifa ya kisanduku cheusi.

Lakini, anaishauri serikali kuungalia upya uwanja wa Bukoba kwa sababu una mambo mawili ambayo ni vitendawili, mfano rubaini akikaribia uwanjani anakutana na milima.

Ajali ya ndege ya Precision Air ilitokea mwaka huu Novemba 6, na kuua watu 19 wakiwamo marubani wawili na abiria, tatizo likielezwa kuwa ni mvua iliyosababisha uwanja kutoonekana.

ELIMU

NA PILLY KIGOME

# Mara inaporejeshewa ‘msosi’ shuleni

MWANADAMU kama ilivyo mimea anahitaji mbolea ambayo ni lishe bora ili kukua na kustawi badala ya kusinyaa, kudhoofika na kudumaa kuanzia utotoni hadi hatua za mwisho za kukua.

Mwili na akili ya mwanadamu vinatakiwa kustawi kikamilifu ili kufanyakazi lakini akili nazo kuwaza na kuleta ufanisi katika kufikiri ipasavyo na kuchaji kila mara ili kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Wanafunzi kukosa mlo shuleni ni changamoto inayowakwamisha kielimu kwa vile njaa huutatiza mwili na uwezo wa kufikiria ambayo ndiyo akili, utatuzi wake uko kwenye kuwapa wanafunzi vyakula shuleni.

Ni mpango wa kutoa vyakula shuleni ili kuinua viwango vya elimu na afya ya uwezo wa akili kwa watoto kwenye mkoa wa Mara.

Kupata chakula pamoja na kufurahia masomo na kuhudhuria madarasani kwa juma lote ndilo lengo kwa kuwa wamekuwa na uhakika wa kurutubisha akili na miili yao na wakiwa shuleni.

Kwa kushirikiana na Ubalozi wa Marekani, wadau, wabunge wa mkoa wa Mara kwa pamoja wako katika mikakati ya kushirikiana kukuza taaluma kupitia mpango wa kutoa chakula shuleni, mradi unaojulikana kwa jina la “Pamoja Tuwalishe”.

Mradi huo unatarajiwa kuwanufaisha watu zaidi ya 355,000 wakiwamo wanafunzi, wanafamilia, walimu, wakulima na wanajamii wengine kwenye eneo la kuboresha taaluma shuleni.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo kwa niaba ya wabunge wa mkoa wa Mara, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na Mbunge wa Butiama, Jumanne Sagini, anasema mradi huo ni muhimu shuleni kwani unaleta tija na ufanisi mkubwa kwa wanafunzi.

Anaeleza kuwa wako katika juhudi za kurudisha mradi huu kwenye shule kwa kuwa unakuwa ni kivutio kikubwa kwa vile unaleta matokeo bora ya taaluma kwa kuupandisha ufaulu juu ukilinganisha na kukikosekana chakula shuleni.


Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, anasema kama hakuna chakula shuleni taaluma inashuka akikumbusha kuwa awali kulipokuwa na mlo kwa wanafunzi katika shule za mkoa wa Mara, walishuhudia taaluma na ufaulu ukipanda hadi kufikia asilimia 98 lakini mradi huo ulivyosimama taaluma ilishuka hadi kufikia asilimia 78.

Anafafanua kuwa mradi huo uliendeshwa kwa kipindi cha miaka 10 ukiibua mafanikio mengi katika shule za mkoa huo ambayo ni pamoja na wanafunzi kujua kusoma na kuandika kwa kiwango cha juu ukitofautisha na mambo yalivyokuwa wakati ule ambao hakukuwa na mlo shuleni.




Wanafunzi wakifurahia chakula shuleni. **PICHA: PILLY KIGOME**

> Pia na huduma hiyo ulituwezesha kulima bustani za mboga za aina mbalimbali, matunda na hata viazi lishe ambapo wanafunzi walikuwa wakijipatia chakula kwa wakati wote.



Naibu Waziri anaiomba Serikali ya Marekani wadhamini wakuu wa mradi huo kwa niaba ya wabunge wote wa mkoa wa Mara, waendelee kuwasaidia watoto wao ili kuweza kukuza elimu mkoani humo na pia afya, kwani uandikishaji wa watoto kuanza elimu ya msingi umeshuka wakati awali kulivyokuwa na mradi huo uandikishaji ulipaa na kufikia asilimia 98 na iliweza kuleta tija na ufanisi.

Anaendelea kuishukuru Wizara ya Elimu, ya Kilimo na Fedha kwa kukubali kurudisha huduma hiyo shuleni na kuipanua kwa vile mradi huo umeongeza mkoa wa Dodoma na baadaye unatarajiwa kuenea nchi nzima.

Naibu Waziri wa Kilimo wa Marekani, Jewel Bronaugh, anasema programu hiyo inatarajiwa kuinua ufaulu wa wanafunzi watakaoshiriki na kufungua fursa zaidi katika siku za usoni.

Anasema Wizara ya Kilimo ya Marekani kuanzia mwaka 2010 imetoa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 67 kwa ajili ya shule za mkoani Mara ili kuboresha lishe kwa wanafunzi ikiwa na lengo la kuinua taaluma, usafi wa mazingira na kuongeza mahudhurio madarasani.

Mradi huo uliwanufaisha zaidi ya wanafunzi 200,000 kutoka shule 231 kupitia shughuli mbalimbali zinazolenga kuongeza uwezo wa wanafunzi ili kuimarisha ufaulu na kuboresha afya na lishe zao.

Mkurugenzi wa Mradi wa Pamoja Tuwalishe maarufu Global Communities, Amina Mgeni, anasema mradi huo utakuja na mkakati wa kukomesha njaa za muda mfupi na mrefu shuleni.

Aidha, akifurahia kuwapo tena kwa huduma ya chakula shuleni, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Suguti iliyoko wilayani Musoma Vijijini, Yasinta Udecho, anasema ni mmoja wa walimu wanufaika wa mradi huo aliyeshuhudia mafanikio mengi.

Analiambia gazeti hili kuwa wamenufaika kwa kiwango cha juu na chenye tija kutokana na mradi huo wa chakula lishe shuleni kwa kuwa wanafunzi walikuwa wanapenda kufika shuleni kwa wakati na kiwango cha ufaulu kiliongezeka kwa kuwa chakula kilikuwa kinapatikana shuleni na kuwafanya wasome bila njaa.

Yasinta anaongeza kuwa, walianza kufaidika na mradi huo kuanzia mwaka 2017 hadi 2021 lakini pia Global Communities iliwajengea vyumba sita kwa ajili ya kupata hedhi salama kwa wasichana na hiyo ilileta tija shuleni hapo kwa kuwa wanafunzi wa kike walijihudumia shuleni kwa miezi yote ambapo awali kabla ya mpango huo wanapofikia hali hiyo walikuwa hawafiki shuleni.

“Pia na huduma hiyo ulituwezesha kulima bustani za mboga za aina mbalimbali, matunda na hata viazi lishe ambapo wanafunzi walikuwa wakijipatia chakula kwa wakati wote”.

Shule nyingine inayofaidika ni Shule ya Msingi Mgeta Wilayani Bunda, Mwalimu Mkuu, Anesta Ringo, anasema yeye ni mnufaika pia wa mradi huo shuleni kwake kwa kuwa wanafunzi walikuwa wanafurahia masomo na kulikuwa na ongezeko la ufaulu.

Anasema mradi huo ulitekelezwa kuanzia mwaka 2012 hadi 2020 na faida walizozipata ni nyingi ikiwamo na ongezeko la mahudhurio na kuliondoa tatizo la utoro madarasani.

Mwanafunzi Neema Masungwa, wa darasa la tano kutoka Shule ya Suguti anaiambia Nipashe kuwa wamefurahishwa na taarifa za mradi huu kurudi tena shuleni kwani unahamasisha kupenda shule na kukuza ufaulu pamoja na kuondoa utoro shuleni.

“Tumefurahi kwa kuwa kuna wenzetu wengine waliosuasua kufika shuleni kwa kusitishwa kwa mradi huo huenda sasa watarudi masomoni,” anasema.

ELIMU
**NA NIMI MWETA**

# Inawezekana mifumo ya kidijitali haifai kutumika mazingira yote



Mbolea ya ruzuku ndani ya maghala, lakini inamfikiaje mkulima ni swali linalotegemea utaalamu ukiwamo wa teknolojia ya kidijitali. **PICHA: MAKTABA**

KILIMO kinapoanza wakulima wanahitaji mbolea ya ruzuku ambayo wanatakiwa kusajiliwa, kupewa namba za siri na taarifa zao kuwekwa kwenye kanzi data. Ni suala la teknolojia

Karibuni viongozi wa mikoa ya Geita na Kigoma kwa upande mmoja, na Wizara ya Kilimo kwa upande mwingine, wamekuwa wakitafuta njia za kuondoa uhaba wa pembejeo hasa mbolea zinazouzwa kwa bei ya ruzuku.

Unapofuatilia kinachotokea inakuwa kana kwamba hakuna sababu ya uhaba wa pembejeo kwani kiasi kinachotakiwa kinajulikana ili mkwamo upo kwenye teknolojia ya usajili na utambuzi.

Taratibu zinazotumika zinaleta usumbufu kutokana na teknolojia iliyokuwa inatumiwa kusambaza haijawa na mafanikio kama ilivyokuwa ikitarajiwa.

Wengi kati ya wakulima waliofika ofisi za wilaya kununua pembejeo waliambiwa hawajapata namba ya siri au ya utambulisho wa kuandikishwa kuwa wanastahili kununua mbolea kazi inayofanywa kwa kutumia mifumo ya kompyuta.

Maelezo ya maofisa wa kilimo kwa upande fulani yanalenga kusema kuwa baadhi ya wakulima wanaulizia pembejeo wakati hawajaandikisha majina yao kama wahitaji, na kutambuliwa hivyo na serikali za mitaa, vyama vya ushirika na ofisi za usajilii wa wanunuzi wa mbolea.

Inavyoelekea ni kuwa waliokuwa wanahangaikia suala hilo walishafuata maelekezo hayo na walitazamia kuwa wakifika huko itakuwa ni suala la kupatiwa viwango vyao kwa kununua mbolea wanayohitaji.

Kwa upande wa pili, maofisa au mawakala wa kampuni ya usambazaji na ununuzi wa pembejeo za ruzuku ya pembejeo walielekea kuamini kuwa wakulima waliokuwa wakihangaika hawakuwa wamefuata utaratibu wa kuandikisha.

Ni katika taarifa za vyombo vya habari ikiwamo ITV, zinazobainisha hayo. Wakulima wanaeleza kuwa mkulima anaweza kujiandikisha hadi mwezi ujao iwe ni mwanzo au hata kuelekea mwishoni na kununua pembejeo.

Wakati wakulima walikuwa wanajua tarehe ya kuanza kulima ni kuelekea mwisho wa Oktoba, au mwanzo wa Novemba, hivyo suala la kutokuandikisha lilikuwa halipo.

Ina maana kuwa endapo yupo mkulima ameambiwa kuwa jina lake halipo katika orodha ya wahitaji, hivyo ni budi aandikishe upya, ni wazi atakuwa ameondolewa katika orodha, ili mtu wa ziada apate usajili na kiasi anachohitaji cha mbolea ya ruzuku.

> Kosa lilianzia hapo, kuwa kilichotangulizwa ni mfumo utakaotumika kuwa una sura ya uhakikisho, wakati kinachostahili kutangulia ni kununua pembejeo na wakulima.

Endapo watu kadhaa wanajikusanya na kuchukua namba za watu wengine wengi, wakabadili kiwango wanachohitaji, watakuwa na uwezo kujizolea tani elfu nyingi wakauze.

Hali hiyo ilionekana wiki chache zilizopita wakati kundi la wananchi katika njia ya vichochoroni wilayani Ileje inayoenda Malawi walisimamisha malori matatu yaliyoshukiwa kuwa na magendo, kwani njia hiyo haitumiwi na magari katika hali ya kawaida.

Wananchi waliweka vizuizi wakauarifu uongozi wa wilaya, ambako Kamati ya Ulinzi na Usalama ilijikusanya, huku polisi pia wakiwa wamearifiwa. Upekuzi ulifanyika na tani 40 za mbolea ziligunduliwa.

Ukiangalia kilichotokea unagundua kuwa licha ya kuwepo mfumo wa kidijitali wa kuandikisha wanunuzi wanaotarajiwa wa mbolea, wajanja hawakosi mbinu za kupitisha mahitaji yao, na inaelekea siyo kwa kutunga majina bandia pekee ila hata kutwaa majina halisi. Vinginevyo kusingekuwa na haja ya kuondoa majina katika orodha na kusema kuwa hawajaandikishwa.

Hao walioandikishwa ili kupeleka tani elfu kadhaa za mbola nchi jirani na kupata faida kubwa hawakuzuiliwa na uwepo wa mfumo wa kidijitali, ambao baadhi ya viongozi wanaupigia mbiu wakisema ni kama mwarobaini wa matatizo mengi wakisahau usemi kuwa ni kuvuna ulichopanda.

Kinachoonekana hapo ni kuwa dhamira inatawala, siyo suala la u-dijitali kumaliza matatizo, lengo ni kujinufaisha kupitia mbolea ya ruzuku na hilo ndilo lililoonekana.

Isitoshe, mfumo huo unaweza ukawa ni kosa kutumiwa katika eneo kama hilo, ambalo halina mtiririko halisi wa bidhaa ambao hata mwenye mali si rahisi kuukwepa na kutumia magendo.

Ni kama kujaza mafuta katika kituo cha kuuza petroli au dizeli, kuwa mifumo ya kujaza mafuta inaunganishwa moja kwa moja na chombo cha kufuatilia mtiririko wa bidhaa hiyo, kidijitali.

Kwa suala la kuuza mbolea ya ruzuku kwa njia hiyo, inasemekana kila mfuko utakuwa na 'stika,' yaani alama ya kutambulisha ni 'mzigo' wa ngapi katika kundi lipi, kama ilivyo tiketi ya basi.

Mifuko mingi iliuzwa inasemekana haina 'stika hizo ' kama ilivyotazamiwa, ambayo ina maana ni mifuko isiyoorodheshwa. Ukiangalia udhaifu huo wa kutumia stika kwa mauzo hayo ya pembejeo unapata swali la kuuliza, nini hasa kilicholengwa katika mfumo huo, na hao walioubuni walikuwa na ushahidi gani kuwa hakuna mianya ya kuhujumu utumiaji wake?

Kosa lilianzia hapo, kuwa kilichotangulizwa ni mfumo utakaotumika kuwa una sura ya uhakikisho, wakati kinachostahili kutangulia ni kununua pembejeo na wakulima.

Sera ikawa ni kurahisisha bei ya pembejeo na kutoa motisha kwa wajanja kujipenyeza na kuiuza kwa faida kubwa nchi za jirani, badala ya kutoa nzuri kwa mahindi, na kutoa kinga kwa wakopeshaji kama SACCOS wakubali kutoa mikopo kwa wakulima itumike kununua pembejeo kwa mfano kwa kuilipa kampuni husika pale mkulima akileta stakabadhi ya ununuzi huo.

Mawazo yanaweza kuwa mengi ila wajanja wameingiza serikali mjini kuwa kushabikia udijitali kindakindaki bila kuangalia mianya iliyoko ya kuhujumu, wabebe mbolea ya chee wanaendelea kufaidika wakulima wakisota.

# Ijue shule wanafunzi wanaotembea k'mita 7, wamo wa darasa kwanza

INATOKA UK.13

wanakata tamaa. Fikiria mtoto wa darasa la kwanza atembee kilometa saba wakati wa kuja shule, bado kurudi," anasema Mwalimu Mkuu.

Anashauri kungekuwapo vituo shikizi vya shule hiyo, ingewasaidia wasome darasa la kwanza hadi la tatu, kuwa karibu na vitongoji vyao na baada ya hapo watakuwa wakubwa kumudu kufika shuleni Sazima, katika umbali uliopo.

Chawala anasema, mwanafunzi anafika shule kati ya saa mbili na dakika 40 hadi saa tatu na ndio maana wanafeli katika somo la hesabu, kwa wanaotoka vitongoji vya mbali, wakiwakuta wenzao wameshasoma somo hilo.

## MAJENGO KUCHAKAA

Mwalimu Mkuu anasema, pia shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa majengo na haijawahi kufanyiwa maboresho tangu ilivyojengwa mwaka 1970, jambo linalohatarisha usalama wa wanafunzi.

Anasema, mazingira ya ubovu wa shule hata ukarabati wake bado ni tatizo na kunahitajika kujengwa upya. Anaendelea: "Kuna darasa ukiingia utaona mbao zinaning'inia ni hatari kwa wanafunzi.

"Hata choo hakuna! Awali kilianguka kutokana na mvua zilizonyesha, tukaamua kutumia choo mbadala ambacho kina matundu saba na chenyewe kimeshajaa."

Pia ana ufafanuzi kwamba kukabili changamoto hiyo, wananchi wameanzisha ujenzi wa choo chenye matundu 12, ambacho hakijakamilika.

## WANAKAA SAKAFUNI

Mwalimu huyo akiongea kwa masikitiko, anasema wapo wanafunzi wanakaa chini kwenye udongo, kwa kuwa sakafu imeshachoka, hivyo wanahitaji jumla ya madawati mpaya 120.

"Kama ulivyoona darasa la nne wanaanza mitihani (mwezi uliopita), tumeenda kuazima madawati katika Shule ya Sekondari ya Mima. Kila mwanafunzi anatakiwa kukaa dawati lake, madarasa manne hayana madawati ikatu-



Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Sazima, Mpwapwa, mkoani Dodoma, wakiwa katika safari ya kilomita saba kuelekea nyumbani. **PICHA: BEATREACE SHAYO**

bidi kwenda kuomba," anaeleza.

Anataja ambayo wanafunzi wake hukaa chini, ni wa madarasa ya tatu, nne la tano kutokana na ukosefu wa madawati.

"Darasa la kwanza wapo wanafunzi 106, dawati moja wanakaa hadi wanafunzi wanne na darasa la nne wapo 156, wengine wanakaa chini. Hii ndio hali halisi katika shule," anaeleza.

Chawala anasema, pia kuna upungufu wa nyumba za walimu, hata zilizokuwapo ni chakavu na zinahitaji kufanyiwa uboreshaji mkubwa.

"Katika nyumba tano zenye unafuu, ni mbili ambazo wanaishi walimu watano, mimi ninaishi katika kijiji cha jirani kwa sababu nyumba hazitoshi, Hivyo, ilinilazimu awali kuishi huko," anasema.

## WALIMU WACHACHE

Chawala anasema idadi ya walimu ikilinganishwa na ya wanafunzi haijitoshelezi, kwani walitakiwa wawe na walimu 20 na sasa waliopo ni sita na kujikuta wakifanya kazi katika mazingira magumu.

"Serikali imekuwa na changamoto ya kuhamisha walimu bila mpangilio wamewahamisha watu wakatuletea mmoja ambaye amechukua nafasi ya mmoja, ambaye alistaafu badala ya kuongeza idadi ya waliotoka wanatupatia pungufu," anasema.

Anasema, mwalimu mmoja anafundisha zaidi ya vipindi sita na yeye anafundisha, hivyo majukumu mengine ya kiutawala inakuwa ni shida kutokana na majukumu kuwa mengi.

## JANGA LA BODABODA

Anasema, tatizo jingine ni shule hiyo ambayo ipo karibu na barabara bodaboda zinapita kwa kasi, wanafunzi wana ugonjwa.

"Kama unavyoiona hii shule uwanja upo upande wa pili wa shule wanavuka barabara, inakuwa ni hatari kwa usalama wao bodaboda zinapita kwa 'spidi'. Hii inaleta changamoto kwa wanafunzi,"anasema.

Pia eneo la shule halina maji licha ya kuwepo kwa tangi la maji karibu, inakuwa changamoto ya kuwataka wanafunzi kutoka eneo la shule kwenda kutafuta maji.

Anasema mwaka 2020 kipindi cha likizo ya wanafunzi iliyotangazwa na serikali wakati wa ugonjwa wa Uviko-19 ulipoingia nchini wanafunzi watano walipata ujauzito.

"Hatujawahi kupata kesi nyingine ya wanafunzi kupata ujauzito ni kwa vile walikaa nyumbani muda mrefu na wazazi huenda hawakuwafuatilia,"anasema.

## MWENYEKITI KIJIJI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sazima, Joram Mkala, analalamika wamekuwa wakituma taarifa kwa viongozi wa Wilaya ya Mpwapwa, kuhusu changamoto zilizoko shuleni, matokeo yake hakuna kinachofanyika.

Anasema, wanaiomba serikali iwasaidie na kuona shule hiyo ipo ndani ya Tanzania na kuwapatia mahitaji muhimu kama ilivyo katika shule nyingine.

"Wanajua kuna tatizo la walimu, lakini wanawaondoa bila kuwaongeza hii ni shida mwalimu mmoja anaweza kuwahudumia wanafunzi 45. Hapa darasa moja unakuta wapo 156," anasema.

Anasema wanapoanzisha mradi, serikali ijitahidi kuwaunga mkono kama walivyoamua kujichangisha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo wasaidiwe katika kukamilisha, ili wanafunzi hao wasipate shida.

"Huu ujenzi wa vyoo kila mwananchi amechangishwa Sh. 10,000 bahati mbaya kuna ambao hawajaweza kuchangia na awamu ya pili tulipanga wachangie Sh. 5,000 kama unavyoona hali zao wengine wameshindwa," anasema.

Anakiri hoja kwamba, vyoo hivyo vinahitajika kukamilika kwa haraka kwani vinavyotumika haviwatoshelezi wanafunzi na tayari vimejaa.

## OFISA ELIMU

Ofisa Elimu wa Shule ya Msingi Wilaya ya Mpwapwa, Jackson Mpankule, alikiri shule hiyo ina upungufu wa walimu na tatizo hilo lipo na hata kwa shule nyingine.

"Kiukweli tunapokea walimu ambao wameomba kuhamia katika halmashauri yetu na kuwapeleka kule ambapo kuna mapungufu. Serikali imetuletea walimu 70 mwaka huu inajua hilo tatizo,"anasema.

Akijibu kuhusu ujenzi wa vyoo, anasema utaratibu wananchi wanapojenga majengo kwa maana ya maboma serikali inakwenda kukamilisha. Mpankule anasema, kwa sasa kuna mpango wa kujenga vyoo katika shule zote za wilaya kutoka katika mradi wa Benki ya Dunia (WB), ambavyo vitakuwa vya kisasa.

"Kwa kuwa wananchi wameshaanza kujenga tutakwenda kukamilisha huo ujenzi na tayari shule hiyo imetengewa Sh. milioni 8.6."

Kuhusu suala la usajili kwa shule shikizi, anasema utoshelezaji wa miundombinu ndio kigezo mojawapo cha usajili wa shule ambao hufanya na udhibiti ubora.

"Shule ikisajiliwa maana yake imekidhi vigezo ukiona haijasajiliwa maana yake haijakidhi vigezo," anasema.

Akijibu swali ya uchakavu wa majengo anasema shule hiyo imetengewa Sh. milioni 40 kwa ajili ya uboreshaji wa majengo.

## WANENAVYO MALENGA

### WABANGAIZAJI

Wapo wabangaizaji, kwetu kwao wengi sana,
Kujituma ni mtaji, wasiadhirike sana,
Na wala siyo kipaji, ni shida zinawabana,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Jinsi unabangaiza, hata Mungu akuona,
Njia yako aangaza, nawe uweze muona,
Hawezi kutelekeza, kesho yako taiona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Mifano iko lukuki, twasoma na tunaona,
Walisema hawatoki, sasa wanang'aa sana,
Vile hawakudiriki, nao kukubaliana,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Neno la Mungu lasema na hayo tunayaona,
Kwenye kazi zote njema, mwishowe kuna kuvuna,
Hivyo acha kulalama, ujishughulishe sana,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Mwenye nacho utaona, kama vile ajivuna,
Kumbe unavyomuona, alishapigika sana,
Sasa mwezi kauona, kivuli amekiona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Huyu Ruto twamuona, jinsi alibezwa sana,
Wengi walivyomuona, ya kwamba hafai sana,
Lakini aling'ang'ana, alipo tunamuona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Bangaiza bangaiza, kesho yako taiona,
Uzidi kujilemaza, utapata tabu sana,
Hilo linajieleza, na mambo tunayaona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Nami ninabangaiza, mwanga nipate kuona,
Mbele nikijisogeza, niweze kutulizana,
Kivuli cha kupendeza, nami niweze kiona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

**HABARI KITAIFA**

# UTT yajivunia ongezeko kiuwekezaji

**Na Frank Monyo**

TAASISI ya Uwekezaji ya UTT AMIS, imesema kuwa thamani ya Mfuko wa Umoja imeongezeka kutoka Sh. bilioni 612.8 kwa Juni 30, 2021 hadi Sh. bilioni 996.5 kwa Juni 30, mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji ya taasisi hiyo, ambayo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Jikimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simon Migangala, alisema ongezeko la Sh. bilioni 383.7 ni sawa na asilimia 62.6 ikilinganishwa na ongezeko la Sh. bilioni 206.8 sawa na asilimia 50.0 kwa mwaka uliotangulia.

"Haya ni mafanikio katika changamoto mbalimbali ambazo dunia inakabiliana nazo, huku uchumi wa Tanzania ukiendelea kufanya vizuri na kuhimili mtikisiko hasa uliosababishwa na matatizo ya vita nchini Ukraine," alisema.

Alisema ni kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa UTT AMIS na mifuko yake kushuhudia ongezeko kubwa kama hilo ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

"Ongezeko la ukubwa wa mifuko hiyo umeenda sambamba na ongezeko la idadi ya wawekezaji 29,832 sawa na asilimia 17.0 waliojiunga katika mifuko kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, mwaka huu, ikilinganishwa na wawekezaji 12,798 sawa na asilimia 8.0 waliojiunga katika mwaka wa fedha uliotangulia," alisema.

"Kama nilivyosema hapo awali, mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake. Faida kwa Mfuko wa Umoja ilikuwa asilimia 12.6 ikilinganishwa na asilimia 8.7 ya Kigezo Linganifu," alisema.

"Kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka Sh. bilioni 258.0 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2021 hadi Sh. bilioni 289.030 Juni 2022. Ongezeko hili la thamani ya Mfuko linatokana na imani ya wawekezaji pamoja na kueleweka kwa elimu inayotolewa kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja," alisema Migangala.

Aidha, alisema machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Pato la Taifa (Gross Domestic Product) lilikua kwa asilimia 5.4 katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia tarehe 31, Machi 2022 na asilimia 4.8 kwa robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2022, ikilinganishwa na asilimia 4.9 na asilimia 4.3 za robo ya tatu na ya nne za mwaka wa fedha 2020/21.

"Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu ya robo mwaka iliyoishia 30 Juni 2022, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.4 katika nchi za Afrika Mashariki na wastani wa asilimia 10.1 kwa nchi za ukanda wa SADC ukiondoa nchi ya Zimbabwe," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, alisema matarajio ya mwaka 2022/23 ya utekelezaji wa mpango mkakati wa UTT AMIS utakaoishia Juni 30, 2024, umekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa.

Kuhusu Mfuko wa Wekeza Maisha, Kyuki alisema mfuko huo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022 unaendelea kufanya vizuri na faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (performance Benchmark).

Alisema faida kwa mwaka ilikuwa asilimia 14.1 ikilinganishwa na asilimia 8.7 ya Kigezo Linganifu.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka Sh. bilioni 1.8 iliyofikiwa 30 Juni 2021 hadi Sh. bilioni 4.4 30 Juni 2022.

"Ongezeko hili la thamani ya mfuko linatokana na imani ya wawekezaji pamoja na kueleweka kwa elimu inayotolewa kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Mwenendo wa uchumi na mazingira katika masoko ya fedha, pamoja na changamoto mbalimbali ambazo Dunia inakabiliana nazo," alisema Kyuki.

## Mikakati kupunguza vifo vya wajawazito vyapamba moto

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wajawazito 300,000 wataondolewa katika hatari ya kupoteza maisha na watoto wao ifikapo 2024, kutokana na kuingizwa kwenye programu ya kupewa vifaa vya kujifungulia, huduma ya mazoezi na ushauri wa lishe.

Programu hiyo maalum iliyopewa jina la BUSELA yenye kauli mbiyu ya ujauzito wenye afya, mtoto mwenye afya inayosimamiwa na Kampuni ya Hatua.

Akizungumza wakati wa kugawa vifaa vya kujifungulia kwa wanawake 200 wenye ujauzito wa miezi sita mpaka tisa katika Hospitali ya Rangi Tatu, Mbagala, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Hatua, Derick Mgaya alisema lengo la kuanzisha huduma hiyo ni kuisaidia serikali kupambana na vifo vinavyotokana na uzazi.

"Lengo letu ni kuongeza nguvu ya kupambana na vifo vya kwakuwahamasisha wakina mama kuwahi kliniki mapema, kufanya mazoezi, kupata lishe lengo pamoja na kugawa vifaa vya kujifungulia kulingana na idadi ya vile tutakavyojaaliwa," alibainisha Mgaya.

Alisema kupitia programu hiyo wameshafikia wanawake wajawazito 2,000 ambapo lengo ni kuwafikia kinamama 300,000 ifikapo mwaka 2024.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema kampuni hiyo imefanya uamuzi sahihi wa kusaidia wajawazito, lengo ni kuona kwa mamna gani wanaisaidia serikali katika kuwafanyisha mazoezi ambayo ni changamoto kubwa inayosababisha wamama baada ya kujifungua kupata matatizo ya kiafya.



Kinamama wakitembeza mboga mitaa ikiwa ni mbinu mojawapo ya kujitafutia riziki kwa njia hiyo, Kigogo Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mradi wawezesha biashara endelevu mkaa

**Na Christina Haule,** Morogoro

MRADI wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) umetekeleza karibu asilimia 90 ya ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2015 katika Kijiji cha Lulongwe, Kata ya Matuli wilayani Morogoro.

Katika kutekeleza ilani hiyo, mradi huo umekamilisha miradi mitano ya maendeleo baada ya kukusanya zaidi ya Sh. milioni 250 kutoka kwenye usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii (USMJ).

Katibu wa CCM Kata ya Matuli, Abdalah Semindu, alisema hayo jana wakati viongozi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) wanaotekeleza mradi huo kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na ushirikiano la Uswisi (SDC) walipotembelea vijiji vyenye miradi kuangalia mafanikio tangu ianzishwe mwaka 2016.

Semindu alisema mwaka 2015 kwenye uchaguzi wakati akimnadi mgombea udiwani katika kata hiyo, Lucas Lemomo, katika kijiji hicho, aliahidi kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi ikiwamo ujenzi na vitu mbalimbali ambavyo hakujua namna ya kuvikamilisha.

Alitaja miradi aliyoahidi kuwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara ambayo ilikuwa inapitika kwa shida, ujenzi wa shule ya sekondari ya kata kwa kuongeza madarasa mawili ili itumike, uwapo wa vikundi vya hisa (VIKOBA), kuweka huduma za afya kwa kujenga zahanati ya kijiji ambayo haikuwapo na ujenzi wa nyumba za walimu.

"Mimi mkaa endelevu nauheshimu kweli kweli kwa sababu umenivika nguo. Nilipoahidi mwaka 2015 kuwa nitawaletea maendeleo, maendeleo yamebebwa na mkaa endelevu, nilisema mchagueni diwani wangu atafanya mambo moja, mbili, tatu, nikiwa sijui nafanyaje. Lakini baada ya mkaa endelevu ahadi zote nimezitimiza. Nadaiwa madeni madogo madogo kama maji hivi na ikifika mwaka 2023 nitamaliza madeni yote katika kata yangu," alisema.

Naye Diwani wa Matuli, Lucas Lemomo, alisema hali ya kijiji cha Lulongwe ilikuwa ngumu kimapato kabla ya mradi lakini baada ya mradi wamejengewa ofisi ya kisasa ya kijiji na kuepukana na adha ya mvua kwa kukaa chini ya miti sambamba na kuwa na masijala ya ardhi.

Alisema baada ya kufundishwa, wamefanya matumizi bora ya ardhi na wananchi kupatiwa zaidi ya hati 200 za viwanja na mashamba. Pia alisema wametumia asilimia 10 ya ardhi huku wakilinda asilimia 90 na kwamba asilimia 10 ya ardhi yenye msitu hutumika kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka 24 ili kukamilisha USMJ.

Lemomo alisema matumizi bora ya ardhi yanazingatiwa na wakazi wa kijiji hicho kwa asilimia 90 kwa sasa na kwamba zamani kabla ya mkaa endelevu kulikuwa na biashara kubwa ya mkaa uliovunwa holela wa baiskeli na pikipiki.

Lakini alisema kwa sasa hakuna sababu ya kuboresha uvunaji kwa kufuata utaratibu kwa mvunaji kuonyeshwa eneo husika na kamati ya misitu jambo lililovutia wateja kufika kijijini kupata mkaa na kununua sehemu moja.

# Rais Samia kuzindua mradi wa maghala ya chakula

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

RAIS Samia Suluhu Hassan, anaanza leo ziara ya siku moja mkoani Manyara, pamoja na mambo mengine, atazindua Mradi wa Vihenge na Maghala ya Mazao ya Chakula, yaliyojengwa Wilaya ya Babati.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), Milton Lupa, ilisema mradi utakaozinduliwa unahusisha vihenge vinane vya kisasa ambavyo vina uwezo wa kuhifadhi tani 25,000 za chakula.

"Mradi huo utakaozinduliwa na Mheshimiwa Rais (Samia), umejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 19.359 mpaka kukamilika kwake na utasaidia kuhifadhi tani 40,000 za mazao ya chakula. Mkandarasi aliyetekeleza ujenzi wa mradi huu ni Kampuni ya UNIA Araj Realizacje ya Poland, aliyekuwa akisaidiwa na Mkandarasi Mzawa ELELAH kutoka jijini Arusha. Msimamizi wa utekelezaji wa mradi huo ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA),"alisema.

Katika mradi huo, serikali kupitia NFRA pia imejenga majengo ya utawala, stoo (bohari) na maabara, ujenzi wa barabara za ndani na kusimika mifumo ya kielektroniki.

Aidha, NFRA imesisitiza kuwa vihenge hivyo vitatumia teknolojia ya kisasa, ambapo mahindi yatakuwa na uwezo wa kuhifadhiwa kwa miaka mitano bila ya kuharibika.

Vilevile, alisema mkandarasi kutoka Poland alitoa mafunzo kwa wafanyakazi nchini Poland, kuweka mzani wa kisasa na kununua trekta ya kusomba mizigo.

Kampuni hiyo, ilianza ujenzi huo Desemba 15, 2018 katika Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara. Inaelezwa kuwa mradi huo utahudumia Kanda ya Arusha (Babati) pamoja na Dodoma, Makambako, Mbozi, Shinyanga, Songea, Sumbawanga na Mpanda.

Kwa sasa, uwezo wa NFRA kukidhi mahitaji ya dharura ya chakula kwa miezi mitatu, ni zaidi ya tani 500,000 ukilinganisha na tani 150,000 iliyokuwa inahitajika miaka ya 1992 wakala ulipoanzishwa.

Teknolojia ya vihenge itawezesha wakala kutumia teknolojia ya kisasa, kupunguza gharama za uendeshaji na itawezesha wakala kuhifadhi chakula kwa muda mrefu zaidi, kupunguza upotevu wa zao la mahindi, baada ya kuvuna (posthaverst loss), kuongeza soko la mahindi nchini na kuimarisha usalama wa nafaka inayohifadhiwa kwa kudhibiti sumukuvu (Aflatoxin) kwa mahindi yaliyohifadhiwa.

Baada ya mradi huo kukamilika, NFRA itakuwa imeongeza uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 zaidi, ambapo vihenge vya kisasa vitakuwa vikihifadhi tani 190,000 na maghala tani 60,000, jambo ambalo litakuwa chachu na mafanikio yenye tija katika kuunga mkono juhudi za utendaji wa serikali.



Baadhi ya mabinti wakijifunza kushona nguo katika Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kituo hicho hutoa mafunzo hayo kwa mabinti waliokimbia kutoka nyumbani kwao kuepuka vitendo vya ukatili wa kijinsia. **PICHA: SABATO KASIKA**

## DC ataka watumishi kuchukuliwa hatua

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, amewaagiza viongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida kuwachukulia hatua watumishi wa afya wanaokiuka maadili yao ya utumishi ili iwe funzo kwa wengine.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na watumishi wa hospitali hiyo katika kikao ambacho kililenga kutatua changamoto zilizoko katika hospitali hiyo kwa lengo la kuboresha huduma.

"Ninazo taarifa wapo walinzi wetu ambao wamegeuza geti kuwa sehemu ya biashara kwa kuuzia kinamama wajawazito vifaa vya kujifungulia kwa gharama kubwa kuanzia sasa naagiza tabia hii ikomeshwe mara moja," alisema.

Mwagisa ambaye aliongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, alisema serikali imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaofika kupata huduma za matibabu katika hospitali hiyo.

Alisema wananchi wanahitaji kupokelewa vizuri wanapofika kupata huduma za matibabu lakini inapotokea hawahudumiwi vizuri malalamiko lazima yawepo na hivyo serikali haitasita kuchukua hatua kwa wasiozingatia maadili ya kazi.

Alisema madaktari na wahudumu wa afya katika hospitali hiyo, wanapaswa kuwaelimisha wajawazito wanapokwenda kliniki ya mwisho kabla ya kujifungua kuandaa vifaa ambavyo wanapaswa kwenda navyo siku ya kujifungua ili waviandae mapema kuepuka garama za kununua kwa gharama ambazo si za kawaida.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Fadhili Chimsala, alisema watumishi wanaokiuka maadili ya utumishi watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda, alisema watumishi wa idara ya afya wanapaswa kitambua kuwa hospitali ni kama gereji hivyo wanapaswa kuwahudumia wananchi vizuri ili kusiwe na malalamiko.

# WASH yataka kuendelea kutolewa fedha za maji

**Na Beatrice Shayo**

WADAU wa Maji na Usafi wa Mazingira nchini (WASH), wameiomba serikali kuendelea kutoa fedha za sekta ya maji na usafi, ili kila mwananchi apate huduma bora na kujiepusha kupata magonjwa ya milipuko.

Katika ujumbe wake kuhusu maadhimisho ya kimataifa ya Siku ya Choo Duniani (WTD) nchini Tanzania, Mkurugenzi Mkazi Shirika la WaterAid Tanzania, Anna Mzinga, alisema wanahitajika wabunifu wa kiteknolojia ili wananchi wapate vyoo bora.

Novemba 19 kila mwaka dunia huadhimisha siku ya choo, kwa mwaka huu kauli mbiu ya 'Usafi na maji yatokayo ardhini, tufanye yasiyoonekana kuonekana.

Mzinga alisema mifumo mizuri ya usafi wa mazingira husaidia kuzuia kuenea kwa magonjwa yanayosambazwa na uchafu wa mazingira na kuwalinda walio hatarini zaidi.

Alisema shirika hilo linashiriki ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na kutengeneza mbolea.

"Hii imesaidia wakazi wa Temeke kudhibiti majitaka katika msongamano wa watu na mifereji michache ambao husafisha maji machafu kuwa mbolea."

Aidha, aliiomba serikali na wadau wa maji na usafi wa mazingira kutimiza wajibu wa kuhakikisha miundombinu inayoweza kukabili athari za mabadiliko ya tabia nchi inakuwapo.

"Nitoa wito kwa serikali na wadau wa WASH kuendelea kutekeleza majukumu yao adhimu katika kusaidia jamii zilizo hatarini zaidi kupata huduma bora za usafi wa mazingira ambazo ni salama, zinazotegemewa katika kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa," alisema.

Alisema mwaka 2021, WaterAid Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya walifanya utafiti kuhusu mazingira ya wafanya usafi katika sekta isiyo rasmi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha, wakabaini kuwa wafanyakazi hao wapo katika hatari ya kupata magonjwa.

"Kutokana na mazingira ya kazi yao ya sekta isiyo rasmi, wanafanya kazi chini ya kiwango na kutoa huduma hafifu. Serikali na wadau wanapaswa kuongeza uwekezaji katika seka ya usafi ili kila mwananchi apate maji safi na usafi wa mazingira."

Alisema takwimu zinaonyesha asilimia 33.5 ya makazi ya mijini kwa Tanzania Bara wana vyoo bora, huku vyoo bora kwa vijijini vikiwa ni asilimia 8.9 na kati ya asilimia 70 hadi 80 ya wakazi wa mijini wakikosa miundombinu ya usafi vikiwemo vifaa vya kukusanyia taka.



## Watuhumiwa 2,000 wa dawa za kulevya watiwa mbaroni

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Kudhibiti Dawa za Kulevya nchini kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, imefanikiwa kukamata zaidi ya watuhumiwa 2,000 na kilogramu 11,974 za dawa za kulevya aina mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2021.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya nchini, Gerard Kusaya, alitoa takwimu hizo kwenye mkutano maalum wa kuhamasisha kupunguza athari za dawa za kulevya kwa wanaojidunga na kutumia dawa hizo kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Kamishna Kusaya alisema takwimu hizo zinaonyesha hali ya uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini sio nzuri na kwamba bado mapambano zaidi dhidi ya dawa hizo yanahitajika.

Alisema mafanikio hayo yalitokana na ushirikiano baina ya wananchi na serikali lakini bado unahitajika kwa ili kunusuru taifa na matumizi ya dawa za kulevya ambayo amedai yana athari kubwa kwa Watanzania hasa vijana.

Akifungua mkutano huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema tangu kuanzishwa kwa kliniki ya kuhudumia watumiaji wa dawa za kulevya mkoani humo zaidi ya 473 kati yao wanaume ni 455 na wanawake 18.

Hata hivyo, aliliagiza Jeshi la Polisi kitengo maalum kinachoshughulikia mapambano dhidi ya dawa za kulevya kuongeza udhibiti wa uingizwaji wa dawa hizo kutoka nje ya nchi, hususan kwenye mipaka ya Kasumulu wilayani Kyela na Tunduma mkoani Songwe.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la HJFMRI nchini Tanzania, Sally Chalamila, alisema shirika hilo limeamua kujihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kuhudumia warahibu wa dawa hizo kutokana na uhusiano wake na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Alisema taifa haliwezi kutangaza kuwa limetomeza ugonjwa huo ikiwa watu wa makundi maalum wakiwamo warahibu wa dawa za kulevya hawajafikiwa na kusaidiwa kuachana na matumizi ya dawa hizo.

# Taasisi za elimu zatakiwa kuisaidia serikali katika uandaaji wa mitaala

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amezitaka taasisi za elimu nchini kuisaidia serikali kuandaa mitaala bora ya elimu ambayo itawajengea uwezo na ujuzi wanafunzi katika kufikia ndoto zao.

Homera alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya saba ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki (CUCoM) akimwakilisha Waziri wa Elimu, Adolph Mkenda.

Alisema Wizara ya Elimu imeanza mchakato wa kupitia mitaala yote ya elimu nchini kwa ajili ya kuboresha ili kuendana na mahitaji ya sasa na katika kufanikisha upatikanaji wa mitaala safi, lazima taasisi za elimu ziisaidie serikali.

"Wakati tukiendelea kutoa elimu bora kwa wanafunzi wetu ni muhimu pia tusaidie uandaaji wa mitaala mipya ya elimu ambayo itaendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, ni jambo nyeti kwa maendeleo yetu Watanzania," alisema Homera.

Aidha, aliwaasa wanachuo hao kuachana na siasa chafu ambazo zitawaharibia ndoto za maisha yao na badala yake wawe waadilifu, wazalendo, waaminifu, wabunifu na wawajibikaji katika kulitumikia taifa.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha St. Agustino, jijini Mwanza (SAUT), Prof. Costarick Mahalu, alisema mikakati ya chuo hicho ni kutoa elimu bora kwa taifa.

Alisema wataendelea kuisaidia serikali kuboresha sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kuwapatia ujuzi na maarifa vijana wa kitanzania.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikatoliki Mbeya CUCoM, Prof. Romuwald Haule, alisema wataendelea kushirikiana na serikali kuboresha mazingira ya utoaji elimu hapa nchini.

Alisema zaidi ya wanafunzi 700 wamehitimu fani mbalimbali na kwamba wataongeza jitihada ili kupata idadi kubwa ya wanafunzi chuoni hapo.




Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, jana alishiriki kupiga kura ya kumchagua Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Serikali yaombwa kuzipa nguvu sheria usawa kijinsia

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imeombwa kuzipa nguvu sheria zote zinazolinda haki sawa kati ya mwanaume na mwanamke kwa kuhakikisha wanapatiwa huduma zote muhimu kwa kuzingatia usawa.

Mkurugenzi wa Shirika la Freedom House nchini, Daniel Lema, alisema wanaume wanashindwa kudai haki za msingi wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na haki nyingine kwa sababu sheria zilizoko zinampa nafasi zaidi mwanamke.

Alisema hali hiyo inasababisha wanaume kukaa na vitu moyoni kutokana na kukosa msaada wa kisheria na nasaha na hatimaye kufanya maamuzi ambayo yanagharimu maisha yao na wengine.

"Kwa sasa wanaume wanakosa nguvu ya kufanya maamuzi na kuchukua hatua kutokana na sheria zilizoko kutowapa nguvu ya kudai haki zao ikilinganishwa na wanawake ambao wana majukwaa na taasisi mbalimbali za kuwasemea na kuwapatia msaada wa kisheria, tunahitaji na sisi tupatiwe madawati na majukwaa ya kusemea tunayopitia," alisema Lema.

Alisema faida ya kuwapo kwa majukwaa yanayotetea na kulinda haki za wanaume itasaidia kupatikana kwa haki na usawa baina ya mwanaume na mwanamke na pia itapunguza vitendo vya ukatili ikiwamo mauaji, ubakaji ulawiti na vipigo.

Mkurugenzi wa Shirika la Empower Youth Prosperity, (EYP), Ipyana Mwakyusa alisema kongamano la wanaume Mkoa wa Mbeya ambalo limefanyika juzi limetoa nafasi ya kujadiliana masuala mbalimbali yanayowakabili kama ya ukatili wa kijinsia na namna ya kujikwamua kiuchumi.

Alisema zaidi ya wanaume 500 kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa huo walishiriki kongamano hilo na kueleza vikwazo mbalimbali wanavyokabiliana navyo.

Alisema, kwa pamoja wamejadiliana namna ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuiomba serikali kufungua majukwaa mbalimbali ili kuwasaidia wanaume kuwasilisha vikwazo vyao.

Alisema kongamano hilo litakuwa endelevu kwa ajili ya kuwasaidia wanaume kufunguka na kuweka mikakati ya pamoja katika kujiponya na matatizo mbalimbali ndani ya ndoa zao kama vile afya akili.

Sylvester Mwashiuya, Mkurugenzi wa Nasaha Hub, alisema msongo wa mawazo kwa wanaume umechangia kwa kiasi kikubwa kufanya maamuzi ambayo yanagharimu maisha yao na wengine.

Alisema hali hiyo inatokana na kukosa sehemu ya kutoa dukuduku zao na kupata tatizo la afya ya akili ambalo ndilo linaongoza kwa wanaume wengi ambao huchukua uamuzi wa kujitoa uhai.





# RC ataja mbinu kuwanusuru wanawake kiuchumi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyumule, amesema njia pekee ya kuwakwamua wanawake kiuchuni na kuondokana na utegemezi ni kuchangamkia fursa za uwekezaji zinazopatikana mkoani hapa.

Senyumule aliyasema hayo jana kwa niaba ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alipokuwa akifungua kongamano la wanawake na mabinti (Mega Ladies Talk Show) lililofanyika jijini Dodoma.

Aliwataka kuchangamkia na kujitokeza kwenye fursa hizo pale zinapojitokeza ili kujiinua kiuchumi kiroho na kijamii badala ya kuendelea utegemezi ambao umekuwa ukiwasababishia wengi umaskini.

"Niwaombe wanawake wenzangu msiziogope hizi fursa zinazojitokeza kwenye maeneo yetu tunayoishi, zilizoko kwenye sekta mbalimbali kama vile za ujenzi, afya, kilimo, elimu, biashara na ujasirimali," alisema.

Pia aliwataka wanawake hao kuhakikisha wanatumia muda wao pia kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan ili afanye kazi zake kwa misingi ya kiroho na weledi utakaosababisha Watanzania kuendelea kuishi na kufanya kazi kwa amani. Sambamba na hilo, alisema wanawake wanapaswa kuendelea kuwaelimisha watoto wao maadili mema ya kiroho na kijamii ili kuepukana na vitendo viovu ambavyo vimekuwa vikileta picha mbaya katika taifa.

Alisema hivi sasa kuna baadhi ya makundi ya watoto yamejitokeza mitaani kufanya vitendo ambavyo vinavyochafua taswira ya nchi kama vile 'panya road' na hii inaonyesha kuwa wamekosa malezi mema ya kiroho na kijamii.

"Jukumu la malezi mema kwa watoto wetu liko kwa wazazi pande zote, hivyo niwaombe tusiwaache kuwapatia elimu ya kiroho ambao itawasaidia kujiepusha na vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikihatarisha amani," alisema.

Mwandaaji wa kongamano hilo, Mchungaji Josephin Kihonza, akitoa taarifa fupi, alisema lengo la kuwakutanisha wanawake na mabinti ni kuwapatia elimu ambayo itakawasaidia kujifunza kiuchumi, kielimu, kiafya, kiroho na kijamii.

Alisema wanawake wengi bado wana mitazamo ya utegemezi licha ya maeneo wanayoishi kuwa na fursa nyingi zinazojitokeza lakini kutokana na kukosa elimu hiyo, wamejikuta wakizifanya wanaume peke yao.

Kihonza alisema pamoja ushiriki huo pia wanawake hao kupitia kongamano hilo, watakuwa wamepata elimu ya uelewa jinsi ya kujitokeza kwenye fursa mbalimbali hasa za ujasiriamali.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma wakati akitoa taarifa ya kufutwa na kusimamishwa kwa uchaguzi kwenye baadhi ya mikoa kwa madai ya wagombea kutoa rushwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Jiji lamshukuru Rais ujenzi wa madarasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia fedha Sh. milioni 580 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 29 ya shule za sekondari kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa nafasi na katika mazingira bora.

Shukrani hizo zilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alipofanya ziara ya kawaida kutembelea shule ya sekondari Miyuji iliyoko jijini hapo.

"Kwa mara nyingine tunamshukuru sana Rais Samia kwa hili alilotufanyia Jiji la Dodoma, ametufanyia mara ya pili mfululizo kwa elimu ya sekondari.

"Katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma hatutarajii watoto watakaofaulu darasa la saba watapa shida kujiunga na kidato cha kwanza watakuta madarasa yote yapo kamili. Kwa hiyo, Januari ni kuingia darasani na kusoma," alisema.

Mafuru alisema amezunguka baadhi ya shule kukagua hali ya ujenzi wa madarasa unavyoendelea.

"Ndugu wanahabari, mmejionea katika shule hii ya sekondari Miyuji wapo kwenye 'roofing stage'. sisi Halmashauri ya Jiji la Dodoma, ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilitupatia muda wa mwisho kumaliza ujenzi wa madarasa haya Desemba 15 kuwa tumekamilisha ujenzi wa madarasa yote 29.

"Sisi tuliporudi ofisini tukasema hebu tutengeneze programu yetu ya ndani ili tuwe na muda wa kutosha kufanya marekebisho pale yatakapohitajika. Nimeongea na Mwalimu Maige na mafundi hapa tunakabidhiwa madarasa haya ndani ya mwezi Novemba," alisema Mafuru.

Akizungumzia kasi ya ujenzi huo kwa shule nyingine zinazotekeleza ujenzi wa madarasa hayo alisema kuwa inaendelea vizuri.

Akitoa maelezo ya mradi wa ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Miyuji, Mkuu wa Shule hiyo, Greyson Maige, alisema walipokea Sh. milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na ofisi moja.

# Aonya matumizi holela dawa chanzo usugu wa magonjwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalage, amesema usugu wa vimelea dhidi ya dawa za antibayotiki unaliweka taifa katika shaka kubwa ya kupoteza nguvu kazi kutokana na kuongezeka kwa magonjwa sugu yasiyotibika kwa kutumia dawa zilizoko.

Aidha, amesema ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 inaonesha kuwa nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, zinaathirika zaidi. Kutokana na usugu huo, amesema takribani dola za marekani bilioni tisa zitatumika kila mwaka kupambana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa hizo ifikapo 2030.

Dk. Shekalage alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma alipokuwa akisoma tamko la Katibu Mkuu Wizara ya Afya kuhusu wiki ya kampeni ya kuzuia usugu wa vimelea dhidi ya dawa za antibayotiki iliyoanza jana hadi Novemba 24, mwaka huu.

"Usugu wa vimelea dhidi ya dawa hizi utachangia kuongezeka kwa umaskini kutokana na kuugua kwa muda mrefu na kutumia dawa za bei ghali zaidi na pia kuongezeka kwa vifo vya mifugo na uzalishaji hafifu wa chakula na kuigharimu nchi mamilioni ya fedha ambazo zingeweza kutumika kuliletea taifa letu maendeleo.

"Ripoti iliyotolewa na Benki ya Dunia mwaka 2017 imeonesha kuwa ifikapo mwaka 2050 uchumi wa dunia utapungua kwa asilimia 3.8 na kwamba kiasi cha dola za Marekani trilioni 3.4 zitapotea ifikapo mwaka 2030 kutokana na tatizo hilo," alisema.

Alisema Tanzania kama ilivyo kwa nchi zingine zinazoendelea, inakabiliwa na magonjwa ya kuambukizwa kwa asilimia 95.

Alisema kutokana na baadhi ya watumishi kutopenda kutumia huduma za maabara, imesababisha wagonjwa wengi kutibiwa bila kupata uhakiki wa majibu kutoka maabara.

"Hali hii imesababisha matumizi yasiyo rasmi ya antibiotiki ambayo husababisha usugu wa vimelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Mfano mwaka 1993 matumizi yalikuwa asilimia 39 mwaka 2002 asilimia 42, 2014 asilimia 67.7 na 2017 hadi 2022 wastani wa asilimia 65," alisema.

Pia alisema utafiti uliofanyika mwaka 2018, ulionyesha kuwa asilimia 90 ya wafugaji wanatumia dawa za antibaiotiki kutibu wanyama badala ya chanjo.

"Takwimu hizi ni kiashiria tosha kwamba ongezeko la AMR ni kubwa na tunahitaji kufanya juhudi za makusudi ili kuweza kujinasua. Umuhimu wa dawa za antibiotiki katika maisha yetu unajidhihilisha wazi tukirejea historia ya uvumbuzi wake.

"Kati ya wagonjwa 100, waliougua nimonia (homa ya mapafu) au maambukizi ya vidonda wagonjwa 90 waliokuwa wakifariki dunia. Uvumbuzi wa antibiotiki ya kwanza aina ya penicillin ulibadili hali na kupunguza vifo hadi kufikia vifo 10 kati ya wagonjwa 100," alisema.

Alisema matumizi mabaya ya dawa jamii ya penicillin yameshasababisha dawa hiyo kujenga usugu kiasi kikubwa.

Dk. Shekalage alisema njia nzuri na rahisi kuzuia na kutokomeza usugu wa vimelea dhidi ya dawa ni kwa jamii na wataalamu wa sekta ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira kutimiza wajibu wao katika kuhakikisha kuwa dawa sahihi inatolewa na kutumika tu pale inapohitajika.

Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, alisema mbinu sahihi ya kukabiliana na tatizo la matumizi holela ya dawa za antibiotiki ni jamii kupatia elimu ya kutosha kuhusu madhara yanayoweza kujitokeza.



## Mwinyi ataja manufaa ubalozi mdogo UAE

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hatua ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kufungua Ubalozi mdogo Zanzibar, itaendeleza kasi katika kukuza uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Konseli Mkuu wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Saleh Ahmeid Alhemeir, aliyefika kwa ajili ya kujitambulisha.

Hatua ya nchi hiyo kufungua Ubalozi mdogo Zanzibar, alisema itatoa msukumo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoanzishwa na ile inayolengwa kuanzishwa siku za usoni.

Alisema ni matarajio yake kuwa kupitia Konseli Mkuu Alhemeir, miradi mbalimbali inayotekelezwa na nchi hiyo kupitia taasisi na mashirika ya fedha ya nchi hiyo itafanikishwa.

Naye Alhemeir alisema hatua ya UEA kufungua ubalozi mdogo Zanzibar itaaongeza kasi ya ushirikiano, hivyo akaahidi kufuatilia miradi mbalimbali ambayo nchi hiyo imelenga kuisaidia Zanzibar.

Pia alisema atahakikisha anasimamia kikamilifu ujenzi wa Ofisi za Ubalozi mdogo wa nchi hiyo visiwani humo.

**Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Konseli Mkuu wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Saleh Ahmeid Alhemeir, aliyefika kwa ajili ya kujitambulisha.**

# Masauni awaonya watendaji Uhamiaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amewaonya watendaji wa Idara ya Uhamiaji kuhusu tabia ya kuchezea mifumo ya kielektroniki ambayo huchelewesha ufanisi wa kazi na kusababisha urasimu ikiwamo katika masuala ya uwekezaji.

Akizungumza jana visiwani hapo wakati akifungua mkutano wa idara za uhamiaji, masauni alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika kuweka mifumo ya kielektroniki kwa lengo ni kuharakisha utendaji wa kazi na kuleta ufanisi katika kushughulikia na kutoa huduma kwa wakati.

Masauni alisema baadhi ya watendaji wamekuwa wakifanya vitendo vya hujuma vyenye mwelekeo wa kukwamisha juhudi hizo huku vikiwamo viashirikia vya rushwa.

"Kitendo cha watumishi wa uhamiaji kuchezea mifumo ya mawasiliano hakivumiliki. Acheni kuchezea mifumo ambayo serikali imetumia fedha nyingi kuiweka," alisema.

Pia aliitaka idara hiyo kuongeza utendaji katika kufuatilia na kudhibiti matukio ya usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na watu wanaoingia nchini kinyume cha sheria na kufanya uhalifu.

Alisema wakati serikali zote mbili zimejipambanua katika sekta ya uwekezaji katika utekelezaji wa miradi mbalimbali mikubwa masuala ya kudhibiti uhalifu ni muhimu.

Naye Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alisema lengo la mkutano huo ni kuwakutanisha wadau mbalimbali wanaofanya kazi kwa pamoja na Idara ya Uhamiaji ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili na kuleta ufanisi.

Alisema Idara ya Uhamiaji katika utekelezaji wa majukumu yake, hufanya kazi na wadau mbalimbali maalumu ili kuharakisha utendaji na majukumu yao kwa pamoja na kuleta ufanisi.

Dk. Makakala aliwataja baadhi ya wadau wanaofanya kazi nao kuwa ni taasisi za kamisheni ya kazi ambazo hujishughulisha na utoaji wa vibali kwa wageni. Ili kufanikisha wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza ushirikiano wa pamoja unahitajika.

"Huu ni mkutano muhimu ambao huwakutanisha wadau wetu muhimu tunaofanya kazi kwa pamoja katika sekta mbalimbali ikiwamo masuala ya utoaji wa vibali vya kazi na uwekezaji," alisema.

Kamishna wa Kazi Zanzibar, Rashid Khamid Othman, alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa utasaidia na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili ikiwamo vibali kwa wageni pamoja na wawekezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati.

"Ziko changamoto katika masuala ya utoaji wa vibali kwa watendaji wa Kamisheni ya Kazi pamoja na Idara ya Uhamiaji na wawekezaji ambazo tunahitaji kuzifanyia kazi," alisema.

Naye Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Hassan Ali Hassan, alisema watautumia mkutano huo pamoja na kupokea changamoto mbalimbali ambazo zitakuwa mwongozo katika utekeleza wa majukumu yao na kuongeza ufanisi katika kutekeleza mikakati ya serikali ya huduma bora.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na mgeni wake Balozi Mdogo wa Umoja wa Falme za Kiarabu Zanzibar (Konseli Mkuu), Saleh Ahmed Al Hemeiri, alipofika Ikulu jijini Zanzibar kujitambulisha. **PICHA: MPIGAPIGA WETU**

# UNESCO yatia mkono mapambano mimba utotoni, ukatili wa kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, limezindua programu ya stadi za maisha kwa walimu wa shule za msingi na sekondari ili elimu hiyo kuitoa kwa wanafunzi shuleni.

Mathias Luhanya, mtaalamu na mratibu wa programu za elimu ya afya na ustawi wa UNESCO, aliyasema hayo juzi visiwani Zanzibar, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa mwongozo wa kuwafundisha walimu stadi za maisha zikiwamo afya, Ukimwi, uzazi na kukabiliana na udhalilishaji wa kijinsia.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, alisema wanazifanyia kazi changamoto ambazo zinawafanya watoto washindwe kufikia malengo yao ndiyo maana wamezindua programu hizo.

Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni mimba za utotoni na utoro shuleni, vinavyosababishwa na uhusiano na wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo huku akibainisha kuwa lengo la programu hizo ni kuwajengea walimu maarifa na mitazamo chanya ya kuwaelimisha wanafunzi ambao wanakumbana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, walimu pia ni wazazi, hivyo ni muhimu kuwa na uwezo wa kuelewa pale mtoto anapokumbana na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema elimu ya afya ya uzazi kwa watoto ni muhimu ili kuepukana na mimba za utotoni na kwamba watoto wengi wanakatisha masomo kutokana na mimba hizo.

"Ni bora kuwakinga wasipate mimba na wakipata tupambane kuwarejesha shuleni, hivyo ni vyema kujiepusha na kujamiiana wakiwa shuleni," alisema.


Alisema mimba za utotoni ni changamoto na Tanzania Bara wastani wa watoto 600 kila mwaka wanaacha shule licha ya tamko na nia nzuri ya Rais Samia Suluhu Hassan watoto waliopata mimba warudi shule bado wanaipoteza fursa hiyo.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Mtopepo, Sabiha Hassan Chum, alisema mwongozo huo ni muhimu kwa kuwa unakwenda na wakati wa matukio yaliyopo sasa ya kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike na wengine kulazimika kuacha shule.

"Mwongozo huu sasa utatuwezesha sisi walimu kusomesha masomo ya stadi za maisha kwa kufuata sheria zinazokwenda na wakati wa matukio," alisema.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, alisema kuwapo kwa mwongozo wa ufundishaji wa masomo ya stadi za maisha ni muhimu kwa kuwa utawawezesha wanafunzi kujiepusha na majanga yakiwamo vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na mimba za utotoni.

Alisema wanafunzi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika kupiga hatua kubwa ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu.





# RAS awa mbogo hati chafu AMCOS

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Siza Tumbo, amevitaka Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), kuongeza ufanisi katika utendaji wao wa kazi na kuondokana na hati chafu zinazosababishwa na kukosekana kwa utunzaji wa taarifa sahihi za wakulima na risiti za malipo.

Tumbo alisema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akifungua mafunzo ya uandishi wa vitabu kwa vitendo kwa makatibu wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) mkoa wa Shinyanga ili kuwajengea uwezo kwenye utendaji wao wa kazi. Alisema katika ukaguzi uliopita kati ya vyama vya msingi 237 vilivyokaguliwa, vyama saba pekee ndiyo vilipata hati safi, 57 hati ya mashaka na 176 hati chafu sababu zikiwa kutotunza taarifa vizuri na kutaka hilo lisijirudie bali wawe makini katika utendaji kazi wao kazi.

"Vyama vya msingi vya ushirika uwekaji taarifa zenu haupo sawa. Uwekaji risiti haujakaa sawa, uwekaji taarifa za wakulima bado haupo vizuri pia, hivyo tumieni mafunzo haya kupata ujuzi ili mkabadilishe namna ya utunzaji taarifa. Mnapewa hati chafu siyo kwamba mmekula pesa lakini kumbe taarifa tu hazipo sawa," alisema Tumbo.

Naye Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga (SHIRECU), Kwiyolecha Nkilijiwa, aliwataka watendaji wa AMCOS kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuhakikisha taarifa zao zinakuwa sahihi, kama ilivyo SHIRECU kwa sasa ambako hakuna tena mambo ya ajabu wala wizi wa mali za ushirika.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa watendaji wa vyama vya msingi vya ushirika ili kuwajengea uwezo namna ya utunzaji wa taarifa zao.

Alisema matarajio ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) baada ya mafunzo hayo ni kuona kunakuwa na uandishi mzuri wa vitabu na utunzaji wa taarifa vizuri kwenye AMCOS na kusiwapo tena na hati chafu wala zenye mashaka.



Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akionesha silaha mbalimbali zikiwamo mbili za kivita Ak 47 walizozikamata katika matukio ya uhalifu na zingine 30 ambazo zimesalimishwa na wananchi kufuatia agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Camilius Wambura. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Aacha shule, akimbilia kilimo cha tikiti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

AMANI Ikumbi mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Nyikoboko iliyoko Kata ya Shilela Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, amedaiwa kuacha masomo yake na kwenda kujihusisha katika kilimo cha matikiti maji ili kujiongezea kipato kwa madai kile anachofundishwa darasani hakielewi.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Mtendaji wa Kijiji cha Shilela, Shimizi Ngeleja, wakati wanafunzi 75 wa kiume wa sekondari ya Nyikoboko na Shule ya Msingi Shilela wakipewa elimu ya ukatili wa kijinsia na njia zake na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) yaliyofanyika katika shule hiyo.

Alisema mwanafunzi huyo alihitimu elimu ya msingi mwaka 2019 katika Shule ya Msingi Shilela na kufaulu vyema akajiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Nyikoboko mwaka 2020 lakini baadaye aliacha shule kwa madai anachofundishwa darasani hakielewi na kutaka kilimo pekee.

Ngeleja alisema taarifa hizo baada ya kuzipata kupitia kwa walimu wake na wazazi walilazimika kukaa naye na kumshauri ili aendelee na masomo lakini ilishindikana na kumpeleka kituo cha polisi kwa hatua zaidi ili kujua pia kama atakuwa anatumia dawa za kulevya hususani bangi.

Aliendelea kusimulia kuwa licha ya kumfikisha kituo cha polisi, bado aliendelea na msimamo wake wa kuacha shule na kujihusisha na kilimo na alidai akitolewa katika kituo hicho na wakiendelea kumlazimisha, atajinyonga hali ambayo ilifanya wakamuacha na sasa ni mkulima.

Hata hivyo, aliwataka wanafunzi kuacha kuiga tabia hiyo na badala yake waendelee na masomo yao na kujitengeneza maisha yao mazuri ya baadaye kwa kuwa hata wakihitimu elimu wana uwezo wa kujihusisha katika kilimo chenye tija na kujiingizia kipato.

Naye Mwalimu wa taalumu katika shule hiyo ya sekondari, John Banda, alielezea tukio la mwanafunzi huyo kuacha masomo na kujihusisha na kilimo cha matikiti maji na walijitahidi kuhakikisha anaendelea na masomo kwa kushirikiana na serikali ya kata lakini ilishindikana.

Alisema kwa sasa wameweka utaratibu wa kukutana na wanafunzi wao kila mwezi na kuzungumza nao ili kusikiliza changamoto wanazokutana nazo na kuzitatua likiwamo suala la kuwasisitiza kuendelea na masomo na wasiinge tabia ya mwanafunzi huyo ambayo inavunja ndoto za wanafunzi.

Mmoja wa wanafunzi wa sekondari ya Nyikoboko, Joseph Masanja, alisema kamwe hawezi kufuata tabia ya mwanafunzi huyo aliyeacha masomo na badala yake atahakikisha anahitimu masomo yake na kama suala la kilimo atakifanya kwa kushirikiana na wazazi wake baada ya kuhitimu sekondari.

Mwanafunzi mwingine, Mathayo Kinya, alisema wanafunzi wa kike wamekuwa wakiendelea kukosa masomo kwa kupata ujauzito na huku wakiwa na uwezo mkubwa darasani na kuiomba serikali kutoa adhabu kali kwa watu wanaokuwa sababu ya kukatisha ndoto zao.

# Wananchi wafundishwa matumizi sahihi fedha

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI wahimizwa kushiriki maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha ili kupata elimu ya matumizi sahihi ya huduma za kifedha kuepukana na udanganyifu na utapeli uloibuka kwa kasi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamishna wa Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, alisema wanasisitiza elimu ya fedha kwa sababu ni raslimali muhimu na yeyote anapohitaji kufanya uamuzi kuhusu matumizi ya fedha, kukopa, kuweka akiba, ni vizuri awe amepata elimu na uelewa wa kutosha.

Alisema maadhimisho hayo ya pili kufanyika nchini yalianza jana na yatafikia kilele Novemba 25, mwaka huu kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya fedha.

"Kwa kweli tungependa wananchi wengi zaidi wajitokeze. Haya ni moja ya mambo ambayo tumeweka kama malengo katika mpango mkuu wa maendeleo ya sekta ya fedha ambao tumeuandaa kwa muda wa miaka 10 na tumekusudia kuhakikisha kwamba Watanzania wengi zaidi wanafikiwa na elimu ya fedha," alisema Dk. Mwamwaja.

Aliongeza kuwa ndani ya wiki moja watatoa elimu pamoja na kuwafahamisha wananchi kuhusu wajibu na haki zao pia wao wanakusudia kupata maoni na mawazo mbalimbali ya maboresho kutoka kwa wananchi.

"Hii ni fursa nzuri ya kupata maoni na mawazo yao kuhusu maeneo mbalimbali ya kuboresha pamoja na kutoa elimu. Tunataka kutumia nafasi hii ya kuwa pamoja na wananchi ili kupata maoni na mawazo yao kwamba ni maeneo gani ambayo wanaweza kuyaboresha, hivyo tunayakaribisha mawazo na michango yao," alisema.

Alisisitiza kuwa kiingilio katika maonyesho hayo ni bure pia hata baada ya siku hizo kukamilika bado wataendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali pamoja na kutoa elimu pia baadhi ya huduma za kifedha zitatolewa katika eneo hilo.

Dk. Mwamwaja aliwaomba wananchi walioko katika Mkoa wa Mwanza na jirani kujitokeza kwa wingi kwa kuwa hiyo ni fursa adhimu ya sekta zote za fedha kupatikana katika eneo moja, hivyo kuokoa muda wao pamoja na kupata nafasi ya kutoa kero na maoni katika maeneo mbalimbali ambayo wanahitaji ufafanuzi.

## G7 yaipa neno UN kuhusu Korea Kaskazini

MAWAZIRI wa mambo ya nje wa kundi la mataifa saba yaliyoendelea zaidi kiviwanda (G7) wamesema Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) linahitaji kuchukua hatua muhimu katika kukabiliana na urushaji wa makombora ya masafa marefu unaoendelea kufanywa na Korea Kaskazini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, katika mkutano wa UN uliofanyika jana Marekani iliomba Korea ijadiliwe kutokana na mfululizo wa makombora yaliyofyatuliwa siku za karibuni.

Pia inaelezwa kuwa mawaziri wa Marekani, Japan, Canada, Ujerumani, Uingereza, Ufaransa na Italia, walisema hatua za Korea Kaskazini zinahitaji mshikamano wa pamoja na thabiti wa jumuiya ya kimataifa.

Ilitajwa kuwa Pyongyang ilifanya majaribio siku ya Ijumaa ya kombora la masafa marefu lenye uwezo wa kufika Marekani bara, muda mfupi baada ya kuonya kuhusu majibu makali ya kijeshi kwa Washington kuimarisha usalama wake katika eneo hilo.

Taarifa ya G7, ilisema jaribio la lililofanyika mwishoni mwa wiki lilikuwa kitendo cha kutojali na ukiukaji mwingine wa wazi wa maazimio ya Umoja wa Mataifa.

"Msururu ambao haujawahi kushuhudiwa wa kurusha kombora la balestiki kinyume cha sheria uliofanywa na Korea Kaskazini mwaka 2022 ni tishio kubwa kwa amani na usalama wa kikanda na kimataifa," ilisema G7. **VOA**

# Korti Afrika Kusini yaamuru Zuma kurejea gerezani

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

MAHAKAMA ya Juu ya Rufani ya Afrika Kusini imeamuru Rais wa zamani Jacob Zuma kurejea gerezani baada ya kukubaliana na uamuzi wa awali kwamba ruhusa ya matibabu ilikuwa kinyume cha sheria, huku ikielezwa kuwa haijabainika iwapo atarudi au laa.

Zuma ambaye ana umri wa miaka 80 alihukumiwa kifungo cha miezi 15 mwaka jana kwa kuidharau mahakama kutokana na kukataa kutoa ushahidi wake wakati wa uchunguzi wa ufisadi.

Pia inaelezwa kuwa kufungwa kwake kulisababisha maandamano ya ghasia katika jimbo la Kwa Zulu Natal na maeneo mengine ya Afrika Kusini na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 300.

**Zuma aliachiliwa baada ya kukaa miezi miwili jela, baada ya mawakili wake kubainisha kuwa alikuwa na ugonjwa usiojulikana.**

Zuma aliachiliwa baada ya kukaa miezi miwili jela, baada ya mawakili wake kubainisha kuwa alikuwa na ugonjwa usiojulikana.



Katika uamuzi wa majaji uliotolewa jana, walisema kwamba mamlaka ya magereza inapaswa kuamua ikiwa muda ambao rais huyo wa zamani ametumia kinyume cha sheria nje ya jela unapaswa kuhesabiwa kuelekea kifungo chake au la.

Mawakili wa rais huyo wa zamani walikuwa wamedai kuwa Zuma alihitaji matibabu ambayo yasingeweza kutolewa gerezani na sasa anaweza kupeleka suala hilo katika Mahakama ya Katiba.

"Ni suala la kisheria lakini ambalo limekuwa na athari za kisiasa huko nyuma," walisema.

Aidha, ilielezwa kuwa kuna wasiwasi kwamba kurejea kwake gerezani kunaweza kusababisha kurudiwa kwa machafuko yaliyoonekana Julai. **BBC**



Rais wa Guinea ya Ikweta, Teodoro Obiang, akihutubia katika moja ya mikutano yake ya hadhara. **PICHA: DW**

# Teodoro Obiang atarajiwa kuiongoza tena Guinea

**CONAKRY,** Guinea

RAIS wa Guinea, Teodoro Obiang, anatarajiwa kuendelea kuitawala nchi hiyo ya Ikweta baada ya uchaguzi wa wiki iliyopita, huku wapinzani wakilalamika kuwa ulitokea udanganyifu na ukiukaji wa sheria kwenye uchaguzi huo.

Rais huyo wa Guinea ya Ikweta Obiang (80) ambaye amekaa madarakani kwa miaka 43 muda unaotajwa kuwa mrefu kuliko kiongozi mwengine yoyote barani Afrika, amewania muhula mwingine.

Obiang aliingia madarakani mwaka 1979 baada ya kuuangusha utawala wa rais wa kwanza aliyeingia madarakani tangu nchi hiyo ilipopata uhuru wake kutoka kwa wakoloni wa Uhispania mwaka 1968.

Katika uchaguzi uliofanyika mwishoni mwa juma lililopita, Obiang anatarajiwa kupata zaidi ya asilimia 95 ya kura na hivyo kuendelea na muhula wa sita. Msimamizi wa vituo vya uchaguzi Maria Amparo Se Obama, alieleza kuwa zoezi la upigaji kura lilikwenda salama.

Inaelezwa kuwa mchakato wa kuhesabu kura unaendelea na matokeo rasmi ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani yanatarajiwa kutangazwa siku chache zijazo.

Pia ilibainishwa kuwa wapinzani hawana matumaini ya kuambulia chochote katika uchaguzi huo na tayari wameeleza juu ya kutokea ubabaifu na mizengwe katika zoezi la kupiga kura.

Andres Esono mmoja wa wagombea wawili wa pekee waliochuana na Rais Obiang katika kinyang'anyiro cha urais, alisema anachokifanya kiongozi huyo ni ulaghai mkubwa na mbaya zaidi kuliko wa hapo awali.

Esono aliwaambia waandishi wa habari kuwa chama chake kimepokea malalamiko kutoka sehemu mbalimbali kwenye taifa hilo kwamba wapigakura walilazimishwa kupiga kura zao hadharani badala ya kupiga kwa siri.

Mgombea mwingine ni Buenaventura Monsuy Asumu wa Chama cha Social Democrat Coalition, ambaye hapo awali alikuwa mshirika wa serikali.

Vyama 14 vya upinzani nchini humo vilijiunga kwenye muungano na chama tawala, ambacho mashirika ya kutetea haki za binadamu yanakilaumu kwa ukiukwaji wa haki za binadamu, vitisho, kuwawinda wapinzani, utesaji, kupotezwa kwa watu na ufisadi.

Serikali ya Obiang pia ililaumiwa kwa kuwaandama wanaodaiwa kupanga mapinduzi waliokimbilia katika nchi nyingine na kuwarudisha kwa nguvu nchini Guinea, ambapo walihukumiwa kifo.

Rais Obiang, alisema ana matumaini ya chama chake cha (PDGE) kushinda tena katika uchaguzi huo baada ya kupiga kura pamoja na mkewe, Constancia Mangue de Obiang.

Katika chaguzi zilizopita, Obiang hakuwahi kupata chini ya asilimia 90 ya kura ambapo mgombea Esono alisisitiza kwamba chama tawala kimefanya tena udanganyifu katika uchaguzi wa Jumapili ya wiki iliyopita.

Licha ya utajiri wake wa mafuta na gesi, taifa la Guinea ya Ikweta limo katika hali ya kushangaza ambapo pengo ni kubwa kati ya tabaka la watawala na idadi kubwa ya watu wanaoishi hasa kwa kutegemea kilimo cha kujikimu.

Inaelezwa kuwa familia ya Rais Obiang kwa muda mrefu inatuhumiwa kuishi katika utajiri mkubwa na kutumia fedha kutoka kwenye hazina ya serikali kufadhili mtindo wake wa maisha.

Mtoto wa Rais Obiang, anayeitwa Teodoro Nguema Obiang Mangue, maarufu Teodorin, anatuhumiwa kwa ubadhirifu wa mali za serikali, huku baba yake akimpandisha cheo na kumtangaza kuwa makamu wa rais, huku wadadisi wakitabiri kwamba anaandaliwa kwa ajili ya kumrithi baba yake.

Mahakama ya Ufaransa mwaka jana ilimuhukumu Teodorin kwa makosa ya ufujaji wa pesa na ubadhirifu wa mamilioni ya fedha za umma. Na kwamba alihukumiwa kifungo cha nje cha miaka mitatu na faini ya Euro milioni 30.

Vilevile mahakama hiyo iliagiza kukamatwa mali zake za nchini Ufaransa zenye thamani ya mamilioni ya Euro. **DW**


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**YOSEFA MKUWA** anatangaza kupootea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0217-0003** kilichotolewa na **PERAMIHO GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 1995. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **SO/RB/167/2022**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**IRENE ZUBERI MOHAMED** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP** yenye index namba **S.1136/0508** iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KASANGEZI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIL/RB/426679/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HELENA MICHAEL MHANDO,** Anatangaza kupotelewa kwa Vyeti vya kidato cha nne ,cheti cha kidato cha nne kilichotolewa Baraza la mtihani kupitia shule ya Forest hill secondary mwaka 2004 chenye namba **(S0310/0037),** Cheti cha kurudia mtihani kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia shule ya kigurunyembe secondary mwaka 2005 chenye namba **(P0359/0076).** Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo cha polisi chochote. **DSM/PHQ/RB/449816/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 28 YA 2021**

**LINDA GODLIVING MEENA................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**JULIUS MTETWA..............................................MJIBU MAOMBI**
**RAJAB ALLY MOHAMED....................................MJIBU MAOMBI**
**ABDALLAH MOHAMED.......................................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**JULIUS MTETWA**
**RAJABU ALLY MOHAMED**
**ABDALLAH MOHAMED**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 25/11/2022 mbele ya mwenyekiti R.W Mmbando wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 18 Mwezi November 2022.

R.W.MMBANDO
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa D,SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na..2212/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU YAHAYA NASSORO A MWICHANDE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NASSORO YAHYA MWICHANDE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa mirathi mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 12 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 15 mwezi 11 mwaka 2022

HAKIMU

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**STELLA SAMWELI KAGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.652 DDH.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBA/RB/366955/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JASTINE MANYAKA MAGESA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 667 CCB – TOYOTA CARINA.** Chassis namba **AT2120062817.** Engine namba **SAH3574T0.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/451141/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR-DEAL AUTO PUT LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.562 BKU** CHASSIS NAMBA **MD2H21BZ7GWD93676.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA **YA POLISI MB/RB/300/2016**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ROZINA ARISTARK MBOYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 918 AJU – SUZUKI ESCUDO.** Chassis namba **TD01W210587.** Engine namba **G16A390171.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/PQH/RB/451452/2022.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI

# Harmonize kamalizana na kina Cheed

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Sanaa la Taifa (BASATA), limesema kwamba, limesuluhisha mambo mbalimbali ya wasanii waliotoka kwenye lebo mbalimbali hapa nchini.

Akizungumzia hilo, Katibu Mtendaji wa BASATA, Kedmon Mapana, amesema Harmonize amemalizana na waliokuwa wasanii wa lebo yake ya Konde Music, Cheed na Killy na sasa kila mmoja anaendelea na maisha yake.

Aidha, Mapana amesema suala la Anjella na Lebo ya Konde Music bado halijafikishwa mezani kwao na mara tu litakapofikishwa watalishughulikia.

"Suala na Harmonize na wasanii wake wale wawili (Cheed na Killy), limemalizika vizuri na kila mmoja anaendelea na maisha yake kama kawaida.

"Lakini suala la Anjellah bado halijafika mezani kwetu, tunawaahidi tutalishughulikia haraka iwezekanavyo," alisema Mapana.





# BURNA BOY KOLABO NA DULLY SYKES

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII mkongwe wa muziki wa Bongo Fleva, Prince Dully Sykes, amesema staa wa muziki kutoka Nigeria, Burna Boy alimtuma mtu amwambie kuwa anahitaji kufanya naye 'kolabo', lakini mtu ambaye alipewa 'mdundo' hakuufikisha.

"Na hauwezi amini Burna Boy mwenyewe ndiye aliyetuma mtu aniambie anataka kufanya kolabo na mimi, lakini tatizo ilikuwa ni aliyepewa 'beat' azifikishe kwa Burna Boy ili achague hakuzifikisha, kwa hiyo sikuona lazima ya kulazimisha vitu," alisema Dully.

Mbali na hayo Dully amefunguka kuhusu Burna kutumia kionjo cha wimbo wake wa Handsome kwenye wimbo wa Harmonize Ft Burna Boy na Diamond Platnumz (kainama) na kusema kuwa aliwaruhusu kutumia vionjo vyake kwa upendo kabisa.



# Jux amkana Paula

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Juma Jux, amejibu tuhuma za kuwa na mahusiano na mrembo Paula Kajala baada ya stori hizo kusambaa katika mitandao ya kijamii kuwa wawili hao ni wapenzi.

Jux kupitia kituo kimoja cha redio amefunguka kuwa hana mahusiano kabisa ya kimapenzi na Paula na anamchukulia kama mdogo wake.

"Hapana naweza kusema ni mdogo wangu tu na hata hajawahi kufika nyumbani kwangu, hiyo video sijawahi kuiona kabisa wala sikumbuki ni lini.

"Paula nimeonana naye, mimi huwa nashangaa ni kwa nini wananihusisha mimi ndiye 'nadate' naye mimi nina mahusiano yangu mengine kabisa."



# BONDIA AZINDUKIA HOSPITALINI PAMBANO DAR BOXING DERBY

**Na Saada Akida**

BONDIA Hemed Rashid amepoteza pambano kwa TKO dhidi ya Iman Bariki 'Man Chuga' kutokana na kushindwa kuendelea kupigana baada ya hali yake kubadilika na kukimbizwa hospitali kwa gari maalum ya wagongwa.

**Katika pambano hilo la Dar Boxing Derby lililofanyika Uwanja wa Kinesi, Dar es Salaam, bondia huyo alikimbizwa Hospitali ya Mkoa wa Temeke kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi.**

Hemed alipoteza pambano katika raundi ya nane baada ya kupigwa ngumi mfululizo akiwa ameonekana kuchoka kabla ya mwamuzi kumaliza pambano, hali iliyosababisha kupelekwa kwenye kona yake kwa msaada kabla ya kuanza kutapika, hivyo daktari wa pambano, Khadija Hamisi, kuchua uamuzi wa kumkimbiza hospitali kupitia gari maalum ya wagonjwa iliokuwapo uwanjani hapo kwa huduma ya kwanza.

Kwa mujibu wa taarifa ya daktari huyo, alisema kwa sasa bondia huyo anaendelea vizuri baada ya kumkimbiza kupata huduma katika Hospitali ya Temeke licha ya awali hali yake kuwa mbaya kutokana na kupoteza fahamu.

"Tunashukuru anaendelea vizuri kwa sababu amepatiwa matibabu na hadi sasa bado anaendelea na matibabu, amefanikiwa kuamka na anaongea, alichokuwa analalamika sana ni maumivu ya kichwa licha ya kutapika sana.

"Lakini amepewa rufani ya kwenda Hospitali ya Mwananyamala ambapo tutampeleka kwa ajili ya kufanya vipimo vya CT Scan kwa kuangalia hali ya kichwa ipoje, na vipimo ambavyo alifanyiwa usiku baada ya kufika Temeke anaonekana yupo sawa hivyo kinachotakiwa ni hiyo CT Scan ambayo itafanyika kesho (leo)," alisema Dk. Hadija.

Mabondia wengine waliofanikiwa kushinda katika pambano hilo la Dar Boxing Derby ni Joseph Maigwisa aliyemchapa Ibrahim Tamba, Roja Mjeshi ambaye alimtandika Said Macho, Said Faraji akimchapa Ramadhan Bunju wakati Omary Mpemba akipoteza dhidi ya Hashim Killaga wa Mbeya.

Wengine walioshinda ni Hamad Furahisha, Mariam Macho, Swahibu Ramadhani, Suma Boyka, Dick Zombi, Haruna Ndaro, Grace Mwakamele, huku Peter Tosh akitoka sare na Jackson Malinyingi.

## SAFARI IMEIVA...




Ofisa Mkuu wa tiGO Pesa, Angelica Pesha (kushoto), akikabidhi tiketi ya kwenda Qatar kushuhudia Fainali za Kombe la Dunia kwa muuza kokoto, Simon Meena, baada ya kuibuka mshindi wa Promosheni ya tiGO ya Wakishua Twenzetu Qatar na Hisense, jijini Dar es Salaam juzi, ambapo washindi 50 waliobahatika watakwenda nchini humo kushuhudia fainali hizo zilizoanza juzi kwa wenyeji Qatar kuangukia kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Ecuador. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *'Mayele' mwingine asaka Kiatu Championship*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Fabrice Ngoyi wa Kitayosce, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, amefikisha mabao matano kwenye Ligi ya Chamioship akiwa mmoja wa wachezaji wawili wanaoongoza katika orodha ya wafungaji bora mpaka sasa.

Bao alilofunga Jumamosi dhidi ya Pamba, likiiwezesha timu yake kupata ushindi wa mabao 3-0, limemfanya kufikisha idadi hiyo ya mabao akiwa sawa na Deogratius Kulwa wa Pamba.

Wakati Ngoyi na Kulwa wakiwa na mabao matano, Mkongomani mwingine wa Kitayosce, Evariste Kayembe anafuatia kwa kupachika mabao manne, huku wengine wenye idadi hiyo ni Said Chota wa Gwambina, Jamil Fadhili (Fountain Gate), Edward Songo (JKT Tanzania) na Shaaban Zuberi wa Biashara United.

Emmanuel Mpuka wa KenGold, anawaongoza wenzake wenye mabao matatu, Martin Kigi wa JKT Tanzania na Juma Uledi wa Ndanda FC.

Ligi hiyo iliendelea Jumamosi ikiwa kwenye raundi ya 10 kwa Kitayosce kuifumua Pamba mabao 3-0, Fountain Gate ikikubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa African Sports, mechi ikichezwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Vinara wa ligi hiyo, Maafande wa JKT Tanzania wakazidi kujichimbia kileleni baada ya kuichapa Mbuni FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Aga Khan jijini Arusha na kufikisha jumla ya pointi 25, Transit Camp ikaondoka kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Biashara United.

Kadhalika, Copco ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Pan African kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Green Warriors ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, na Ndanda ikalazimishwa suluhu kwenye uwanja wake wa nyumbani, Nangwanda Sijaona dhidi ya KenGold. Mechi nyingine ni juzi Jumapili ambapo Gwambina ikiwa nyumbani iliichapa Mashujaa mabao 2-1.

## Polisi Z'bar yazidi kutepeta Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UPEPO wa matokeo mabaya umeendelea kuiandama timu ya Maafande wa Polisi baada ya juzi kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Malindi SC katika mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa 13 mechi ikichezwa usiku katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Kwa matokeo hayo, yanaifanya timu hiyo ya Polisi kupoteza jumla ya mechi saba na kutoka sare nne huku ikishinda michezo miwili kati 13 iliyocheza hadi sasa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Mtuli, alisema licha ya kufanya vibaya katika mzunguko huu bado wanayo nafasi ya kurekebisha makosa yao katika mzunguko wa pili baada ya usajili wa dirisha dogo.

Alisema matokeo hayo hayamaanishi alikosea kufanya usajili, bali kufanya vibaya katika soka ni jambo la kawaida pale upepo wa matokeo mazuri unapokuwa hauvumi upande wako.

Alisema wachezaji wa kikosi hicho wanacheza vizuri na wanajituma kwa kufuata maelekezo yote ya mwalimu, lakini kinachotokea ni kuzidiwa mbinu kwa baadhi ya michezo.

"Tunacheza vizuri sana, wachezaji wanajituma ila tu bahati kwa mzunguko huu naona haipo upande wetu, tunajitahidi kuyafanyia kazi karibu mapungufu yote tunayoyaona kwa kila mchezo, ila bado ninamatumaini ya timu yetu kufanya vizuri," alisema.

## Karate kupigwa Desemba Dar

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Taifa ya mchezo wa Karate yanatarajiwa kutimua vumbi Desemba 10 -11, mwaka huu katika Uwanja wa Ndani wa Taifa, Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, mchezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya mchezo huo ambaye ni Msemaji wa Chama cha Karate cha Wanawake Tanzania (Tawoska), Salha Abdallah, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu za Tanzania Bara pamoja na Visiwani Zanzibar.

"Maandalizi yetu yanaendelea vizuri kuelekea kwenye mashindano hayo ambayo yatasaidia kupata wachezaji watakaounda timu yetu ya Taifa ya Karate, hivyo mtu ambaye anataka kujiunga na mchezo huu anaruhisiwa nafasi bado zipo.

"Mchezo huu unasaidia kumfanya mwanamke awe mwepesi vile vile anapunguza mafuta mwilini, hivyo wote wanakaribishwa," alisema.

## ZISIKUPITE

### GORDON ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Tottenham inamfuatilia winga wa Everton na England, Anthony Gordon, mwenye umri wa miaka 21, kabla ya dirisha la usajili la Januari. ***(Football London)***

### CHAMBERLAIN KUONDOKA LIVER

KIUNGO wa kati wa zamani wa England, Alex Oxlade-Chamberlain, mwenye umri wa miaka 29, anatarajiwa kuondoka Liverpool kama mchezaji huru msimu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### JONG AFUNGUKA BARCA

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, amesema klabu hiyo ya LaLiga ilihusika kufichua maelezo ya mkataba wake kwa vyombo vya habari. ***(De Telegraaf, via Mirror)***

### GUERREIRO AZUIWA

KLABU ya Borussia Dortmund haitamuuza mchezaji anayesakwa na West Ham na Leeds United, Raphael Guerreiro, mwenye umri wa miaka 28, kabla ya mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kukamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Bild)***

### LUKAKU KUSHUKA THAMANI

CHELSEA ina wasiwasi kuwa Romelu Lukaku kutocheza kwenye Kombe la Dunia kunaweza kuathiri thamani ya mshambuliaji huyo wa Ubelgiji mwenye miaka 29, watakapojaribu kumuuza baada ya kumaliza mkopo wake wa msimu mzima katika klabu ya Inter Milan. Lukaku ameondolewa kwenye mechi mbili za kwanza za nchi yake. ***(Evening Standard)***

### GARNACHO MKATABA MPYA

KLABU ya Manchester United inakaribia kumpa mshambuliaji kinda wa Argentina, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 18, mkataba mpya wenye thamani ya pauni 50,000 kwa wiki. ***(Daily Star)***

### VAN GAAL NA KUMTAKA MANE

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Lous van Gaal, ambaye sasa ni kocha wa Uholanzi, amesema alitaka kumsajili mshambuliaji wa pembeni wa Senegal na Liverpool, Sadio Mane, 30, wakati alipokuwa Old Trafford. ***(Metro)***

### SUAREZ AIANIKA GREMIO

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool na Barcelona, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 35, alikataa ofa kutoka kwa Gremio kwa sababu raia huyo wa Uruguay atajiunga na klabu ya MLS. ***(Bild)***


### ARNAUTOVIC KAIKATAA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Austria, Marko Arnautovic mwenye umri wa miaka 33, amekataa mara kwa mara kujiunga na Manchester United msimu wa majira ya joto - ingawa familia yake ilimtaka aondoke Bologna. ***(Laola1)***

### ZIYECH KUVUTWA MILAN

AC Milan inafikiria kumchukua kwa mkopo winga wa Chelsea Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29 katika dirisha la Januari mwakani. ***(Corriere Dello Sport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: MJADALA WANGU NA MESSI HAUTAKAA UISHE

### ●●● Hata kama ningeshinda Kombe la Dunia, ungekuwapo...

**DOHA,** Qatar

CRISTIANO Ronaldo anatumaini kuwa anaweza kuwa mtu wa "kumwangalia" Lionel Messi Qatar, lakini haamini kwamba ushindi wa Kombe la Dunia kwa Ureno utamaliza mjadala wa soka wa nani zaidi kati yao.

> **Ronaldo na Messi ndio magwiji wawili wa kisasa wa mchezo huo, huku wafuasi wa kila mchezaji wakidai kuwa wao ndio bora zaidi wa wakati wote.**

Hata hivyo, licha ya mafanikio ya ubingwa wa Ulaya kwa Ureno na ushindi wa mwaka jana wa Argentina kwenye Copa America, hakuna kati yao aliyeshinda Kombe la Dunia.

Ronaldo amevumilia msimu mgumu katika Klabu ya Manchester United, lakini amewasili Qatar akiwa na hali ya kujiamini, hata kama haamini kwamba analolote la kuthibitisha.

"Hata kama ningeshinda Kombe la Dunia, kungekuwa na mjadala huu," alisema.

"Mimi ni mchezaji mwenye tamaa; ningependa kushinda shindano hili, lakini ikiwa sitashinda, bado ninafurahi kwa kila kitu ambacho nimefanya hadi sasa.

"Kama wangeniambia kuwa sitashinda taji tena, ningejivunia nilichofanya. "Kushinda Kombe la Dunia ilikuwa ndoto kwangu; inawezekana, lakini tutaona. Natumai nguvu zote ziko upande wetu."

Ronaldo na Messi ni wapinzani wa muda mrefu, lakini walipiga picha pamoja kwa ajili ya mchezo wa chess katika kampeni ya matangazo ya Louis Vuitton kabla ya fainali hizo.

Kama Ureno na Argentina kila moja itashinda makundi yao, wawili hao hawatakutana uwanjani hadi fainali ya Desemba 18, mwaka huu.

"Ilikuwa ni kampeni ambayo nimekuwa nikifanya, ambayo nimekuwa nikiitaka kwa miaka mingi," alisema Ronaldo.

"Nimetimiza ndoto ya kuweza kuifanya; kila mtu anajua ukuu wa chapa.

"Itakuwa Kombe langu la tano la Dunia. Nina umakini na nina matumaini makubwa kwamba mambo yatakwenda vizuri."

Ronaldo na Messi wamekutana mara mbili pekee katika mechi za kimataifa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 407

MECHI KALI

DODOMA FC
VERSUS
YOUNG AFRICANS

1 | 5.64
X | 3.01
2 | 1.69

PIGA *150*87#


Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CAMAVINGA MATARAJIO KWA MBAPPE KUIBEBA UFARANSA



**DOHA,** Qatar


EDUARDO Camavinga ameuunga mkono Kylian Mbappe kukabiliana na shinikizo lililoongezwa baada ya Karim Benzema kuondolewa kwenye Kombe la Dunia kwa Ufaransa.

Kikosi cha kocha Didier Deschamps kinaanza kutetea taji lao nchini Qatar dhidi ya Australia katika mpambano wa leo Jumanne wa Kundi D, lakini 'Les Bleus' watafanya hivyo bila washambuliaji wawili muhimu.

Christopher Nkunku aliumia goti lake baada ya Jumanne kugongana na Camavinga mazoezini, kabla ya tatizo la paja kwa Benzema kumfanya mchezaji huyo kutoshiriki michuano hiyo.

Ufaransa, ambao tayari hawakuwa na Paul Pogba na N'Golo Kante, bado wana safu nyingi za ushambuliaji huku Mbappe, Antoine Griezmann, Olivier Giroud na Ousmane Dembele wakitarajiwa kuanza. Kiungo wa kati wa Real Madrid, Camavinga anaamini Mbappe ataongeza kasi iwapo Benzema hayupo, ikizingatiwa kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, tayari amezoea kukabiliana na shinikizo la Ufaransa na Paris Saint-Germain.

"Kylian anaweza kufanya hivyo. Amezoea kuwa na kila kitu mgongoni. Amezoea kupokea shinikizo hili," Camavinga alisema.



## *Mendy hatihati kuondoka*

**LONDON,** England

KIPA wa Chelsea, Edouard Mendy, ana wakati mgumu husuan nafasi yake katika kikosi cha kwanza chini ya kocha Graham Potter kwa mujibu wa ripoti.

Mendy alikuwa na mafanikio mazuri Stamford Bridge tangu aliposajiliwa akitokea Rennes mwaka 2020 kwa kitita cha Pauni milioni 22, lakini sasa mambo yamemwendea kombo.

Nafasi ya Mendy kikosi cha kwanza cha Chelsea imekuwa finyu kwa sasa tangu Thomas Tuchel alipofungashiwa virago nafasi yake ikichukuliwa na Graham Potter.

Kipa namba mbili wa 'The Blues', Kepa Arrizabalaga ndiye amekuwa chaguo namba moja la Potter badala ya Mendy baada ya kuumia mguu.

Baada ya kurejea kikosini, Mendy alikosa baadhi ya mechi za hivi karibuni na Kepa akisimama langoni huku hofu ikitanda huenda huo ndio mwisho wa nafasi yake kikosi cha kwanza.

Wakati huohuo taarifa zimeripoti Potter ameanza kumnyemelea kipa wa Brighton, Robert Sanchez, aliyemfundisha wakati alipokuwa huko kabla ya kujiunga na Chelsea.

,110,340

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/11/22 | 19:00 | Mexico vs Poland | 2.74 | 2.99 | 2.69 |
| 02. 22/11/22 | 22:00 | Forest Green vs Cheltenham | 2.30 | 3.60 | 2.58 |
| 03. 22/11/22 | 22:30 | Grimsby vs Accrington | 2.65 | 3.80 | 2.38 |
| 04. 22/11/22 | 22:30 | Salford City vs Bradford City | 2.42 | 3.65 | 2.42 |
| 05. 22/11/22 | 22:45 | Crawley Town vs Gillingham | 2.37 | 3.11 | 2.97 |
| 06. 22/11/22 | 22:45 | Linfield Belfast vs Larne | 2.84 | 3.28 | 2.37 |
| 07. 22/11/22 | 22:45 | AFC Wimbledon vs Sutton United | 2.42 | 3.65 | 2.42 |
| 08. 23/11/22 | 02:30 | Deportivo Pasto vs America De Cali | 2.61 | 2.94 | 2.65 |
| 09. 23/11/22 | 18:00 | Farco FC vs Ismaily SC | 2.93 | 2.68 | 2.78 |
| 10. 23/11/22 | 22:30 | Port Vale vs Barnsley | 2.45 | 3.53 | 2.45 |
| 11. 23/11/22 | 22:30 | Colchester vs Bristol Rovers | 2.79 | 3.79 | 2.28 |
| 12. 25/11/22 | 13:00 | Wales vs Iran | 2.31 | 3.00 | 3.30 |
| 13. 25/11/22 | 16:00 | Qatar vs Senegal | 4.90 | 3.55 | 1.71 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 22/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4302 | Argentina vs Saudi Arabia | 1.15 | 6.99 | 17.97 |
| 13:00 | 5260 | Alashkert Martuni vs Pyunik Yerevan | 2.47 | 2.95 | 2.81 |
| 14:00 | 2033 | Shijiazhuang vs Dalian Aerbing | 2.25 | 3.32 | 2.83 |
| 14:00 | 3562 | CS Maritimo U23 vs FC Vizela U23 | 2.41 | 3.55 | 2.48 |
| 14:30 | 1137 | Shenzhen vs Guangzhou Evergrande | 2.10 | 3.31 | 3.11 |
| 14:30 | 4488 | Henan Jianye vs Wuhan Zall | 1.31 | 4.86 | 7.58 |
| 14:30 | 5369 | Hangzhou NG vs Shanghai SIPG | 4.68 | 4.00 | 1.57 |
| 15:00 | 3264 | Ural Yekaterinburg vs CSKA Moscow | 3.16 | 3.45 | 2.03 |
| 15:00 | 4765 | Bkma Yerevan vs Ararat Armenia | 7.80 | 4.39 | 1.34 |
| 16:00 | 2413 | Gasogi United vs Sunrise | 2.00 | 2.87 | 3.99 |
| 16:00 | 2717 | Mekelakeya vs Sidama Bunna SC | 2.44 | 2.83 | 2.97 |
| 16:00 | 3505 | Denmark vs Tunisia | 1.46 | 4.09 | 7.18 |
| 17:00 | 2697 | Urartu vs Ararat Yerevan | 1.55 | 3.70 | 5.45 |
| 17:30 | 4034 | FK Khimki vs Nizhny Novgorod | 2.78 | 3.07 | 2.42 |
| 19:00 | 1328 | CD Marino vs CD Mensajero | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 19:00 | 4988 | Dodoma FC vs Young Africans | 5.64 | 3.01 | 1.69 |
| 19:00 | 5638 | Mexico vs Poland | 2.71 | 2.91 | 2.81 |
| 20:00 | 5592 | Torpedo Moscow vs Sochi | 3.64 | 3.50 | 1.85 |
| 22:00 | 1098 | Burton vs Tranmere | 2.04 | 3.31 | 3.26 |
| 22:00 | 1319 | Stevenage vs Arsenal U21 | 2.17 | 3.60 | 2.77 |
| 22:00 | 1379 | Wolverhampton U21 vs Manchester United U21 | 2.73 | 3.51 | 2.23 |
| 22:00 | 1622 | Forest Green vs Cheltenham | 2.15 | 3.30 | 3.01 |
| 22:00 | 2066 | Plymouth vs Charlton | 2.34 | 3.60 | 2.53 |
| 22:00 | 4506 | France vs Australia | 1.27 | 5.41 | 10.02 |
| 22:00 | 4839 | Lincoln vs Morecambe | 1.97 | 3.69 | 3.11 |
| 22:00 | 4895 | MK Dons vs Newport | 1.77 | 3.51 | 3.99 |
| 22:30 | 1981 | Salford City vs Bradford City | 2.31 | 3.40 | 2.67 |
| 22:30 | 3696 | Peterborough vs Chelsea U21 | 1.61 | 3.89 | 4.47 |
| 22:30 | 5794 | Grimsby vs Accrington | 2.38 | 3.51 | 2.53 |
| 22:45 | 1971 | AFC Fylde vs Boston Utd | 2.04 | 3.30 | 3.25 |
| 22:45 | 2175 | Coalville Town vs Mickleover Sports | 2.23 | 3.73 | 2.61 |
| 22:45 | 2321 | Curzon vs Blyth Spartans | 1.98 | 3.40 | 3.31 |
| 22:45 | 2597 | Telford vs Kidderminster | 3.16 | 3.35 | 2.06 |
| 22:45 | 2698 | Halifax vs Dorking Wanderers | 1.85 | 3.79 | 3.55 |
| 22:45 | 2841 | Poole Town vs Truro City | 3.45 | 3.84 | 1.82 |
| 22:45 | 2860 | Oxford City vs Dartford | 2.53 | 3.31 | 2.48 |
| 22:45 | 2880 | Nuneaton vs Basford United | 1.80 | 3.65 | 3.70 |
| 22:45 | 3107 | South Shields vs Bamber Bridge | 1.52 | 4.29 | 4.78 |
| 22:45 | 3229 | Rushall Olympic vs Tamworth | 2.86 | 3.59 | 2.12 |
| 22:45 | 3879 | Plymouth Parkway vs Dorchester Town | 1.99 | 3.85 | 2.97 |
| 22:45 | 3902 | Farsley Celtic vs Chester | 2.97 | 3.41 | 2.13 |
| 22:45 | 4217 | Hyde United FC vs Lancaster City | 1.45 | 4.49 | 5.27 |
| 22:45 | 4438 | Bolton vs Barrow | 1.61 | 3.89 | 4.47 |
| 22:45 | 4726 | AFC Wimbledon vs Sutton United | 2.23 | 3.51 | 2.73 |
| 22:45 | 4742 | Stratford Town vs Redditch United | 2.67 | 3.59 | 2.23 |
| 22:45 | 4885 | Ipswich vs Portsmouth | 1.89 | 3.46 | 3.55 |
| 22:45 | 5512 | Crawley Town vs Gillingham | 2.32 | 3.16 | 3.01 |
| 22:45 | 5732 | Stourbridge vs Hednesford Town | 1.67 | 3.74 | 4.27 |
| 22:45 | 5882 | Linfield Belfast vs Larne | 3.06 | 3.20 | 2.17 |
| 23:45 | 3610 | FC Vizela vs GD Chaves | 2.09 | 3.26 | 3.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM YATAKA 'PIRA BIRIANI'

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuichapa Namungo FC bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Majaliwa, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kalimangonga Ongala, huo ukiwa ni mchezo wake wa sita mfululizo kushinda kwenye ligi hiyo, amesema sasa anataka kukitengeneza kikosi chake ili kiwe kinatawala mechi, kucheza soka safi na kumiliki mpira muda mwingi.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo, Kally alisema wamepata ushindi na pointi tatu muhimu, lakini walikuwa kwenye presha kubwa hasa kipindi cha pili wakati wapinzani wao wakisaka bao la kusawazisha.**

"Kwenye mechi hii tulibadilsha mfumo kuendana na Namungo walivyo, na nadhani tumeweza kufanikiwa, tumepata pointi tatu muhimu hilo, lakini mimi binafsi huwa napenda kuitawala mechi, inatakiwa sasa tuwe tunamiliki mpira kwa kiasi kikubwa, Azam ni timu kubwa haitakiwi kushinda kwa presha, ishinde huku inamiliki na kutawala mpira, najua kazi ni kubwa ya kuifanya, hivyo na safari ni ndefu, lakini naamini hapo mbele tutafanikiwa kwa hilo," alisema straika huyo wa zamani wa Abajalo, Yanga na timu hiyo anayoifundisha.

Kuhusu rekodi aliyoiweka ya kushinda mechi sita mfululizo, alisema yeye kama kocha haangalii hilo, badala yake anachokitilia maanani ni timu yake kupata ushindi tu.

"Siangalii rekodi, hizi zinakuja na kuondoka, naangalia timu yangu kushinda na kupata pointi tatu tu basi," alisema.

Akiizungumzia mechi hiyo, alisema baada ya kupata bao alijua kipindi cha pili wapinzani wao watawashambulia kama nyuki kwa sababu hawana jinsi na wapo nyumbani, lakini kwa bahati nzuri waliweza kuhimili na kuondoka na ushindi.

Hii ni mechi ya sita mfululizo kwa Azam kushinda tangu Kally alipopewa jukumu la kukaimu nafasi hiyo kutoka kwa kocha aliyeondoka, Mfaransa Denis Lavagne.

Mara ya mwisho Azam kupoteza mechi ilikuwa ni Oktoba 21, mwaka huu dhidi ya KMC ikichapwa mabao 2-1, na baada ya hapo, Kally alibebeshwa jukumu na kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Simba, Ruvu Shooting, Namungo na Ihefu, ikaichapa Mtibwa Sugar mabao 4-3, na Dodoma Jiji 2-1, hivyo sasa kufikisha pointi 29 kwenye mechi 13 ambazo imecheza mpaka sasa.

**CHA PILI HICHO...**



Mshambuliaji wa Ecuador, Enner Valencia, akiifungia timu yake bao la pili kwa kichwa kwenye mechi ya ufunguzi ya Fainali za Kombe la Dunia 2022 dhidi ya wenyeji Qatar, iliyopigwa juzi nchini humo. Straika huyo anayeichezea Klabu ya Fenerbahce ya Uturuki alifunga mabao yote mawili wakishinda 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yapanga kurudi

INATOKA UKURASA 32

tumekuja na mikakati mingine tofauti na msimu uliopita, tumedhamiria kuonyesha ukubwa na ubora wetu wa awali," alisema Ahmed.

Alisema wataendelea kuwakosa Jimmyson Mwanuke, Israel Mwenda, Peter Banda ambao wako katika matibabu pamoja na Sadio Kanoute ambaye amepewa muda wa kupumzika na kutokana na kuumia mchezo uliopita.

"Kuhusu makocha wawili wapya, Kocha wa Viungo, Kelvin Mandla na wa makipa, Chlouha Zakaria, wataanza kukaa benchi kwenye mchezo wetu dhidi ya Mbeya City baada ya kukamilika kwa vibali vyao vya kazi.

"Suala la kocha mkuu mchakato unaendelea na hivi karibuni tutamtambulisha kwa sababu tunahitaji mwalimu huyo kufika haraka kwa kuwa tayari Selemani Matola ameshaenda kuongeza ujuzi," alisema.

## *Yanga yapania kuishusha*

INATOKA UKURASA 32

"Wapinzani wetu wasitarajie kukutana na mechi nyepesi, tunajua Yanga inacheza vizuri ikicheza nyumbani au ugenini, lakini tumeangalia na kujua ubora wao na mapungufu yao ambayo tutayatumia," alisema Liogope.

Alisema wanataka kuwa na mwendelezo wa ushindi, kwani wametoka kucheza mechi tatu za ugenini na kufanikiwa kupata pointi nne, ikiwamo ya mwisho ambayo waliichapa KMC mabao 2-1.

"Tunatakiwa kujituma, naamini tutapata matokeo mazuri, kikubwa mashabiki wetu waje tu kutupa sapoti kwa sababu tupo nyumbani," alisema.

Dodoma Jiji ipo nafasi ya 15 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi tisa tu.

Michezo
Jumanne Novemba 22, 2022
Nipashe



‘Mjadala wangu na Messi hautoisha’

UKURASA 29

MVUA YA MABAO...



Winga wa England, Bukayo Saka (kulia), akishangilia sambamba na Declan Rice baada ya kuifungia timu yake bao la tatu na la pili kwake dhidi ya Iran kwenye mechi ya Kombe la Dunia nchini Qatar jana. Katika mechi hiyo iliyomalizika kwa England kushinda 6-2, mabao mengine yalifungwa na Jude Bellingham, Raheem Sterling, Marcus Rashford na Jack Grealish. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yapanga kurudi na 12 Dar

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri na kukusanya alama 11 za michezo ya ugenini, Klabu ya Simba imesema wamekwenda Mbeya wakiwa na mkakati mpya wa kuvuna pointi tatu muhimu dhidi ya Mbeya City.

‘Wekundu wa Msimbazi’ hao tayari wamewasili Mbeya na kesho watakuwa na kibarua kigumu katika Uwanja wa Sokoine jijini humo hiyo ikiwa ni mechi yao ya sita kucheza ugenini tangu kuanza kwa msimu huu.

Katika mechi tano ilizocheza ugenini, Simba imevuna pointi nane baada ya kushinda michezo miwili, sare mbili na kupoteza moja.

Mbali na mchezo huo, Simba wana michezo mingine mitatu ugenini dhidi ya Polisi Tanzania, Coastal Union na Kagera Sugar, ambayo wamesema wamejipanga kushinda yote na kukusanya alama 12 kabla ya kurejea Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Ahmed Ally, alisema msimu uliopita walipoteza pointi mbele ya Mbeya City, safari hii wameingia Mbeya na mkakati maalum wa kuhakikisha wanapata alama tatu katika mchezo huo.

Alisema msimu huu wanahitaji kupambana kuhakikisha wanapata pointi 12 katika michezo yote minne, wakianzia na dhidi ya Mbeya City ambao msimu uliopita ulikuwa mfupa mgumu kwao.

“Kikosi cha wachezaji 25 kimeondoka leo (jana) saa 5:00 usiku, tunaenda kusaka alama 12 ugenini, Hii ‘misheni’ inaitwa ‘12 away’, mashabiki wa Simba katika maeneo husika jiandaeni kikamilifu kuipa sapoti timu iweze kuvuna alama tatu kwenye kila mchezo.

“Tunaanza dhidi ya Mbeya City kubeba alama tatu msimu huu, mchezo wetu katika Jiji la Mbeya

INAENDELEA UK. 31

# Yanga yapania kuishusha Azam

## ●●● Kuwakosa nyota watano leo, Dodoma Jiji yawaonya ikiwaeleza wasitarajie...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, leo watakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida kucheza dhidi ya wenyeji Dodoma Jiji FC, huku wakiwakosa nyota wao watano ambao ni Heritier Makambo, Bernard Morrison, Farid Mussa, Stephane Aziz Ki na Djuma Shaaban.

**Itakuwa ni mechi ya 11 kwa Yanga na ya 12 kwa Dodoma Jiji, huku ikitaka kuendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi ya 48.**

Iwapo Yanga, yenye pointi 26 itashinda mechi ya leo, itarejea tena kileleni kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufikisha pointi 29 sawa na Azam FC, lakini itakuwa juu kwa mabao ya kufunga, huku pia ikiwa na mechi mbili mkononi.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Nasreddine Nabi, amesema kikosi chake kilichosafiri hadi mkoani Singida kipo imara kwa mechi hiyo, huku akiusifia Uwanja wa Liti kuwa uko vizuri tofauti na baadhi ya viwanja vingi vya mikoani.

“Tumeangalia afya za wachezaji kuwatoa uchovu ili wakabiliane na mechi hii, lakini tuliiangalia Dodoma Jiji ikicheza na KMC, Dar es Salaam kwa ajili ya mambo ya kiufundi, naamini wachezaji watakaopata nafasi watakwenda kufanya tutakachowaelekeza.

Tutawakosa Makambo, amepata matatizo kwenye mguu atakuwa nje kwa mwezi mzima, mwingine ni Stephano Aziz Ki, anamalizia adhabu yake ya mechi tatu, Bernard Morrison ambaye na yeye amepata matatizo kidogo ingawa tunaamini kuwa si kubwa, Farid na Djuma, hawa hawatokuwapo kwenye mechi,” alisema Nabi.

Kuhusu uwanja, aliwapongeza wamiliki na watunza uwanja huo kwani ameukagua na kukuta uko kwenye hali nzuri.

“Uwanja ni mzuri, tunatoa pongezi, si mzuri sana, lakini ni afadhali kuliko baadhi ya viwanja vingine vya mikoani, wakati mwingine tusiwe watu wa kulaumu tu, inapotokea watu wanafanya vizuri basi napo tusifie,” alisema kocha huyo.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, amesema wamejipanga vizuri kucheza na timu kubwa kama Yanga akiamini mechi itakuwa ni ngumu kwani inacheza na mabingwa watetezi.

“Sisi kama timu, tumejipanga vizuri kwenye mechi dhidi ya Yanga, ni timu kubwa, nzuri na mabingwa watetezi, maandalizi yetu ni mazuri, najua tunakutana na mechi ngumu, sisi pointi tatu ni muhimu kwa sababu hatuko vizuri kwenye msimamo wa ligi, tunacheza nyumbani, najua Yanga ina mashabiki wengi na sisi pia tunao.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >